# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 14 Juni, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka 2018/2019.

Taarifa ya Mwaka ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 *(The Annual Report of the Institute of Finance Management for the Financial Year 2015/2016)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali, swali letu la kwanza kwa siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Omar Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Shangazi.

Na. 433

**Tathmini Kuhusu 10% ya Wanawake na Vijana**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y. MHE. OMAR A. KIGODA)** aliuliza:-

Kumekuwa na utekelezaji hafifu wa kusaidia akinamama na vijana kutoka kwenye ile asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri:-

Je, Serikali ina tathmini yoyote ya jinsi gani agizo hilo limetekelezwa kwa kila halmashauri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hufanya ufuatiliaji na tathmini kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka kuhusu utekelezaji wa agizo la kila Halmashauri kutenga asilimia 10 kwa ajili ya vikundi vya vijana na wanawake. Taarifa za

ufuatiliaji na tathmini ndizo zimesaidia Serikali kubaini changamoto za usimamizi na uendeshaji unaotokana na upungufu wa kisheria, ikiwa ni pamoja na baadhi ya wanufaika wa mikopo kuwa wagumu kurejesha mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 yatakayompa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa nguvu ya kutunga kanuni bora zaidi zitakazolazimisha halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo ya akinamama na vijana, Serikali inaamini taratibu za utoaji wa mikopo hiyo, usimamizi na urejeshaji wake zitakuwa nzuri zaidi ukilinganisha na hali ilivyo sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa, Serikali imenyang'anya vyanzo vya mapato vya halmashauri lakini pia imeshusha asilimia za mazao hasa ya kibiashara kutoka asilimia 5 mpaka 3, hivyo halmashauri nyingi kushindwa kutoa hii asilimia 10. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kusaidia kuongeza ruzuku katika eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa, zipo halmashauri ambazo zinategemea mazao ya kilimo pekee, kwa mfano Halmashauri ya Lushoto, Halmashauri ya Handeni na nyinginezo na zipo halmashauri ambazo zina rasilimali kama madini, hivyo mfuko huu unakuwa hauna ulingano kwa maana kwamba yapo maeneo ambayo wanapata mapato makubwa na mengine wanapata mapato kidogo sana. Hatuoni kwamba kwa kufanya hivi tunaleta misingi ya ubaguzi katika pato la Taifa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza amesema kwamba, kuna baadhi ya vyanzo vya mapato halmashauri zimenyang'anywa. Nataka nimhakikishie kwamba, utaratibu wa Serikali ni mzuri. Katika baadhi ya vyanzo ambavyo vimechukuliwa, kwa mfano, vinavyokusanywa na *TRA,* bajeti ya halmashauri inakuwa iko palepale na baada ya ukusanyaji bajeti ambayo ilitengwa huwa inarudishwa kwa halmashauri. Kuhusu kwamba kwa nini tusiweke ruzuku maalum ili kufidia, nadhani ni wazo ambalo tunaweza tukalifanyia kazi kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili kwamba baadhi ya halmashauri mapato ni kidogo ukilinganisha na halmashauri nyingine. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi na Waheshimiwa Wabunge kwamba katika ukokotoaji ambao tutaufanya hivi karibuni, kama sehemu ya kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kuziangalia hizi halmashauri zetu. Tutaangalia utaratibu ambao ni mzuri zaidi ili kusudi halmashauri ambazo zina uwezo mkubwa na halmashauri ambazo hazina uwezo kabisa tuangalie namna ya kutekeleza agizo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakasaka, Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na taarifa mbalimbali kuhusu baadhi ya halmashauri kutoa mikopo hii ya vijana na akina mama kwa upendeleo. Serikali imewahi kulifanyia uchunguzi jambo hili na inasema nini kuhusu suala hili kama kweli lipo katika baadhi ya halmashauri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi yetu sisi ya Wizara hivi karibuni hatujawahi kupokea malalamiko ambayo ni ya msingi kabisa kutoka katika halmashauri yoyote, kwamba kuna upendeleo katika utoaji wa mikopo. Kwa sababu utaratibu uliopo kila halmashauri inatakiwa iwe na Kamati ya Mikopo ambayo ndiyo hupitisha mikopo ile na miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Mikopo ni Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nijibu tu kwamba, kwa kweli utaratibu uliopo inawezekana kuna baadhi ya vikundi vikawa havijaguswa kwa mwaka ule husika kwa sababu fedha zenyewe zinakuwa hazitoshi, ni kidogo. Kwa mfano, unaweza ukawa na shilingi bilioni moja ukataka kutoa mikopo kwa vikundi 80 katika halmashauri, lakini halmashauri ina vikundi 600 kwa hiyo ni wazi kwamba kuna baadhi ya vikundi vitakosa. Kwa hiyo, jambo la msingi ambalo nataka nishauri halmashauri ni kwamba wasirudie kuvipa mikopo vikundi ambavyo vilipata mikopo mwaka jana na mwaka huu vikapata, bali vipate ambavyo mwaka jana havikupata. Huo ndiyo utaratibu mzuri zaidi na hiyo ni kupitia Kamati ya Mikopo ya Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ilipitisha Sheria Ndogo ya Nyongeza ya Tozo mbalimbali katika Halmashauri na sheria ile ikasainiwa na Waziri mwenye dhamana wa TAMISEMI. Katika hali ya kushangaza, Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi alikuja Kigoma Machi, 2018 na

kutangaza kwamba sheria ile isitekelezwe. Mpaka sasa watendaji wa halmashauri wanaogopa kukusanya ushuru kwa sababu ya agizo la Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi. Serikali inasema nini kuhusu jambo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambazo tunazo katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni kwamba Baraza la Madiwani lilipitisha viwango vya tozo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, hizo taarifa ndizo tulizonazo na hata Mkuu wa Wilaya ya Kigoma anazo taarifa hio na ametuarifu. Kwa hiyo, hizi taarifa ambazo Mheshimiwa Zitto amezileta ni mpya na yeye ni rafiki yangu, hajawahi hata kuja ofisini kuniambia. Kwa hiyo, tutafuatilia baada ya kuwa amezitoa hapa ili tuone zina ukweli kiasi gani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chegeni halafu Mheshimiwa Paresso.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami napenda tu kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa halmashauri nyingi kwa sasa hivi ziko taabani, kwa maana kwamba kimapato nyingi zinasuasua; na kwa kuwa Serikali imeendelea kuchukua baadhi ya vyanzo vingi vya halmashauri na hivyo kufanya halmashauri hizi kushindwa kufanya kazi na kutekeleza majukumu yake kama ilivyotakiwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaamini kwamba kwa mwenendo huu unazidi kuuwa ile dhana ya kugatua madaraka ya *D-by-D*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Chegeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jukumu la msingi kubwa la Serikali ni kusimamia maendeleo ya wananchi wake wote kwa usawa. Kuna baadhi ya halmashauri unaweza ukakuta katika maeneo yao kuna vyanzo ambavyo vinaweza vikawa vinawapatia mapato ambayo kimsingi yakikusanywa kwa asilimia 80 hadi asilimia 100 yanaweza yakatoa mchango mkubwa sana katika pato la Taifa ili kuweza kuligawanya na halmashauri nyingine ambazo zina matatizo ziweze kupata japo kidogo. Kwa hiyo, huo ndiyo msingi wa baadhi ya kodi kuweza kuchukuliwa kukusanywa na *TRA* ili kusudi ule mgawanyo wa mapato kitaifa uweze kuwa mzuri zaidi kwa halmashauri zote au kwa maeneo yote, hilo ndio jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na changamoto ambazo zipo katika halmashauri jambo la kwanza ambalo tumewashauri na Kamati ya Bunge imetoa ushauri ndani ya Bunge hili ni kwamba, kila halmashauri wakae chini katika vikao vyao vya mabaraza watathmini vyanzo vya mapato walivyonavyo kwa sababu halmashauri nyingi tu vipo vyanzo vya mapato ambavyo hawavikusanyi. Kwa hiyo, watathmini vyanzo vya mapato walivyonavyo na wanavyokusanya walete Mheshimiwa Waziri aweze kuwapitishia ili kusudi waweze kuongeza wigo wa mapato. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ambayo yamewasilishwa hapa Bungeni na Serikali muda huu yanaeleza kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI inatengeneza kanuni za kulazimisha halmashauri iweze kutenga hizo fedha kwa ajili ya mfuko huu. Suala si kuwa na kanuni na sheria kali, suala ni kwamba vyanzo vingi vya halmashauri vimechukuliwa na Serikali Kuu hivyo halmashauri inashindwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwapa mikopo wanawake na vijana. Ni kwa nini Serikali sasa, kwanza iache kutengeneza kanuni hizo lakini itenge fedha hizo kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa sababu mapato yote imeyachukua?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Paresso na Bunge lako Tukufu kwamba agizo la kutenga asilimia 10 linahusu makusanyo ya ndani. Kama wamekusanya Sh.100 basi asilimia 10 ya Sh.100 watenge hiyo hiyo. Hatujasema kwamba mtu amekusanya Sh.100 atenge Sh.200, hapana. Amekusanya Sh.100 basi atoe asilimia 10 ya hiyo Sh.100 ili kusudi aweze kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri ambayo imekusanya Sh.100,000,000 inatakiwa itoe Sh.10,000,000 kwa ajili ya vikundi vya vijana na wanawake. Kwa hiyo, kama kuna changamoto nyingine, taratibu za mawasiliano ndani ya Serikali Wakurugenzi wa Halmashauri wanazifahamu sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na

Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa, linaelekezwa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 434

**Hitaji la Vitanda Chuo cha Maendeleo – Kilwa**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA** aliuliza:-

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa kina upungufu mkubwa wa vitanda na hata vichache vilivyopo vimechakaa sana kwani vilinunuliwa tangu mwaka 1969. Mahitaji halisi ya vitanda vinavyohitajika chuoni hapo ni zaidi ya vitanda 50 *(double decker)*:-

Je, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitanda pamoja na samani nyingine chuoni hapo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* kwa ajili ya kuandaa rasilimali watu watakaotumika katika viwanda ili kufikia lengo la Serikali la kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda ifikapo mwaka 2025. Vyuo hivi vitasaidia kuongeza fursa ya mafunzo ya ufundi stadi sambamba na elimu ya wananchi *(folk education).* Aidha, vitasaidia kuwaandaa vijana kwa kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa vyuo hivyo, Serikali imetoa kandarasi kwa vyuo vitatu ambavyo ni Taasisi ya Teknolojia Dar-es-Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili vifanye uchambuzi wa kina wa hali halisi ya miundombinu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, pamoja na samani katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kikiwemo Chuo cha Maendeleo cha Wananchi Kilwa Masoko. Taratibu za ukarabati zitaanza baada ya kukamilika kwa zoezi hili. Aidha, Wizara inafanya zoezi la kubaini mahitaji ya watumishi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, zoezi linalotarajiwa kukamilika Julai, 2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jibu lisilokamilika kutokana na kwamba mimi niliulizia Kilwa lakini amejibu kwa pamoja. Ni lini sasa uchambuzi wa kina na hali ya halisi utakamilika ili vyuo hivyo vipate huduma inayohitajika? Hilo ni swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Chuo cha Maendeleo cha Wilaya ya Kilwa kina mafunzo ya udereva, lakini mpaka sasa hivi hakuna gari la kujifunzia. Ni lini Wizara itapeleka gari katika Chuo cha Maendeleo Wilaya ya Kilwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa kifupi kwa maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bungara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zoezi litakamilika lini, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, zoezi hilo litategemea kukamilika mwezi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chuo kupatiwa gari, kama tulivyosema tunafanya tathmini ya kuangalia vitu vinavyohitajika ikiwa ni pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Kama gari ni moja kati ya vitu vitakavyoonekana kwamba vinahitajika basi Serikali itajipanga ili kuweza kuhakikisha kwamba linapatikana kadri uwezo utakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karagwe ina idadi ya watu wasiopungua 350,000 lakini tuna *A Level* moja tu ya Bugene Sekondari na haina maktaba hata moja, lakini pia ina upungufu wa madarasa yasiyopungua 17. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Bunge hili yuko tayari kuambatana na mimi akajionee hali ilivyokuwa mbaya pale Bugene Sekondari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo la kwenda kutembelea huko, Naibu Waziri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Bachungwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ni kama amewahisha shughuli kwa sababu swali linalofuata linahusiana vidato vya tano na sita. Hata hivyo, mimi sina shida niko tayari kwenda naye jimboni kwake, kuna maeneo maarufu sana nataka nifike kule kama Chamchuzi. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba sina shida na kwenda kwa hiyo tutaongea tuone umuhimu wa kufanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi nami niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo kwenye Chuo cha Maendeleo Kilwa zinafanana kabisa katika changamoto zilizopo katika Chuo cha Bandari kilichopo Tandika pala Temeke ambako chuo hicho kilianza kufundisha wanafunzi kabla hakijapata ithibati, hivyo wanafunzi wote walio-*graduate* kuanzia mwaka 2016 kurudi nyuma hawakupewa vyeti vyao mpaka hivi leo. Jambo hili limezua mtafaruku mkubwa, wanafunzi hawa hawajui hatima yao, wanashindwa kuendelea na masomo zaidi na wanashindwa kupata ajira. Nilitaka kujua kauli ya Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wanafunzi hawa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtolea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema kwamba kuna changamoto katika Chuo cha Bandari. Changamoto hiyo imeshafika Wizarani kwetu na kwa sasa tunaishughulikia na wanafunzi watapatiwa majibu muda si mrefu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi na ninaulizwa kwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia.

Na. 435

**Kila Wilaya kuwa na Shule ya Kidato cha Tano na Sita**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano inatoa elimu bure hali iliyosababisha wananchi wengi kupeleka watoto wao shule, huku ufaulu wa wanafunzi kuingia kidato cha tano ukiongezeka:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kila wilaya kuwa na Shule za Kidato cha Tano na Sita kuwa ni wa lazima hasa ikizingatiwa kuwa kuna baadhi ya wilaya hazina shule hizo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza Shule za Kidato cha Tano na Sita na kuhakikisha zinakuwa kwa kila wilaya hasa wakati huu ambapo wahitimu wa Kidato cha Nne wameongezeka kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Hii ndiyo sababu ya Serikali kuelekeza kuwa na Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita kwa kila tarafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu, Wilaya/ Halmashauri inaweza kuwa na Shule za Kidato cha Tano na Sita zaidi ya moja kutegemea idadi ya tarafa zilizopo. Hivyo, inashauriwa wadau wa Wilaya/Halmashauri ambazo hazina Shule zenye Kidato cha Tano na Sita kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri husika kujenga shule au

kuongeza miundombinu katika shule zilizopo na kufuata taratibu husika kusajili shule mpya iliyojengwa au kupata kibali cha kuanzisha kidato cha tano na sita katika shule zilizopo. Utekelezaji huo utasaidia kuondoa changamoto ya baadhi ya wanafunzi wenye sifa za kuendelea na masomo ya kidato cha tano kukosa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha kwamba Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita ni za kitaifa, ambapo hudahili wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali za nchi kulingana na tahasusi (*combinations*) za masomo zilizopo. Hivyo kwa sasa wahitimu wenye sifa kutoka wilaya zote nchini hupangwa katika shule hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, natambua jitihada za Wizara ya Elimu za kuanzisha Shule za Sekondari za Kata lakini ni ukweli usiopingika kwamba wananchi wengi baadhi ya maeneo wanashindwa kupeleka watoto wao maeneo ya mbali, mfano Jimbo la Kilindi ambako wazazi hawana uwezo wa kupeleka watoto wao kidato cha tano na cha sita. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kushirikiana na halmashauri yetu ambapo tumeshafanya jitihada kubwa kutembelea Shule za Sekondari za Kilindi Girls, Kikunde na Mafisa ambazo tayari zina miundombinu kwa ajili ya kupata sifa ya kuwa na kidato cha tano na sita? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kigua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kama niko tayari katika kutembelea shule za jimboni kwake kama alivyotaja, mimi niko tayari kuzitembelea lakini naomba tu niendelee kusizisitiza kuwa Shule za Kidato cha Tano na Sita ni shule za kitaifa. Kwa hiyo, hata kama tukijenga Kilindi bado haitakuwa kwa ajili ya wanafunzi wa kutoka Kilindi tu, watatoka wanafunzi Tanzania nzima.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya Kilindi yanafanana kabisa na yale matatizo ya shule za Mbagala. Niishukuru Serikali kwa kujenga madarasa mengi katika shule ya Msingi Majimatitu na Mbande. Shule hizi zilikuwa zinaandikisha wanafunzi 6,000 kila mwaka, kwa kweli watoto hawa ni wengi. Je, Serikali haioni haja ya kuandaa shule ya sekondari za *high school* katika maeneo ya Chamazi, Mbande, Nzasa na Charambe katika Jimbo la Mbagala ili watoto wanaomaliza sekondari waende kwenye *high school* maeneo hayo hayo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimekustahi tu kwa sababu wewe ni mtani wangu lakini nilianza na Mheshimiwa Richard Ndassa. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwa halmashauri ambazo zinahitaji kuanzisha Shule za Kitado cha Tano na Sita, utaratibu ni kwamba wao wenyewe wajipange na wajenge miundombinu husika baadaye waombe kibali kutoka Wizara ya Elimu na sisi tutaangalia na tukijiridhisha kwamba inafaa hatutakataa kuzisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba kwa sasa kama kuna changamoto ya wanafunzi wa kutoka Mbagala kuweza kupata elimu ya kidato cha tano na sita karibu bado fursa zipo katika shule nyingine za kitaifa kwa sababu kimsingi kidato cha tano na sita zote ni shule za Kitaifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rishard Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo la Sumve lina shule za sekondari 17 ikiwemo Shule ya Sekondari ya Talo ambayo inazo sifa zote kama vile miundombinu na tumeshaleta maombi Serikalini. Je, ni lini sasa shule hiyo ya sekondari itawekewa kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeendelea kusema kwenye majibu yaliyopita, Wizara ya Elimu ipo tayari kupokea maombi ya kutoka kwenye halmashauri zinazofikiri zinataka shule ziweze kupatiwa ruhusa ya kuendesha kidato cha tano na sita. Sisi tutakachofanya tutaenda kujiridhisha na hali ya miundombinu kuangalia kama kweli kuna mazingira ya kukidhi kuanzishwa kidato cha tano na sita. Kama nilivyosema, lengo letu kama Wizara tunataka angalao tuhakikishe kwamba katika kila tarafa kuwe na kidato cha tano na sita. Kwa hiyo, tukiangalia mazingira kama yanaridhisha sisi hatuna shida. Kwa hiyo, naomba waanze wao walete mapendekezo Wizarani na sisi tutayafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Omar Mgumba.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa elimu ya bure ni kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la kumi na mbili, lakini kidato tano na sita hawamo. Hawa wote ni watoto wa mtu mmoja, kuna sababu gani za msingi *form five* na *six* wakaachwa kusamehewa karo? Naomba Waziri atoe maelezo kwa sababu wote ni watoto wake, kwa nini hawa waachwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema kwamba watoto wote ni watoto wa Taifa hili kwa hiyo haitakiwi kuwa na ubaguzi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali siku zijazo kadri uwezo utavyoruhusu tutatoa elimu bure ikiwezekana mpaka chuo kikuu bure. Kwa sasa, kutegemeana na hali halisi ya kifedha, tutaendelea kwanza kuimarisha miundombinu na mazingira katika shule za ngazi ya elimu msingi, kuanzia shule za awali mpaka kidato cha nne na kuendelea kutoa elimu bure na uwezo ukiongezeka hatuna shida kuongeza kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama mnavyofahamu Serikali inatoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu. Tunatoa shilingi bilioni 427 kila mwaka kwa sasa. Kwa hiyo, anachosema ni kitu cha kweli. Kwa kweli siku zijazo uwezo utakapoongezeka hata kidato cha tano na sita nayo itakuwa ni elimu bure.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgumba.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kwa mujibu wa sera angalau kila tarafa iwe na shule ya sekondari ya kidato cha tano na sita; na sisi Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki tumeshaanza ujenzi huo katika tarafa zote tatu za Mkuyuni Ngerengere na Nelson Mandela. Shule ya Nelson Mandela tulishamaliza bado bwalo kumalizia juu. Je, Serikali iko tayari kutuunga mkono kumalizia bwalo ili mwezi wa saba wanafunzi waanze, ukizingatia mwaka jana zaidi ya wanafunzi 60 wamekosa kwenda katika hizo shule za kitaifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kama Serikali iko tayari kuwaongezea nguvu kukamilisha bwalo na anataka limalizike mwezi wa saba, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na nia ya Wizara ya kuendelea kusaidia ujenzi wa miundombinu bado muda wa matayarisho utakuwa ni muhimu kwa sababu kipindi cha mwezi mmoja kwa kweli kina changamoto katika taratibu za kawaida za kupata fedha. Hata hivyo, halmashauri yake walete mapendekezo na sisi tutajipanga ili tuweze kuwasaidia katika mipango mingine ijayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei Massay, Pauline Gekul na Mheshimiwa Halima Bulembo.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Mbulu Vijijini na Halmashauri ya Mbulu tumejenga Shule ya Kidato cha Tano na kila kitu tayari na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI amekuja kuigagua. Tumetuma maombi na Naibu Waziri anafahamu tunahitaji kuianzisha mwaka huu na kila kitu tayari. Je, kibali hicho kinatoka lini ili mwaka huu watoto hawa waingie shuleni na kusaidia Tanzania ya elimu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia sana kuhusu shule anayosema na ombi lao liko mezani kwenye Wizara yetu. Naomba tu nimhakikishie kwamba tutalishughulikia mapema iwezekanavyo ili ikiwezekana katika mwaka wa masomo unaofuata wanafunzi wa kidato cha tano waweze kuingia katika shule anayosema.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika jimbo letu la Babati Mjini tuna *A – level* moja (Babati Day) lakini Serikali walitupa mwongozo kwamba tutafute *A – level* nyingine na sisi halmashauri yetu tukapendekeza Sekondari ya Kwaangw', Kata ya Maisaka. Mheshimiwa Naibu Waziri anapafahamu sana hapo maana anapita, tukawekeza nguvu zetu zote pale, sasa halmashauri haina vyanzo vya kutosha na *A – level* hiyo inatakiwa ianze mapema. Mheshimiwa Naibu Waziri Serikali sasa iko tayari kutuongezea nguvu ili hiyo sekondari ya *A – level* ianze mapema?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Wizara yetu ambayo Wabunge wametupitishia kwa ajili ya mwaka unaokuja tumetenga shilingi bilioni 168 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika taasisi mbalimbali za elimu kwa ngazi mbalimbali; kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu. Kwa hiyo, Wizara ina fedha za kusaidia ujenzi wa miundombinu. Tunachotaka kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge na mkiwa sehemu ya Mabaraza la Madiwani leteni maombi nasi tukijiridhisha kwamba kuna mahitaji hatutasita kuwasaidia. Kwa hiyo, nimshauri Mheshimiwa Gekul kwamba sisi tuko tayari kupokea maombi yenu lakini leteni kwa taratibu zilizowekwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Bulembo.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** nakurushukuru. Serikali itakubaliana na mimi kwamba sekta binafsi ina mchango mkubwa katika elimu. Mwaka jana wanafunzi takriban 19,000 waliokuwa wanaingia kidato cha tano walikosa nafasi katika shule za Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri, hamuoni imefika wakati sasa kuzipunguzia kodi shule binafsi ili hawa wanafunzi wanaokosa nafasi katika shule za Serikali waweze kumudu ada elekekezi katika shule binafsi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba sekta binafsi ina nafasi nzuri sana katika kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu. Serikali itaendelea kushirikiana nao ili

kuondoa changamoto zinazowakabili ili waweze kuwekeza kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshaondoa tozo na kodi kubwa nne ambazo zilikuwa zinawaletea changamoto. Tupo tayari kujadiliana nayo ili kuangalia ni namna gani tunaweza kuboresha mazingira ili waweze kuwekeza kwa urahisi zaidi.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekondari ya *High School* ya Kaliua inapokea watoto kutoka Tanzania nzima na ina watoto wegi sana lakini kuna upungufu mkubwa sana wa mabweni ya wasichana na wavulana. Pamoja na juhudi za halmashauri za kuendelea kujenga bado mahitaji ni makubwa sana. Serikali iko tayari sasa kupeleka nguvu katika Sekondari ya *High School* ya Kaliua ili watoto wale wapate mabweni ya kutosha kwa sababu hivi tunavyoongea baadhi ya wavulana wanakaa kwenye madarasa kwa kukosa mabweni ya kulala?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo tayari kuangalia uwezekano wa kusaidia kujenga miundombinu katika shule aliyosema. Kama nilivyosema kwenye maswali mengine

tunahitaji kupata maombi, ni lazima halmashauri yenyewe ituletee maombi ili tuangalie ni namna gani tanaweza kusaidia. Kwa hiyo, tuko tayari kujenga miundombinu, tumeshajenga mingi katika nchi nzima lakini tunaangalia vilevile na bajeti. Kwa hiyo, alete maombi yataangaliwa pamoja na maombi mengine.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, linaulizwa kwa Waziri wa kilimo.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali, lakini kabla ya kuuliza swali langu ningependa kupata ruhusa yako ya kuiombea heri na baraka na Mwenyezi Mungu awape subira familia na wananchi wa Wilaya ya Kakonko kwa kumpoteza Mbunge wao, Mheshimiwa Mwalimu Samson Bilago. Mwenyezi Mungu ailaze Roho ya Marehemu mahali pema peponi.

Na. 436

**Kuunda Bodi ya Zao la Mchikichi**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaunda Bodi ya zao la Mchikichi kama ilivyoanzisha kwenye mazao mengine?

(b) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kuhusu kuendeleza zao hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza

Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Na.19 ya Mwaka 2009 ilianzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo ina jukumu la kuhamasisha uzalishaji na kufanya biashara ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko. Kwa sasa Bodi imeanza kufanya biashara ya zao la mahindi na alizeti kwa kununua, kusafisha na kusaga unga wa mahindi na kukamua mafuta ya alizeti. Bodi itakuwa inaongeza mazao mengine kulingana mahitaji, uzalishaji na uwepo wa biashara (*commercial viability*) ya zao husika. Aidha, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa zao la mchikichi katika ukuaji uchumi wa Taifa na kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi itatoa kipaumbele kwa zao hilo ili liweze kushughulikiwa na Bodi hii katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa usimamizi wa mazao ya nafaka na mchanganyiko katika uzalishaji na masoko, Serikali inatarajia kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, kwa maana ya (*Cereals and other Produce Regulatory Authority).* Kwa maana hiyo, mamlaka hiyo itakuwa na jukumu la kudhibiti na kusimamia biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko ili kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo cha mazao husika ikiwemo zao la mchikichi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa zao la michikichi nchini unaratibiwa na Kituo cha Utafiti cha Mikocheni kilichopo Dar es Salaam kwa kushirikiana na Kituo cha Utafiti cha Tumbi kilichopo Tabora. Aidha, Kituo cha Utafiti Tumbi kimeweza kukusanya hifadhi nasaba (*germplasm)* za michikichi iliyoko nchini, wakati Kituo cha Utafiti cha Mikocheni kinatafiti namna ya kuzalisha miche ya michikichi kwa njia ya *tissue (tissue culture*) na baadaye kuisambaza kwa wakulima. Vilevile kituo hicho cha Mikocheni kina mpango wa kuingiza mbegu mama bora toka nje ya nchi na

kuzitathimini ili kuona uwezekano wa uzalishaji wake hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sabreena Sungura.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali inatambua kwamba zao hili la mchikichi nchi yetu iliipatia nchi ya Malaysia miaka ya 70 na limekuwa likifanya vizuri sana kwenye nchi hiyo na kukuza uchumi. Kwa kuwa zao hili linazalisha bidhaa zaidi ya 10, naweza nikataja tu chache kwa kifupi sana, linatumika kuzalisha mafuta ya mawese lakini pia mafuta ya mise kutokana na mbegu iliyoko ndani. Pia zao hili majani yake yanasaidia kuezekwa katika mapaa yetu ya nyumba, lakini pia linasaidia katika utengenezaji ...

**MWENYEKITI:** Uliza swali sasa.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Wa sabuni za magadi ambazo hata Wabunge wako katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wamekuwa wakizitumia na mazao mengine kutokana na muda naomba nisiyataje. Kwa nini sasa Serikali haioni ni wakati muafaka wa kutengeneza Bodi maalumu ambayo itashughulika na mchikichi na kutotegemea Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa sababu Bodi hiyo inaendeshwa kwa kusuasua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, haiwezekani zao la mchikichi kwa kiwango kikubwa lilimwe katika Mkoa wa Kigoma na mikoa jirani, lakini Kituo cha Utafiti kikawekwa Mikocheni Dar es Salaam na Tabora. Kwa nini sasa wasifungue ofisi ya utafiti katika Mkoa wa Kigoma ili wakulima wetu wa michikichi waweze kwenda kufanya *consultation* na kupata ushauri mbalimbali katika mkoa wao? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu ndugu yangu Mheshimiwa Sabreena Sungura maswali yake mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge anayetoka Kigoma kwa kufuatilia zao zima hili la mchikichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye maswali yake, swali la kwanza, kila zao linataka liwe na Bodi yake, kwa maana hiyo gharama zake zinakuwa kubwa sana. Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Bodi yetu ya Mazao ya Nafaka Mchanganyiko si kwamba inasuasua, tunawashukuru sana Wabunge juzi wamepitisha bajeti yetu ya Wizara ya Kilimo na sasa hivi tumejipanga kuhakikisha kwamba Bodi yetu ya Mazao Mchanganyiko inafanya kazi kwa kuboresha zaidi ili hili zao letu la mchikichi ambalo linasimamiwa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko liweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye swali lake la pili kwamba kwa nini Mkoa ule wa Kigoma usiweze kuwa na Kituo cha Utafiti. Ni kwamba hivi vituo vyetu vya utafiti hususan katika zao la michikichi vimewekwa kikanda. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba katika Mkoa wa Tabora, pale Tumbi tafiti zetu zinafanyika mahali pale. Kwa maana hiyo, hata kile Kituo cha Mikocheni kinafanya *tissue culture*. Naomba niseme kwamba Mkoa wa Tabora uko katika Kanda ya Magharibi ambapo Mkoa wa Kigoma upo chini yake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbaraka Dau na Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Faida zote zinazopatikana katika michikichi zinapatikana pia katika zao la minazi. Je, Serikali ina mikakati

gani ya kufufua zao la minazi ambalo linalimwa zaidi katika Mikoa ya Ukanda wa Pwani?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Dau swali lake moja dogo la nyongeza kuhusu minazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunaelewa kwamba minazi nayo ni zao muhimu sana kwa kilimo katika nchi hii. Kama nilivyosema ni kwamba kupitia Bodi yetu ya Mazao Mchanganyiko ambayo Bunge lako Tukufu limepitisha bajeti hapa, minazi nayo ipo chini ya Bodi yetu ya Mazao na Nafaka Mchanganyiko. Kama Serikali tuko tayari kuhakikisha kwamba tunaimarisha zao la minazi ili nalo liweze kuwa ni zao la kibiashara na chakula kama kiungo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa Zungu.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakubaliana nami kwamba uanzishwaji wa Vituo vya Utafiti wa Mazao ya Kilimo, vilianzishwa vingi kwa kanda na lengo lilikuwa zuri, lakini utendaji wa vituo hivyo umeanza kusuasua hivi karibuni kwa sababu ya kutokupata fedha za kutosha za kusimamia shughuli zake. Mfano mzuri ni Kituo cha Utafiti wa Mazao ya Korosho pale Naliendele. Ni lini Serikali sasa itapeleka fedha za kutosha ili vituo hivi vianze kufanya kazi kama vilivyokusudiwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa mkwe wangu Nape Nnauye, Mbunge wa Jimbo la Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Vituo vingi vya Utafiti vya Wizara yetu ya Kilimo, vinasuasua lakini kama tunavyoelewa kwamba vituo hivi na sisi kama Wizara tumewaambia pia wajiongeze zaidi hata wao, si tu kutegemea pesa ya Serikali kwa sababu vituo vyetu vya utafiti vinaweza pia vikaandika *proposal* kwa ajili ya kuweza kupata fedha pia kutoka kwa wafadhili mbalimbali ili viweze kufanya kazi yake vile inavyotakiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Vulu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Zao la mawese ambalo ndiyo mchikichi linazalisha vilevile petroli na mafuta ya kula. Nchi ya Malaysia ambayo imechukua mbegu hii Tanzania ina mafanikio makubwa sana ya zao hili. Je, Serikali namna ilivyofanya sasa kupeleka zao la korosho kila mkoa, kwa nini kusiwe na *affirmative action* ya kupanda michikichi siyo chini ya milioni 30 ili Serikali *i-benefit* na zao hili ambalo ni zuri kwa uchumi wa nchi hii? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu tu kwamba sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha zao hili la mchikichi ambalo linatoa mafuta ya mawese linafanikiwa kwa kasi. Kama Wizara ya Kilimo tuna programu yetu ya *Supporting Indian Trade and Investment in Africa* (SITA),

kuhakikisha kabisa zao hili la mchikichi nalo linatiliwa mkazo na liweze kufanya vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zaynab Vulu na Kuchauka.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa zao la mchikichi linafanana na zao la nazi; na kwa kuwa watu wa Pwani wanategemea sana zao la nazi; kwa kipindi kirefu zao hilo limekumbwa na ugonjwa ambapo minazi inanyauka na Serikali iliahidi kufanya utafiti. Je, utafiti huo umefikia wapi na kuna mkakati gani wa kuhakikisha zao hilo litafufuliwa upya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Dkt. Tizeba, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Naomba nimjibu Mheshimiwa Zaynab Vulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyauko ni ugonjwa ambao unakumba mazao mengi na mbinu iliyopo mpaka sasa ya kukabiliana na mnyauko ambayo inaeleweka ni kwa kufanya usafi (*sterilization)*. Mbinu hii imekuwa ikiandamana na hasara na vimelea hawa kuendelea kubaki kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasayansi sasa hivi duniani wanaelekea kwenye mbinu nyingine *bio-control* ambapo *enzymes* zinazalishwa kwa ajili ya kimelea mahsusi kilichosababisha mnyauko kwenye zao au mmea fulani. Utafiti huu umeendelea kufanyika katika vituo vyetu vya utafiti na sasa hivi tuko katika hatua ya kujenga kiwanda cha kuzalisha hivi vimelea *(enzymes)* zitakazokabiliana na aina mbalimbali ya minyauko katika mimea yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Ryoba na Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Bodi ya Mazao Mchanganyiko iko imara na haijatetereka. Naomba kuuliza kwa nini wakati tunaingiza zao la ufuta kwenye stakabadhi ghalani wasimamizi wakapewa Bodi ya Maghala badala ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Dkt. Tizeba, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Bodi kununua mazao na mfumo wa kuuza ni vitu viwili tofauti. Hata hiyo Bodi ya Mazao Mchanganyiko ikitaka kununua zao linalouzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, itabidi na wao waende wakanunue huko kwenye huo mfumo. Siyo kwamba Bodi ya Mazao Mchanganyiko maana yake ni mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Bodi na yenyewe itashiriki kununua kama wanunuzi wengine walivyo kwa kwenda kununua kwenye mfumo huo wa stakabadhi ghalani. Kwa hivyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge asichanganye haya mambo, Bodi hii itafanya biashara ya kununua mazao na kuuza kwa kushindana na wafanyabiashara binafsi na watu wengine katika mazao mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Marwa Ryoba na Mheshimiwa Zitto.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali kuhusu ununuzi wa pamba, Mkoa mzima wa Mara, Wilaya za Serengeti, Bunda, Musoma Vijijini na maeneo mengine mpaka sasa hawajaanza kununua pamba. Tuliomba hapa kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo kwamba mtindo uliokuwa unatumika zamani wa kununua pamba uendelee kuliko huu wa kulazimisha mwananchi atembee kutoka Kilometa ngapi akafungue akaunti benki jambo hili limekuwa gumu kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Kwa hiyo, naomba kuuliza ni lini pamba itaanza kununuliwa Mkoa wa Mara?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Dkt. Tizeba, majibu, ni lini?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa pamba ulifunguliwa tarehe 1 Mei na ununuzi unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini kutegemeana na upatikanaji wa pamba ulivyo. Pamba haikomai kwa mara moja nchi nzima, inakomaa tofauti kulingana na ukanda wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi ununuzi katika Mkoa wa Mara umeshaanza, nimezungumza leo asubuhi na Mkuu wa Mkoa. Tatizo lililoko Mara ni wale wanaohusika kununua wanawatapeli wananchi kwamba akilipa taslimu anapewa Sh.800 badala ya Sh.1,100 bei iliyotangazwa ya kununua pamba msimu huu. Sasa hivi maelekezo yapo, watafutwe wanaofanya huo udanganyifu ili wananchi wapate haki yao kwa mauzo halali wanayoyafanya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Februari, 2017, Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Kigoma *RCC* ilipitisha mkakati wa kuendeleza zao la michikichi. Mpaka leo toka barua imepelekwa Wizara ya Kilimo hata kujibu kwamba imepokea barua ile kutoka Mkoa wa Kigoma haijajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yote yanayotolewa hapa kuhusiana na *tissue culture* Mikocheni, utafiti pale Tabora si ya kweli kwa sababu Kigoma ndiyo imepeleka mbegu Mikocheni na wala si Serikali. Je, Serikali haitaki kututhibitishia kwamba imeshikwa na wafanyabiashara wanaoagiza mawese ghafi kutoka Indonesia na Malaysia na ndiyo maana haitaki hata kujibu barua ya Mkoa wa Kigoma ya kuendeleza zao la michikichi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa nini hamtaki kujibu barua ya Halmashauri ya Kigoma, hilo tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la kaka yangu Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake ni zuri na kwa sababu Serikali hii ya Awamu ya Tano ni ya Hapa Kazi tu basi ningemwomba sana, sana, sana Mheshimiwa Mbunge kaka yangu kwa heshima na taadhima atuletee nakala ya hiyo barua sisi tuko tayari kuifuatilia na kuhakikisha kwamba tunaifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum na linaulizwa kwa Waziri wa Majina Umwagiliaji.

Na. 437

**Tatizo la Maji Njombe Kusini**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo la maji katika Jimbo la Njombe Kusini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inaendelea kutekeleza miradi ya maji katika Halmashauri zote nchini, ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Njombe imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.55 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji. Mpaka sasa Serikali imekamilisha Miradi ya Maji katika Vijiji vya Peruhanda, Limage, Igominyi, Igoma na Iwongilo. Miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma ya maji Njombe Mjini ambapo ni Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Njombe, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali inatekeleza mradi kutoka Chemchem ya Kibena kwa gharama ya shilingi bilioni 1.1. Hadi kufikia Mei, 2018, kazi zilizokamilika ni ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 2.2; ujenzi wa kidakio cha maji; ununuzi wa dira za maji na ufungaji wa pampu mbili za kusukuma maji zenye uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 72 kwa saa. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimai 90 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali itatekeleza mradi wa maji kutoka Mto wa Hagafilo kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa Njombe Mjini na maeneo ya pembezoni mwa mji huo. Usanifu wa mradi huo umekamilika na kazi zitakazotekelezwa ni ukarabati wa chanzo cha Magoda; ujenzi wa chanzo cha Mto Hagafilo; ulazaji wa bomba kuu; ulazaji wa mabomba ya usambazaji; ujenzi wa matanki na ufungaji wa dira za maji. Mradi huo utagharimu Dola za Marekani milioni 13.5 ikiwa ni mkopo nafuu kutoka Serikali ya India. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Njombe tunaishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, imetupa pesa kwa miradi mikubwa ya maji ya Njombe Mjini, Wanging'ombe na Mji wa Makambako. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza miradi mikubwa ya maji Wanging'ombe pamoja na Mji wa Makambako? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, ni lini Serikali itaenda kutatua kero ya maji Wilaya ya Ludewa katika Kata za Milo, Mavanga na Mkomang'ombe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali haya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Eng. Isack Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Njombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeza kwamba swali lake ni zuri na swali hili linahusu pia maeneo

mengine ambayo mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India Dola milioni 500 utakwenda kutekeleza miradi ya maji katika miji 17. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 6 Juni, Katibu Mkuu ameunda kikundi cha Mainjinia nane ambao wanatengeneza *terms of reference,* watafanya kazi kwa muda wa siku 16, tarehe 20 tutakuwa tumeanza kuaandaa nyaraka kwa ajili ya kuanza kutangaza zabuni. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Neema Mgaya kwamba tayari tunalifanyia kazi pamoja na wote watakaofaidi mkopo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na Ludewa Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza miradi katika maeneo hayo. Kwa sasa tunaingia katika Programu ya Awamu ya Pili, tutahakikisha kwamba vijiji vyote alivyovitaja vinapata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kuzungukwa na Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa lakini bado wanakabiliana na changamoto kubwa ya maji. Njia zote ambazo Serikali wamekuwa wanatumia wameshindwa kabisa kumaliza changamoto za wananchi wa Mkoa wa Rukwa. Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka sasa kutumia Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa kuweza kumaliza tatizo hilo la maji kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Eng. Isack Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye mwenyewe anakaa Mkoa wa Rukwa ni shahidi kwa macho sio kuambiwa

kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekamilisha utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji pale mjini Sumbawanga na Mheshimiwa Rais anakwenda kuzindua mwezi huu, huduma ya maji inapatikana kwa asilimia 100 katika Mji wa Sumbawanga. Pia tunaendelea kutekeleza miradi mingine katika Mkoa wa Rukwa na kwenye Awamu Pili ya Programu ya Sekta ya Maendeleo ya Maji tutahakikisha mkoa mzima unapata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, Ziwa Rukwa maji yake hayafai kwa matumizi ya binadamu. Kwa hiyo, ziwa linalofaa ni Ziwa Tanganyika na tayari tuna andiko la kuchukua maji kutoka Ziwa Tanganyika kupeleka Mkoa wa Rukwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Mollel na Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Tabora Kaskazini lina vyanzo vichache sana vya maji, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kusafiri na mimi kwenda kutembelea chanzo kikubwa cha maji pale Kijiji cha Majengo Ikuza ili kuona kama kinafaa kugawa maji kwenye vijiji vya karibu vya Kanyenye, Ikongolo, Kiwembe na Majengo yenyewe?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mkaone, mnaweza kwenda kuona, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari na tayari nimeshazungumza naye, majukumu hayo nimemkabidhi Mkurugenzi wa Mamlaka wa Maji ya Tabora ili aende akatembelee eneo lake na kutumia chanzo hicho cha maji ili Jimbo lake lipate maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Pamoja na majibu mazuri na jitihada za Waziri mwenye dhamana kutatua kero ya maji hapa nchini, naomba majibu ni lini Serikali itatusaidia wananchi wa Halmashauri ya Arusha *DC* katika Kata za Oldonyosambu na Oldonyowasi ambako wananchi na hasa watoto wameathirika na maji yenye kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride*?

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Eng. Isack Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana kwa jinsi ambavyo anawatetea wananchi wa Arusha ambao kuna maeneo ambayo maji chini ya ardhi yana madini ya *fluoride.* Siyo Arusha tu, madini ya *fluoride* yapo Shinyanga na juzi nimegundua juzi yapo hata katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuona umuhimu na athari hii inayosababishwa na madini ya *fluoride* ilitengeneza kiwanda na kuna utafiti wa kutengeneza madini kwa kutumia mifupa ya ng'ombe kwa ajili ya kuondoa *fluoride* na tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa. Mwaka jana tulitengeneza mitungi zaidi ya 200 na kusambaza kwa wananchi na mwaka ujao wa fedha tunatengeneza zaidi ya mitungi 1,000 kwa ajili ya kusambaza kwa wananchi ili kuondoa hayo madini ya *fluoride*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kupata mafanikio makubwa. Wazazi walipata madini hayo lakini watoto wanaozaliwa sasa hivi wako vizuri hawana athari ya madini ya *fluoride*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Ungando na Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ndanda limegawanyika katika maeneo matatu ya mtandao wa maji. Kuna upande wa Mashariki ambao unaanzia Kata ya Nanganga mpaka Chikukwe kwenyewe kuna mradi mkubwa wa maji unafanyika pale. Kata ya Magharibi kwenye Vijiji vya Chingulungulu...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, sasa hivi Serikali imeanzisha utaratibu wa kuchimba mabwawa kwa ajili ya maji na kuendeleza mabwawa ya zamani ikiwepo bwawa lililoko Kata ya Lukuledi. Nataka kufahamu kutoka kwa Waziri kwa sababu maji safi na salama yanayotokea bomba la Mbwinji yamefika mpaka Kata ya Chikunje ambapo ni kilomita 10 tu kufika kwenye Kata ya Lukuledi. Je, Serikali haioni haja ya kuendeleza mradi huu wa maji badala ya kwenda kuendeleza lile bwawa ambalo halina chanzo cha uhakika cha maji zaidi ya maji ya mvua?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu lengo lake ni kuhakikisha wananchi wanapata maji. Kwa ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kama kuna chanzo cha uhakika, tunaweza kuweka utaratibu kuhakikisha wananchi wako wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ungando, Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Mto Rufiji kupeleka maji Ikwiriri, Bungu na Nyamisati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa mjukuu wangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imepata *grant* kutoka Serikali ya Korea na tumeanza *feasibility study* ambayo inakamilika Julai, 2018 kwa ajili ya kuchukua maji kutoka Mto Rufiji kuyaleta Dar es Salaam kupitia kwenye maeneo yote ikiwepo pamoja na eneo Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mangungu, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara Naibu Waziri alitoa ahadi ya kusaidia kupatikana kwa mtandao wa maji katika Jimbo la Mbagala. Hata hivyo, katika tenda waliyotangaza mwezi uliopita maeneo yote ya Mbagala hayajatajwa, wameendelea na maeneo yale yale ambayo kila siku wamependelea kupeleka maji. Je, wananchi wa Mbagala tutegemee nini juu ya upatikanaji wa maji safi na salama kutoka katika chanzo cha Ruvu Juu na Ruvu Chini?

**MWENYEKITI:** Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwaambie wananchi wake wa Mbagala wakae mkao wa kula. Jumatatu pale Dar es Salaam nakutana na Benki ya

Maendeleo ya Ufaransa, walishatuahidi kutoa dola milioni 130 kwa ajili ya mradi wa maji safi na maji taka eneo la Temeke ikiwemo na Mbagala. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba tu asubiri kidogo atapata majibu, wananchi wa Mbagala hawajaachwa. Tunahakikisha Dar es Salaam yote inapata maji safi na salama ikiwemo pamoja na visima vya Kimbiji na Mpera. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Kaboyoka wa mwisho.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dodoma linakua kila kukicha na uwezo wa DUWASA kuwahudumia wananchi wa Dodoma unapungua kutokana na fedha zinazotolewa na Serikali. Wananchi wanaoishi Ntyuka, Ng'ong'ona, *UDOM*, Mtumba hawana maji.

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba watu wanaohamia Dodoma na walioko Dodoma wanapata maji safi na salama kwa wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki hii nimeshuhudia utiaji wa saini wa mradi wa kupeleka maji katika mji wa Serikali pamoja na eneo la Mtumba, kwa hiyo, maji yatapatikana.

Hata hivyo, chanzo cha Makutopora Mzakwe kina uwezo wa kutoa lita milioni 61.5, kwa hiyo, maji yapo na sasa hivi tunazalisha lita milioni 46. Kwa hiyo, maji bado tunayo Mheshimiwa Mbunge. Sasa hivi tunaweka mradi wa kusambaza maji ili tuweze kufika maeneo yote aliyotaja Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bunge lako lilipitisha hapa kwamba kilimo cha umwagiliaji ndiyo tu kinachoweza kutoa umaskini katika nchi hii. Kwa kuwa Jimbo la Same Mashariki tumepeleka maombi yetu yana miaka 16 sasa ya kujengewa miundombinu kupitia Bwawa la Yongoma kwa ajili ya umwagiliaji. Je, Waziri anaweza kuniambia lini Bwawa hili la Yongoma litajengwa ili tukuze kilimo cha umwagiliaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inakamilisha stadi ya mpango kabambe kwa ajili ya suala la kilimo cha umwagiliaji. Mpango ambao ukishakamilika utaainisha maeneo yote tutakayotekeleza miradi ikiwemo pamoja na kutumia Bwawa la Yongoma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tunafika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kwa siku ya leo. Leo mnafahamu ni siku muhimu sana kwa Taifa hili, kwa hiyo, nitangaze wageni tulio nao. Tuna wageni wa Mheshimiwa Spika walipo kwenye Jukwaa la Spika wanatoka kule Songambele Kongwa, Ndg. Onesmo Nywage – Mheshimiwa Diwani; Mheshimiwa Mfaume Kizingo – Katibu

wa Chama wa Wilaya ya Kongwa, Ndg. Elia Lesilwa; Ndg. Chrispin Mguli; Ndg. Pascal Kisongela; Ndg. Tumaini Ndumuza, Ndg. Rajabu Maziwa; Ndg. Adam Saidi; Ndg. Janeck Mpinge; Ndg. Robert Chilonzola; Ndg. Tumaini Chaulema; Ndg. Chrenesi Ayubu; Ndg. Felician Mlowe na Ndg. Hussein Pawaga. Karibuni sana ndugu zetu, naamini ninyi ni Wagogo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliopo Jukwaa la Spika pia ambao ni wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni kutoka Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bwana Dotto James; Naibu Katibu Mkuu - Suzana Mkapa; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Khatibu Kazungu; Naibu Katibu Mkuu – Ndg. Amina Shaban; Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania - Prof. Florens Luoga; Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania - Dkt. Yamungu Kayandabila; na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* – Bw. Charles Kichere. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Kamishna wa Bajeti – Bi. Mary Maganga; Kamishna wa Sera – Bw. Benedicto Mgonya; Kamishna wa Fedha za Nje – Bw. John Rubuga; Mhasibu Mkuu wa Serikali – Bw. Francis Mwakapalila; Msajili wa Hazina - Bw. Athumani Mbuttuka, huyo ndiye anayeshikilia rasilimali zote za Serikali kwenye makampuni kwa niaba ya wananchi wa Tanzania; Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali – Ndg. Mohamed Mtonga; Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)* – Dkt. Albina Chuwa. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo pia Kaimu Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ubia na Sekta ya Umma na Sekta Binafsi – Bw. John Mboya; Mkurugenzi wa Idara ya Kuondoa Umaskini – Dkt. Anna Mwasha; Mchumi Mkuu upande wa Mipango – Dkt. Lorah Madete, wale ambao hamumfahamu huyo ni binti yangu; Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kilimo Tanzania – Ndg. Augustino Chacha; Mtendaji Mkuu wa *TID Corporate Bank* –

Ndg. Frank Mugeta; na Mtendaji Mkuu wa *TIB Development Bank* – Bw. Charles Singili. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunaye Balozi wa Uingereza Nchini, Hon. Sarah Cooke; *Senior Political Officer* katika Ubalozi wa Uingereza – Sylivester Ernest; na Mchumi kutoka *DFID* - Mark Dray. Karibni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Kusumbin Bhangwanji Meisuria, mke wa Mheshimiwa Bhagwanji na dada yake Mheshimiwa Bhagwanji ambaye anaitwa Lalitabin Nageda Meisuria. Karibuni sana. Bhagwanji Baniani peke yake humu ndani. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni nane wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoka Chama cha Wanawake wa Tasnia ya Filamu Nchini *(CWTF)* na Mpango wa Damu Salama wakiongozwa na Meneja Mpango wa Damu Salama Dkt. Magdalena Lyimo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambaye ni binti yake kutoka Ngara Mkoani Kagera, Ndugu Joyce Gashaza. Karibu sana binti yetu. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Grace Kiwelu ambaye ni Mwenyekiti wa BAVICHA Vunjo, Mkoani Kilimanjaro, Ndugu Bony Mbando. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Siha kwa tiketi ya Chadema, Bwana Frank Kisinani Tarimo na Ndugu Valerian Juwal - *DED* wa Wilaya ya Siha. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Rose Kamili ambao ni watoto wake na wajukuu kutoka Jijini Dar es Salaam na Dodoma hapa. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Pauline Gekul ambao ni watoto wake kutokea hapa Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dodoma, Ndugu James Ezekiel na Ndugu Mariam Bura. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambao ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Jimbo la Hanang, Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Godluck Solomon. Karibuni wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Risala Kabongo ambao ni rafiki yake ambaye ameambatana na mwanaye kutoka Jijini Dodoma hapa. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Karagwe. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ni matangazo ya wageni, tunaendelea na matangazo. Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi kwa masikitiko makubwa anaomba niwatangazie Wabunge kwamba Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi amefiwa na mume wake jana saa 11.00 jioni katika Hospitali ya Bugando na mazishi yanatarajiwa kufanyika Mjini Mwanza siku ya Jumamosi wiki hii na tutaendelea kupewa taarifa zaidi kuhusiana na mazishi hayo.

Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya anawatangazia Wabunge kwamba leo ni siku ya Wachangia Damu Duniani. Anawaomba Waheshimiwa Wabunge tujitokeze kwa wingi kuchangia damu ili kuokoa maisha hasa ya wanawake wajawazito na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano. Zoezi hili litafanyika Viwanja vya Nyerere *Square* hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

## Majibu ya Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa John W. Heche kuhusu Serikali kupiga Marufuku Usafirishaji wa *Carbon*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, yafuatayo ni maelezo ya Spika kuhusu mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa John Wegesa Heche tarehe 4 Juni, 2018 kuhusu Serikali kupiga marufuku usafirishaji wa *carbon*.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka siku hiyo Mheshimiwa Heche aliomba mwongozo wa Spika akisema kwenye mikoa yetu ambayo mingi tunazalisha dhahabu kwa mfano Mkoa wa Mara, hatuna hiyo *plant* ya *elusion,* ndiyo akaomba mwongozo. Katika hali hiyo wanapopiga marufuku usafirishaji wa *carbon* inakuwaje?

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Heche aliomba mwongozo wa Spika kuhusu kauli iliyotolewa na Waziri wa Madini wakati akihitimisha hoja yake kwamba ni marufuku kusafirisha *carbon* kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine. Katika mwongozo huo Mheshimiwa Heche aliomba suala hilo liangaliwe na ikiwezekana Wabunge walijadili kwa sababu mikoa mingi inayozalisha dhahabu hapa nchini kwa mfano Mkoa wa Mara haina *plant* ya *elusion* hivyo marufuku hiyo au katazo hilo litaathiri watu wengi kiuchumi.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia mwongozo huo, Kiti kilitoa uamuzi kwamba suala hilo lifanyiwe kazi na kwa wakati muafaka Serikali itakuja kutoa maelezo Bungeni. Kwa hali hiyo, nimuite Waziri wa Madini atoe maelezo kuhusu suala lililoombewa mwongozo na Mheshimiwa Heche. Karibu Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Juni, 2018 Mheshimiwa John Heche aliomba mwongozo wa Mheshimiwa Spika kuhusiana na katazo la usafirishaji wa *activated carbon* kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine. Kufuatia mwongozo huo, Mheshimiwa Spika

alituelekeza tuweze kutoa maelezo Bungeni kuhusiana na katazo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakavyokumbukwa tarehe 1 Juni, 2018 nilipokuwa nikifanya majumuisho ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2018/2019, nilitangaza katazo la usafirishaji wa *activated carbon* zinazotoka katika mitambo ya kuchenjulia dhahabu kutoka nje ya mkoa ambao una mtambo wa uchenjuaji kupelekwa katika *elusion plant* iliyo kwenye mkoa mwingine ili kufanya uchenjuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia ilitokana na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge waliyoitoa wakati wakijadili hotuba ya bajeti ya Wizara yangu. Katazo hili pamoja na mambo mengine lililenga kudhibiti masuala mbalimbali ambayo yalikuwa yakifanyika kinyume cha sheria na kanuni ikiwemo ukwepaji wa kulipa kodi za Serikali; kulipa mrabaha wa Serikali; kulipa ushuru wa huduma kwa halmashauri husika *(service levy);* utoroshaji madini na matukio ya wizi wa madini wa mara kwa mara unaofanywa na wachimbaji wasio waaminifu kwa kutorosha *carbon* na kuzipeleka nchi jirani ambako kumejengwa *elusion plants*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mabadiliko ya teknolojia hususani urahisi wa upatikanaji wa teknolojia ya uchenjuaji wa madini inathibitisha wazi kwamba teknolojia hiyo inaweza kuwekwa kila mkoa ambako kuna mahitaji ya uchenjuaji. Kufuatia mabadiliko ya teknolojia ya uchenjuaji katika miaka ya 2000, idadi kubwa ya wachimbaji na wachenjuaji wadogo nchini wamekuwa wakitumia kemikali ya *cyanide* kwa ajili ya kuchenjua madini ya dhahabu. Teknolojia hii inahusisha kutumia matenki ya kuozoshea *(VAT leaching)* na *activated carbon* ambazo hufyonza dhahabu kutoka katika udongo uliowekwa katika matenki na kuchanganywa na kemikali ya *cyanide*. Dhahabu iliyofyonzwa kwenye *activated carbon* huchenjuliwa katika mitambo ya uchenjuaji *(elusion plants)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kubwa ya mitambo hii au *elusion plants* imejengwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Dodoma, Tabora, Musoma, Shinyanga, Songwe na Singida na hivyo kupelekea wachenjuaji wengi wa dhahabu kusafiri kwenda kwenye mikoa hiyo kufuata huduma hiyo. Kabla ya katazo hili, Ofisi za Madini kwenye maeneo husika zimekuwa zikitoa vibali vya usafirishaji wa *carbon* zenye dhahabu kutoka eneo moja hadi lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya malengo ya Sera ya Madini ya mwaka 2009 ni pamoja na kuimarisha mfumo wa sheria na udhibiti katika sekta ya madini ili kuhakikisha kwamba Serikali inanufaika na mapato yanayotokana na sekta ya madini. Matukio mengi ya wizi wa *carbon* na mengine ya ukiukwaji wa sheria na kanuni yameripotiwa katika siku za hivi karibuni na Serikali haiwezi kukaa kimya wakati matukio haya yanayoikosesha Serikali mapato yakiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Mkoa wa Geita kati ya Januari hadi Aprili, 2018, yaliripotiwa matukio matano yaliyohusisha uporaji wa *carbon* zilizo na dhahabu zenye uzito wa tani 10.5 na thamani ya shilingi bilioni 1.72 ambapo mrabaha wa Serikali kiasi cha shilingi milioni 103 kingeweza kukusanywa, ada ya ukaguzi kiasi cha shilingi milioni 17.1 ingeweza kukusanywa, lakini pia kwa upande wa halmashauri wangeweza kukusanya ushuru wa huduma wa shilingi milioni 5.16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Februari, 2018 Mkoani Mwanza liliripotiwa tukio lililohusisha wizi wa *carbon* zilizo na dhahabu zenye uzito wa tani 1 zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi milioni 58.14 kwa wastani wa bei ya Februari, 2018 ambayo ni sawa na Sh.95,000 kwa gramu ya dhahabu. *Carbon* hizo zilizoibiwa endapo zingechenjuliwa zingeweza kuzalisha kiasi cha gramu 612 za dhahabu. Pia kwa upande wa mrabaha wa Serikali tungeweza kupata kiasi cha shilingi milioni 3.488; ada ya ukaguzi kiasi cha shilingi 581,400 lakini pia halmashauri

ingeweza kutoza ushuru wa huduma wa shilingi 174,420 na hii ni kwa hiyo tani moja tu ambayo imeibiwa. Hadi leo hii napotoa maelezo haya *carbon* hizo zilizoibiwa hazijapatikana, hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali yenye jumla ya Sh.4,244,220 kwa tani hiyo moja tu ambayo *carbon* zake ziliweza kuibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mei, 2018 katika eneo la Magambas, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga, liliripotiwa pia tukio la wizi wa *carbon* zenye uzito wa tani 2.23 zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi milioni 80 na ambapo mrabaha wa shilingi milioni 4.8 na ushuru wa huduma kwa halmashauri kwa shilingi 240,000 ungeweza kukusanywa. *Carbon* hizo za Magambas zilikuwa zimeombewa kibali cha kuzisafirisha na maombi hayo yalikataliwa kufuatia mgogoro uliopo katika eneo hilo na ndipo inasadikika kwamba *carbon* hizo zilitoroshwa na kubadilishwa na *carbon* zisizo na dhahabu. Tukio hili kwa sasa tunaendelea kulichunguza na kulifuatilia na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama wamekuwa wakifanya kazi nzuri katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya kimsingi yanatoa taswira kwamba zoezi la usafirishwaji wa *carbon* kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine limegubikwa na utata na udanganyifu mwingi na hivyo Serikali imeamua kuchukua hatua za udhibiti wa biashara ya usafirishaji wa *carbon* kutoka mkoa mmoja hadi mwingine ili kuongeza ufanisi katika kudhibiti mnyororo mzima wa uchenjuaji na usafirishaji wa *carbon*. Katazo la kusafirisha *carbon* kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine linalenga kuwa na manufaa yafuatayo na nitataja tu takribani manufaa saba.

(i) Kudhibiti matukio ya wizi wa *carbon* na hivyo kuiwezesha Serikali kukusanya mapato yake;

(ii) Kudhibiti utoroshwaji wa madini unaofanywa na baadhi ya wachimbaji na wachenjuaji wasio waaminifu kwa kuwa uchenjuaji wote utafanyika sehemu moja ambayo itasimamiwa kwa karibu zaidi na mamlaka za maeneo husika;

(iii) Kudhibiti ukwepaji na ucheleweshwaji wa malipo ya kodi, mrabaha na ada ya ukaguzi wa madini unaofanywa na baadhi ya wachenjuaji wa madini wanaposafirisha *carbon* nje ya maeneo ya miradi yao kuchenjua dhahabu;

(iv) Kuchochea ujenzi wa mitambo ya kuchenjulia kwenye maeneo husika ambapo hatua hii itachochea uwepo wa masoko kwenye maeneo husika na hivyo kuinua uchumi wa maeneo hayo;

(v) Kuongeza mapato ya mkoa husika kutokana na malipo ya ushuru wa huduma yatakayolipwa na wamiliki wa miradi ya uchenjuaji au *VAT leaching* na *elusion plants*;

(vi) Kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza mzunguko wa fedha kutokana na uchenjuaji kufanyika katika eneo husika kupitia huduma za vyakula, malazi, bidhaa, benki na huduma nyinginezo; na

(vii) Kuongeza ajira kwa wananchi wa maeneo ambapo shughuli za uchenjuaji zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kulifahamisha Bunge lako Tukufu, tangu nilipotoa katazo hili tarehe 1 Juni, 2018, kwa kipindi cha siku tisa tu tarehe 1 - 9 Juni, 2018, Serikali imeanza kunufaika na tumeweza kuona manufaa zaidi. Mfano, takwimu zetu zinaonesha kwamba katika Mkoa wa Geita, vibali 40 vya kuchenjua *carbon* yenye dhahabu yenye uzito wa kilogramu 22,110 vilitolewa ambapo dhahabu iliweza kuzalishwa takribani gramu 28,402.83 yenye thamani ya Sh.2,290,910,480.95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uzalishaji huo, Serikali iliweza kupata malipo ya mrabaha wa Sh.137,454,628.86 pamoja na ada ya ukaguzi Sh.22,909,104.81 ikilinganishwa na vibali saba ambavyo vilitolewa kwa mwezi mzima kwa upande wa Geita. Kwa siku tisa peke yake

tumeweza kutoa vibali vya Geita takribani 40 na mtaona manufaa hayo kama nilivyoyaeleza. Serikali ilipata malipo ya mrabaha wa shilingi milioni 64.8 na ada ya ukaguzi ya shilingi 10,806,368.83. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganifu wa vibali 137 vilivyotolewa kwa kipindi hicho cha mwezi mmoja wa Mei, 2018 kutoka Mkoa wa Geita kwenda Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kuchenjua *carbon* yenye uzito wa dhahabu kilogramu 92,750 iliyozalisha gramu 42,418.23 na thamani ya Sh.3,514,097,358.42 unaonyesha dhahiri kwamba Serikali ilipata malipo ya mrabaha wa Sh.210,845,841.81, hiyo ni kwa mwezi mzima. Ukiangalia kwa siku tisa tu peke yake Geita imeweza kupata mrabaha wa takribani shilingi milioni 137. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa Mei, 2018 kwa uzalishaji uliofanyika Mkoani Mwanza kwenye hizo *elusion plants* kwa vibali ambavyo vilitolewa Geita badala ya kuchenjuliwa katika *elusion plants* za Geita zikaenda kuchenjuliwa Mwanza ilikuwa ni takribani asilimia 69.73, wakati kwa mwezi huo huo vibali vilivyotolewa Mkoani Geita na uzalishaji kufanyika Geita ilikuwa ni asilimia 30.23. Utaweza kuona kabisa *elusion plants* Geita zipo lakini wameenda kuchenjulia Mwanza mwisho wa siku Geita wenyewe wamenufaika kwa asilimia 30.27 tu, ni jambo ambalo kwa kweli haliwezi kukubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, kwa siku tisa pekee baada ya kutolewa kwa katazo, uzalishaji uliofanyika Geita kwa vibali vilivyotolewa Geita hadi sasa ni asilimia 67 ya vibali 137 vilivyotolewa kutoka Mkoa wa Geita kwenda Mkoa wa Mwanza. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba kutokana na katazo hili usimamizi umekuwa rahisi na utakuwa rahisi zaidi lakini tutaweza kupata ongezeko la uzalishaji wa dhahabu na kuimarika kwa mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo haya ya Serikali, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi

kwa ujumla kwamba Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ipo makini na haiwezi hata kidogo kuruhusu upotevu wa mapato ya Serikali katika sekta ya madini kupitia usafirishaji wa *carbon* zenye dhahabu. Serikali ilitoa fursa ya kusafirisha *carbon* kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine lakini udhibiti wake umekuwa ni mgumu na ndiyo maana katazo hili limekuja ili kuweza kuongeza udhibiti zaidi kwa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nawashauri wawekezaji wenye mitambo ya kuchenjulia dhahabu kuharakisha ujenzi wa mitambo hiyo kwenye maeneo yasiyokuwa na mitambo ya aina hiyo na wawekezaji wengine wenye nia ya kuwekeza katika mitambo ya kuchenjulia kuja kuwekeza katika maeneo yaliyotengwa katika mikoa husika. Tutaendelea kuhusisha na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika kusimamia zoezi la kuchakata *carbon* nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nishukuru kwa mara nyingine tena kwa kupata fursa hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa maelezo yako Mheshimiwa Waziri wa Madini, tunashukuru.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama...

**MWENYEKITI:** Nani amekuruhusu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Heche umesema kwa madhumuni yapi, unaomba mwongozo au unafanya nini?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Waziri ametoa majibu na kwa kweli ukiangalia kwenye...

**MWENYEKITI:** Umesimama kwa mujibu wa Kanuni ipi?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusimama kwa mwongozo ambayo ni Kanuni ya 68(7) lakini nataka kuhusu utaratibu kwamba Waziri anasema uongo. Kwenye hili jambo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Serikali imetoa maelezo, unaweza usiridhike nayo au ukaridhika. Siku ile wewe uliomba mwongozo kwa Kiti kama nilivyo-*make reference* hapa kwa suala hili na kikaagiza suala hili Serikali ije ilitolee maelezo na maelezo ndiyo hayo yametolewa. Wewe katika hatua ambayo inafuata ni kipindi cha mwongozo kama kiti kitaruhusu. Ndiyo maana nikasema kama unasimama useme tu mwongozo wa kiti, twende hivyo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Basi niombe mwongozo kwa sababu jambo hili, kwanza kuna mambo ambayo siyo ya kweli yanasemwa humo ndani ya majibu ya Serikali. Kwa mfano, kusema kwamba Mkoa wa Mara kuna *elusion plant* siyo kweli. Kama ulinisikiliza vizuri mimi nilisema kuna watu wamekopa kwenye mabenki, *SACCOS* na maeneo mengine yote wanadaiwa, *collateral* wameweka nyumba zao na muda unapofika wa benki kutaka kulipwa huwezi kuwaambia kwamba Serikali imepiga marufuku mimi nisipeleke *carbon* kwenye kuchenjua kwa muda huu na ghafla tu kwa hiyo mnipe muda mwingine, watauza nyumba yako na wataharibu maisha yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala nilisema limekuja ghafla mno. Pamoja na majibu mengine ambayo yametolewa kwa Serikali ambayo pia unaweza kuyahoji sana kwa sababu utaratibu unapopewa kibali...

**MWENYEKITI:** Wewe sasa unachangia hoja, nilikuwa nataka tu uniombe mwongozo nikupe mwongozo.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa nini Serikali isitoe walau muda kwa watu wale ambao hawana hizi *elusion plant*

kwenye maeneo yao waendelee kupeleka kwa sababu hizi *elusion plant* zinakwenda kufanyika ndani ya nchi hii. Kwanza sioni mantiki ya kuzuia watu kusafirisha kitu ndani ya nchi hii kwenda kufanyia sehemu ambako anahitaji yeye mwenyewe, hata kama kungekuwa na *elusion plant* kwenye maeneo hayo, kuna *variation* ya bei, unaweza kukuta Mwanza ni bei chini kuliko Mara au maeneo mengine lakini hasa kwenye maeneo ambayo watu hawana hizi *elusion plant* kwa nini wasipewe muda ili hata hao wanaokuja kujenga, kwa sababu huwezi kujenga *elusion plant* kwa siku moja. *(Makofi)*

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo.

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo, mnajua leo ni siku muhimu sana, nimechukua mwongozo mmoja huku na nitachukua mmoja huku, mmekuwa wawili.

**MBUNGE FULANI:** Na huku.

**MWENYEKITI:** Hakuna msinipotezee muda, atauliza pia Mheshimiwa Mbarouk, mmetosha.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Sasa ni-*balance* basi, kama nachukua wawili nachukua na mmoja huku Mheshimiwa Mabula.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, u-*balance* na *gender*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huwezi kuniambia kwamba ni haki ya Mbunge kutaka mwongozo, mimi ndiyo na-*manage* muda siyo wewe. Tunaendelea, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo, natumia Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu unahusu Wizara ya Kilimo kuhusu ununuzi wa zao la pamba. Wakulima wa pamba hasa Mkoa wa Mara sijui mikoa mingine, wamekuwa na tatizo kubwa sana la ununuzi wa pamba na hasa pale wanapokwenda kununua pamba na kuambiwa kwamba waende wakalipiwe hela zao benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anahitimisha bajeti yake hapa, walitoa maelezo kwamba mkulima atakwenda kwenye eneo la kuuzia pamba na makampuni yatapeleka fedha kupitia Chama cha Ushirika na akifika anauza pamba yake na kupewa fedha yake palepale. Kumekuwepo na kauli mbili, kuna maeneo ukienda kwenye kituo unaambiwa utalipiwa benki lakini maeneo mengine wanalipiwa palepale. Hivi karibuni tuliona maelezo ya Waziri kwamba siyo lazima kwenda kulipia hela benki kwa mkulima anayeuza zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo ya Waziri, ni lipi sahihi sasa, ni lile ambalo mkulima anapeleka pamba yake anapewa fedha pale pale au ni kwenda kulipiwa benki? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba mwongozo wako kutokana na majibu yaliyoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Madini juu ya usafirishaji wa *carbon* zenye dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Geita ndipo inapopatikana dhahabu na maeneo mengine na sisi Mwanza hatuna dhahabu kwenye Wilaya ya Nyamagana isipokuwa kule Misungwi. Kwa mujibu wa Sera ya Rasilimali za Taifa, madini na aina nyingine za rasilimali za Taifa kama ambavyo tumewahi kuzungumza ikiwemo gesi, kwa mfano, mwaka 2014 wakati tunasema gesi hii ni kwa jili ya maslahi ya Watanzania, tukawaomba watu wa Mtwara waridhie gesi hii ili iweze kusafirishwa kwenda maeneo mengine ili na Watanzania wote wafaidike nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa wakati Serikali inaruhusu wachenjuaji hawa kufunga mashine kwenye mikoa mbalimbali, Mwanza kuna wachenjuaji zaidi ya *plant* 28 zimefungwa pale, wametumia fedha na wamekopa fedha nyingi sana. Siyo tu kukopa fedha kwenye mabenki, ajira ipo kwa kiwango kikubwa sana. Leo tunavyozungumza kwa siku hizi chache tu toka katazo hili limeanza, watu wanataabika kwenye yale maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka sana niiombe Serikali pamoja na kwamba inadhani mapato mengi yanapotea kwa namna moja au nyingine lakini yapo mazingira ya kuifikiria. Mwanza ndipo ilipo kampuni moja ambayo imekuwa *credited* duniani kwa ajili ya uchenjuaji na utafiti mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Serikali itusaidie wanadhani tatizo ni wachenjuaji au tatizo ni usimamizi? Maana inawezekana wachenjuaji wakawa kila sehemu lakini kumbe tukawa na usimamizi mbovu. Kama Geita zipo mashine za kuchenjua, ndani ya siku tisa wamepata faida hiyo ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema, kwa nini usimamizi huu usiimarishwe kila sehemu hawa watu wakapata

faida na usimamizi huu ukatoa faida kwa kila mtu? Tuwaruhusu kwa sababu rasilimali hii ni ya kwetu sote, tukianza leo kila Mkuu wa Mkoa aseme hapa basi na sisi tunaunga mkono, tutakuwa tunapoteza dira ya Taifa hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Serikali itafakari suala hili na iangalie kwa makini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ukitoa matangazo hapa kuhusu Siku ya Kuchangia Damu Duniani ulitueleza kwamba leo ni Siku ya Kuchangia Damu Duniani. Nimesikia leo katika vyombo vya habari Mheshimiwa Waziri akipiga marufuku kuuza au kununua damu katika hospitali zetu na vituo vyetu vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako nijue Serikali imejipangaje katika hili kwa sababu mimi kama nimepeleka mgonjwa hospitalini damu hakuna na ipo ya kununua siwezi kuacha mgonjwa wangu afe kwa sababu Waziri amepiga marufuku, ina maana itanilazimu ninunue. Vinginevyo Waziri atueleze vituo vyetu vya afya na katika Benki ya Damu nchini ipo damu ya kutosha kwamba hata mtu akiwa anaumwa basi atapatiwa damu hiyo ambayo ipo? Naomba taarifa ya Serikali katika hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge. Nimeona nichukue maombi ya mwongozo kwa hawa Waheshimiwa Wabunge wanne; Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Mabula na Mheshimiwa Mbarouk.

Waheshimiwa Wabunge, hili la Mheshimiwa Mbarouk kwa vile Waziri wa Afya yupo, nitampa nafasi tu aweze kulifafanua lakini tangazo hilo ni muhimu sana kwa Watanzania na hasa kwa Wabunge ambao tumeletewa tangazo hilo na tukio hili linatokea Dodoma hapa. Tukajaribu kuunga mkono jitihada za Serikali katika upatikanaji wa damu salama.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Getere, mkanganyiko ambao anasema upo kwa upande wa uuzaji wa pamba na wanunuzi wa pamba, nitaomba kama Waziri ana majibu atafafanua tu lakini akijibu swali la nyongeza lililoulizwa alijaribu kufafanua tena kwa upande wa eneo la Bunda *specifically* lakini Serikali ipo na msimu umeshaanza. Kama kuna mkanganyiko wa malipo kwa mwenye mali yaani mwenye pamba akalipie wapi, ule usawa kwamba wengine benki na wengine palepale linaweza likafafanuliwa.

Waheshimiwa Wabunge, hili la Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Mabula, hoja ya Waheshimiwa hawa ingawa imetokana na *statement* ya Serikali iliyotolewa sasa hivi, unaona kabisa kwamba Waheshimiwa hawa wawili walioomba mwongozo hawakuridhika na maelezo ya Serikali, *basically* ndiyo hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu kwa suala hili, pamoja na maelezo mazuri ya Serikali ambayo yana sura unaiona ya ukweli lakini pia kuna upande wa pili kwamba muda ambao umetolewa hata kama ni kutekeleza nia hii njema, unapopiga marufuku kuanzia leo maana yake ni kwamba ni kuanzia leo huwezi ukasafirisha. Kwa hali ya kawaida tu unapaswa uzingatie unatoa fursa kwa upande wa pili kwa wale ambao wamewekeza kwa nia njema kwa kukaribishwa na sera zetu, angalau hayo mnayoyasema wapewe nafasi yao wakasema kama ni Mara hawana *elusion plant* wafanyeje wao, si lazima wasafirishe kupeleka mahali fulani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu kwamba Serikali hebu mliangalie tena, tuwasikilize hawa. Lengo tunataka tupate mapato halali ya Serikali lakini pia tusiwaumize wananchi wanaofanya kazi hii. Kwa hiyo, naomba sana upande wa Serikali tusitoe mkanganyiko kwa kitu ambacho kilikuwa kinafanya vizuri tu tangu juzi. Huo ndiyo mwongozo wangu, liangalieni tena. Madini ya dhahabu yapo mengi katika nchi hii, tunakaribisha uwekezaji na hawa wawekezaji kama anavyosema Mheshimiwa Mabula, nendeni Mwanza *elusion plant* ile inafahamika. Ni kweli kuna wizi sisi tunayajua haya mambo na ndiyo maana watu wanaenda mahali ambapo kuna uhakika wa kupata haki yao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu huo, Serikali liangalieni tena suala hili.

**MBUNGE FULANI:** Watoe majibu.

**MWENYEKITI:** Watatupatia majibu, Serikali ipo Bungeni hapa hawababaishi, Serikali haibabaishi hata siku moja. Tupo hapa, acha waliangalie watarudi tu na kutupatia majibu, Waziri na timu yake nawaamini sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namkaribisha Waziri wa Fedha na Mipango aweze kuwasilisha hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa Waziri, una muda wako usiozidi saa moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/2019. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kushiriki Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa na afya njema, amani na utulivu. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtapokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na kuishauri Serikali kwa uzalendo ili kuhakikisha tunafikia malengo ya Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kumpongeza Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri. Chini ya usimamizi wao wa dhati mipango na programu mbalimbali za Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi imetekelezwa kiasi cha kuridhisha na Taifa limepiga hatua kubwa kimaendeleo kuelekea malengo ya Dira yetu ya Maendeleo ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati itakapofika mwaka 2025. Aidha, uongozi wao umedhihirisha kwamba ushindi katika vita dhidi ya rushwa, ufisadi, uzembe na ukwepaji kodi inawezekana. Hivyo, juhudi hizi zinapaswa kuungwa mkono na wananchi wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika mwaka 2017/

18 na kujumuika nasi Bungeni katika Mkutano huu wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni (CCM); Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha (CCM); Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini (CCM); Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM); na Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Jimbo la Longido (CCM). Ushindi walioupata unaonesha imani kubwa ya wananchi kwa Chama cha Mapinduzi. Aidha, naomba kumpongeza Dkt. Adelardus Kilangi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini (CCM) ambaye amechaguliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Bunge la Afrika. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita, Mbunge wa Handeni Vijijini (CCM) kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa *Caucus* ya Vijana ya Bunge la Afrika. Ushindi wao umeleta heshima kubwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu wake, Mheshimiwa Jitu Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, kwa ushauri wao mahiri na wa kizalendo uliotusaidia kuboresha kwa kiasi kikubwa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwako, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini (CCM) na Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, aliyekuwa Mbunge wa Buyungu (CHADEMA). Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu matano. Kwanza ni utangulizi; pili ni mwenendo wa hali ya uchumi wa Taifa katika mwaka 2017 na robo ya kwanza ya mwaka 2018; tatu ni muhtasari wa mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18; nne ni maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19; na tano yatakuwa ni majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa hali ya uchumi mwaka 2017. Nitaanza na uchumi wa dunia. Katika mwaka 2017, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.7 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 3.1 mwaka 2016. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa uwekezaji, biashara na uzalishaji viwandani na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani ya bidhaa na huduma kwa nchi zilizoendelea pamoja na kuimarika kwa uchumi wa nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka kufikia wastani wa asilimia 3.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2016. Ongezeko hili lilitokana na kushuka kwa viwango vya kubadilishia fedha za kigeni; kuondolewa kwa ruzuku; kupanda kwa kodi; na kuongezeka kwa wastani wa bei za bidhaa mbalimbali ikiwemo nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kuwa asilimia 1.7 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 0.8 mwaka 2016. Hata hivyo, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia ulipungua na kuwa asilimia 2.6 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2016. Kupungua kwa mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia kulitokana na kushuka kwa bei za vyakula na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Afrika na Kikanda. Kwa upande wa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa asilimia 2.8 mwaka 2017 ambapo uliongezeka kutoka asilimia 1.4

mwaka 2016. Matarajio ni kufikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2018. Matarajio hayo ya ongezeko la ukuaji wa uchumi yametokana na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji wa madini na uzalishaji wa mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 11.0 ikilinganishwa na asilimia 11.3 mwaka 2016. Kushuka kwa mfumuko wa bei kwa nchi hizo kulichangiwa zaidi na kuimarika kwa sera za fedha na kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni pamoja na upatikanaji mzuri wa chakula uliotokana na hali nzuri ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki katika mwaka 2017 ulikua kwa wastani wa asilimia 1.9 na uchumi wa Tanzania ndiyo uliokua kwa kasi zaidi ikilinganishwa na nchi nyingine katika jumuiya hiyo, ukikua kwa wastani wa asilimia 7.1, ikifuatiwa na Rwanda, uchumi wake ulikua kwa asilimia 6.1; Kenya asilimia 4.8; Uganda asilimia 4.5, Burundi asilimia 0.0 na uchumi wa Sudan Kusini ulipungua kwa asilimia 11.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi zaidi kufikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2018. Ongezeko la kasi la ukuaji linatarajiwa kutokana na maboresho yanayoendelea kufanyika na hususani katika sera na taratibu za uwekezaji na uendeshaji biashara. Sanjari na maboresho ya sera, Serikali za nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimepanga kutekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati ya uimarishaji wa miundombinu ikijumuisha miradi ya bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Bandari ya Tanga Nchini kwetu Tanzania na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* ambayo inaunganisha Tanzania, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo *(DRC),* Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2017 na robo ya kwanza (Januari - Machi, 2018), mwenendo wa mfumuko wa bei katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki uliendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja isipokuwa kwa nchi ya Burundi. Kati ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Uganda ilikuwa na wastani mdogo zaidi wa mfumuko wa bei wa asilimia 5.0 ikifuatiwa na Tanzania ambayo ilikuwa na wastani wa asilimia 5.1, Rwanda asilimia 6.6, Kenya asilimia 7.3 na Burundi asilimia 13.1. Hali hii ilichangiwa na mwenendo imara wa ugavi wa chakula katika Ukanda wetu wa Afrika Mashariki pamoja na kutobadilika kwa bei za nishati ya mafuta katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Nchi Wanachama wa *SADC* ulikua kwa asilimia 2.8 mwaka 2017 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 2.7 mwaka 2016. Aidha, katika mwaka 2018, uchumi wa Nchi za *SADC* unatarajiwa kukua kwa kasi ya asilimia 3.1 na hii itatokana na matarajio ya kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kufuatia mwenendo mzuri wa hali ya hewa katika mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Taifa. Pato halisi la Taifa kwa mwaka 2017 lilifikia shilingi trilioni 50.5 ikilinganishwa na shilingi trilioni 47.1 mwaka 2016 na hii ni sawa na ukuaji wa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2016. Ukuaji huu ulitokana na jitihada za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu; kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya madini na kuimarika kwa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi husika, shughuli za uchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na uchimbaji wa madini na mawe ambao ulikuwa kwa asilimia 17.5; usambazaji wa maji asilimia 16.7; uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 16.6; habari na mawasiliano asilimia 14.7 na ujenzi asilimia 14.1. Shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na misitu

zilikua kwa asilimia 3.6 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2016. Aidha, shughuli za utawala zilipungua kwa asilimia 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya kilimo, ukuaji ulitokana na kupatikana kwa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mazao; kuongezeka kwa huduma za ugani na upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo. Aidha, kupungua kwa shughuli za utawala kulitokana na kushuka kwa gharama za mishahara ya watumishi wa umma wasiokuwa na sifa, watumishi hewa na makosa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa sekta za kiuchumi katika pato la Taifa. Kwa upande wa mchango katika pato la Taifa katika mwaka 2017, shughuli za huduma ikijumuisha huduma za msingi katika jamii, utalii, ulinzi, habari na fedha zilichangia asilimia 37.5 ikilinganishwa na asilimia 39.2 mwaka 2016. Aidha, shughuli za kilimo zilichangia asilimia 30.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 29.2 mwaka 2016. Vilevile shughuli za uzalishaji viwandani na ujenzi zilichangia asilimia 26.4 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 24.9 mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa pato la kila mtu. Pato la wastani la kila mtu Tanzania Bara lilifikia Sh.2,275,601 kutoka Sh.2,086,168 mwaka 2016 na hili ni sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 9.1. Kiasi hicho cha pato la wastani kwa kila mtu kwa mwaka 2017 ni sawa na Dola za Marekani 1,021 ikilinganishwa na Dola za Marekani 958 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa bei. Katika mwaka 2017 mwenendo wa mfumuko wa bei ulikuwa tulivu kutokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula nchini; utulivu wa bei za nishati hasa mafuta katika soko la ndani na nje ya nchi; na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na

za bajeti. Wastani wa mfumuko wa bei *(annual average inflation)* kwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2016. Aidha, mwenendo wa mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 5.2 Januari, 2017 hadi kufikia asilimia 4.0 Desemba, 2017. Vilevile katika kipindi cha Januari hadi Aprili, 2018, mfumuko wa bei umeendelea kupungua kutoka asilimia 4.0 Januari hadi asilimia 3.6 Mei, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujazi wa fedha na karadha. Katika kipindi cha mwaka unaoishia Desemba, 2017, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi *(M3)* na *M3* inajumuisha fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mfumo wa kibenki; amana binafsi zilizo kwenye mabenki zinazohamishika kirahisi; amana za akiba na za muda maalum; na akiba ya fedha za kigeni. Kwa hiyo, ujazi wa fedha kwa tafsiri hii pana *M3* ulifikia shilingi bilioni 24,711.3 kutoka shilingi bilioni 22,877.6 Desemba 2016 sawa na ongezeko la asilimia 8.0. Ukuaji huu ulikuwa juu ya kiwango cha ukuaji wa asilimia 3.8 kwa mwaka ulioishia Desemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la rasilimali katika fedha za kigeni kwenye Benki Kuu ya Tanzania ambazo zilikuwa kwa asilimia 41.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.7 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania za kuongeza ukwasi katika sekta ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa viwango vya riba. Katika mwaka 2017 mwenendo wa viwango vya riba uliongezeka ambapo riba za mikopo zilifikia wastani wa asilimia 18.42 kutoka wastani wa asilimia 15.66 mwaka 2016. Riba za mikopo ya mwaka mmoja ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.24 kutoka wastani wa asilimia 12.87 mwaka 2016. Kwa upande mwingine, riba za amana za muda maalum ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 9.62 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 8.78 mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, riba za amana za mwaka mmoja zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 10.86 kutoka wastani wa asilimia 11.03 mwaka 2016. Kutokana na mwendo huu, tofauti kati ya riba za amana na za mikopo za mwaka mmoja iliongezeka kufikia wastani wa asilimia 7.38 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 1.83 mwaka 2016. Riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara imebakia kuwa juu kutokana na benki hizo kuweka tahadhari kubwa kwa wateja wanaoshindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati na kuongezeka kwa mikopo chechefu *(non-performing loans).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.26 mwishoni mwa mwaka 2017 kutoka asilimia 13.49 mwaka 2016. Vilevile riba za dhamana za Serikali zilipungua kufikia wastani wa asilimia 8.19 mwaka 2017 kutoka asilimia 15.12 mwaka 2016. Aidha, riba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 2.0 mwishoni mwa Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa thamani ya shilingi. Katika kipindi cha mwaka ulioishia Desemba, 2017, mwenendo wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani uliendelea kuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha mwezi Desemba, 2017, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh.2,228.86 ikilinganishwa na wastani wa Sh.2,177.07 katika kipindi kama hicho mwaka 2017, ikiwa ni tofauti ya wastani wa Sh.57.79.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu ulitokana na kuboreshwa kwa usimamizi pamoja na utekezaji wa sera thabiti za bajeti na za fedha *(prudent fiscal and monetary policies)* pamoja na mwenendo mzuri wa urari wa mapato ya fedha za kigeni. Aidha, katika kipindi cha mwezi Machi, 2018 dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh.2,246.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017, amana katika benki za biashara ziliongezeka hadi shilingi bilioni 20,381.9

ikilinganishwa na shilingi bilioni 18,766.5 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 8.6. Ongezeko hili lilitokana na jitihada za benki na Serikali kuhimiza wananchi kutumia huduma za benki katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuendelea kuongezeka kwa matawi ya benki nchini ikiwa ni pamoja na matumizi ya wakala wa benki *(agent banking).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho sekta binafsi ilikuwa na jumla ya shilingi bilioni 19,821.3 sawa na asilimia 97.2 ya amana zote. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni ikilinganishwa na amana zote ulipungua na kufikia asilimia 29.9 mwaka 2017 kutoka asilimia 31.1 mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi. Mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi mwaka 2017 iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 16,883.1 kutoka shilingi bilioni 16,808.9 mwaka 2016. Kiasi hicho ni sawa na ukuaji wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.2 mwaka 2016. Mwenendo huu ulichangiwa na tahadhari zilizochukuliwa na benki za biashara kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu pamoja na benki za biashara kupendelea zaidi kuwekeza katika dhamana za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza ukwasi kwenye uchumi na kuimarisha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Hatua hizo ni pamoja na kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na mabenki ya biashara *(Statutory Minimum Reserve Requirement);* kupunguza riba za Benki Kuu *(discount rate);* kupunguza riba za dhamana za Serikali; na Serikali kuendelea kulipa malimbikizo ya madeni kwa wakandarasi na watoa huduma wa hapa nchini waliokuwa wamekopa katika benki za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, benki za biashara zimeendelea kutumia mfumo wa kuhifadhi taarifa za wakopaji ili kupunguza vihatarishi katika kutoa mikopo

mipya kwa sekta binafsi. Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2018 mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi ulikua kwa wastani wa asilimia 1.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji wa rasilimali. Aya ya 28 katika kitabu cha hotuba yangu, imeainisha mwenendo wa ukuzaji wa rasilimali kwa mwaka 2017, ambapo mwenendo ulikuwa mzuri na uliendelea kuongezeka kwa asilimia 19.5 kwa bei za mwaka 2007. Sekta binafsi ikiongoza juhudi hizo kwa kuchangia asilimia 74.9 ya rasilimali za kudumu na Serikali ikichangia asilimia 25.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 29 mpaka ya 32 katika kitabu cha hotuba yangu imebainisha mwenendo wa sekta ya nje ambao ni wa kuridhisha. Urari wa malipo yote *(balance of payments)* ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,649.5; urari wa biashara ya huduma *(balance of trade and services)* ulikuwa na ziada ya dola za Marekani 1,909.7; na nakisi katika urari wa malipo ya kawaida *(current account)* unajumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho wa mali wa kawaida, ilipungua kwa asilimia 43.8 na kufikia dola za Marekani milioni 1,210.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,154.6 mwaka 2016. Mwenendo huu umetokana na kupungua kwa malipo nje ya nchi yanayohusiana na usafirishaji hususan mizigo pamoja na kushuka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje na malipo ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa akiba ya fedha za kigeni, katika kipindi cha mwaka 2017, akiba yetu ilifikia dola za Marekani milioni 5,906.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,325.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kiasi hicho kilikuwa kinaweza kulipia gharama za kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 5.4 na hivyo kupita kiwango kilichowekwa katika hatua za mtangamano wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki cha angalau miezi minne na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni kulitokana na jitihada za Benki Kuu ya Tanzania

kuendelea kununua fedha za kigeni kutoka katika soko la ndani, upatikanaji wa fedha za mikopo ya kibiashara *(external non-concessional loans)* na kushuka kwa gharama za uingizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maisha ya watu. Katika aya ya 33 mpaka ya 34 ya kitabu cha hotuba yangu, tumeainisha mabadiliko ya hali ya maisha ya watu kwa kina. Kwa mujibu wa taarifa ya makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2018, Tanzania ina wastani wa ongezeko la watu la asilimia 3.1 kwa mwaka. Idadi ya watu inakadiriwa kuongezeka kutoka watu milioni 49.0 mwaka 2016 hadi watu milioni 52.6 mwaka 2017 na matarajio ni kufikia watu milioni 54.2 mwaka huu wa 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 34 ya kitabu cha hotuba yangu, tunaeleza kuwa viwango vya vifo vimeendelea kupungua kutoka wastani wa vifo 9.0 kwa kila watu 1,000 mwaka 2013 hadi vifo 7.2 mwaka 2017. Wastani wa vizazi kwa wanawake kati ya miaka 15 hadi 49 ulipungua kutoka wastani wa watoto 5.3 mwaka 2013 hadi watoto 5.1 mwaka 2017. Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka vifo 42.8 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2013 hadi kufikia vifo vya watoto 34.5 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 24.6 mwaka 2015/2016. Malengo ya Serikali ni kuendelea kupunguza kiwango cha umaskini hadi kufikia asilimia 16.7 na asilimia 12.7 mwaka 2020 na mwaka 2025 kwa mtiririko huu. Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha upatikanaji wa takwimu mbalimbali hususan zitakazotoa viashiria vinavyotumika kutathmini mwenendo wa hali ya umaskini nchini kupitia utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi wa mwaka 2017/2018 ambao unaendelea nchini hivi sasa. Utafiti huu ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano utatoa picha halisi ya hali ya umasikini nchini ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha utoaji wa huduma za jamii husussan huduma za afya, elimu, maji na upatikanaji wa umeme kama ambavyo tumeainisha katika aya ya 37 mpaka aya ya 40 ya kitabu cha hotuba ambapo katika huduma za afya maambukizi ya malaria yamepungua kutoka asilimia 14.4 mwaka 2016 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017 na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa watu wenye umri wa miaka 15 mpaka 49 yameendelea kupungua kutoka asilimia 5.8 mwaka 2017/2018 hadi asilimia 4.8 mwaka 2016/2017. Mafanikio haya yametokana na juhudi za Serikali katika uhamasishaji na utoaji elimu dhidi ya malaria na maambukizi ya virusi vya Ukimwi, lakini pia mwitikio mzuri wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, hatua mbalimbali zilizochukuliwa zimepelekea idadi ya wanafunzi waliojiandikisha kujiunga katika shule za msingi na sekondari kuongezeka. Wanafunzi wa shule za msingi waliongezeka kufikia 9,317,791 ikilinganishwa na wanafunzi 8,639,202 mwaka 2016. Kwa upande wa wanafunzi wa sekondari wamefikia 1,908,857 mwaka 2017 ikilinganishwa na wanafunzi 1,806,955 mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma ya maji, upatikanaji wa maji vijijini umefikia takribani asilimia 56.9 na asilimia 72.0 kwa maeneo ya mijini. Aidha, upatikanaji wa huduma ya nishati umeendelea kuboreshwa ambapo uwiano wa idadi ya watu wanaofaidika na huduma ya umeme nchini imefikia asilimia 67.5 mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18. Aya ya 42 mpaka ya 60 katika kitabu cha hotuba yangu, zimeainisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018, ambao ulikuwa ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021. Hivyo, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018 ulijikita katika maeneo makuu manne ya

kipaumbele, ambapo kwanza ilikuwa ni viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; pili, ilikuwa kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu; tatu, kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na nne, kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018 upo katika hatua mbalimbali na umefafanuliwa kwa kina katika hotuba za mipango na bajeti za Mawaziri wa sekta husika. Hivyo, nitaeleza hatua zilizofikiwa kwa baadhi tu ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/2018 na hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, miradi ya kielelezo. Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kielelezo ikiwemo ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* na kufikia utekelezaji wa asilimia kumi; kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania kwa kuongeza ndege mpya moja aina ya *Bombardier Q400;* na kukamilisha maandilizi ya kuanza ujenzi wa mradi wa umeme katika Mto Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ya kielelezo ni pamoja na shamba la miwa na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi, ambapo ujenzi wa kiwanda unaendelea na jumla ya hekta 1,000 kati ya hekta 1,200 zimelimwa ambapo hekta 860 zimepandwa miwa. Hekta 800 kati ya hizo 1,200 za wakulima binafsi zimelimwa ambapo hekta 650 zimepandwa miwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa jitihada za kusomesha wanafunzi kwa wingi kwenye fani na ujuzi adimu na maalumu kwa ajili ya maendeleo ya watu na viwanda na kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu, wanafunzi wamedahiliwa katika fani na ngazi mbalimbali zikiwemo ngazi za stashahada, shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu katika vyuo vikuu na taasisi mbalimbali na pia ufundi stadi ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi katika maeneo ya kipaumbele kama nilivyosema, uko katika hatua mbalimbali na taarifa zake zinapatikana kuanzia aya ya 44 hadi aya ya 58 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2017/2018. Changamoto hizo ni pamoja na kutopatikana kwa mikopo na misaada kwa wakati; kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika ugharamiaji na utekelezaji wa miradi katika mpango. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha ushiriki wa wadau na hususan washirika wa maendeleo kwa kufikia muafaka wa taratibu za kufuata kupitia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo *(Development Corporation Framework)*; kuweka mpango kabambe wa kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuchochea ushiriki mpana wa sekta binafsi; kubainisha miradi itayotekelezwa kwa mfumo wa ubia; kuwa na mfumo shirikishi wa majadiliano na wabia; na kuweka taratibu zitakazoongeza upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo na miradi ya kipaumbele kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019. Katika kufikia malengo na shabaha za mpango wa maendeleo ya 2018/2019, msisitizo utaelekezwa kwenye maeneo makuu manne sawia na vipaumbele vya mpango wa maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambapo kwanza itakuwa ni viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, miradi itakayopewa msukumo wa kipekee ni pamoja na:-

(a) Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma; kiwanda cha kufua chuma cha Liganga; shamba la miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; ujenzi wa mtambo wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika; uanzishwaji wa kanda maalum za kiuchumi; na Eneo Maalum la uwekezaji Kurasini. *(Makofi)*

(b) Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Katika eneo hili, msukumo utakuwa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya hususan huduma za kibingwa; elimu na ujuzi; huduma za ustawi wa jamii; upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe bora; na kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama vijijini na mijini.

(c) Mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara. Miradi itakayopewa msukumo wa kipekee katika eneo hili ni pamoja na ujenzi wa bwawa na mtambo wa kufua umeme kwa kutumia maji Mto Rufiji; ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda mpaka bandari ya Tanga; kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi asilia kuwa kimiminika; kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge;* na kuboresha Shirika la Ndege, Tanzania.

(d) Kuimarisha utekelezaji wa mipango na miradi. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha kwa maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi kwa kutekeleza kwa kikamilifu mapendekezo ya mkakati wa ugharamiaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo; kuweka vigezo vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji; na kuimarisha mifumo ya kitaasisi kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa kuzingatia mwongozo wa usimamizi wa uwekezaji wa umma.

(e) Kuhamishia Makao Makuu ya shughuli za Serikali Kuu Dodoma. Serikali inashirikiana na wadau ikiwemo sekta binafsi na Mashirika ya Kimataifa kujenga Jiji la Dodoma. Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu upatikanaji wa maeneo ya kujenga Ofisi na nyumba za viongozi wa Serikali kwa kuzingatia mahitaji na maboresho ya mpango wa ardhi katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya ziada kuhusu miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2018/2019 yanapatikana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 27 hadi 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2018/2019. Aya ya 65 mpaka ya 66 katika kitabu cha hotuba yangu zimeainisha vihatarishi *(risks)* vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa mpango na hatua za kukabiliana navyo. Vihatarishi hivyo ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha; ushiriki wa sekta binafsi usiokidhi; na ongezeko kubwa la idadi ya watu. Katika kutekeleza mpango huu, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeweka tahadhari zifuatazo: kuongeza ukusanyaji wa mapato; kushirikiana na wadau kubuni vyanzo vipya; na kuimarisha nidhamu katika usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali inaendelea kujadiliana na sekta binafsi katika kukuza uwekezaji; kuhamasisha matumizi ya tekonolojia sahihi katika uzalishaji ili kuongeza uzalishaji na kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugharamiaji wa Mpango wa Mwaka 2018/2019. Aya ya 67 mpaka ya 71 katika kitabu cha hotuba yangu zimeainisha ugharamiaji wa Mpango na vyanzo mbalimbali wa 2018/2019 vikiwemo mapato yatokanayo na kodi; mapato yasiyo ya kodi; mikopo na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo; uwekezaji wa Mashirika ya umma na vyanzo bunifu vikiwemo kuimarisha utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; uuzaji wa dhamana za Serikali katika masoko ya Kimataifa; uvuvi wa bahari kuu; na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi. Maelezo ya kina kuhusu ugharamiaji wa Mpango yanapatikana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 54 hadi 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji tathmini na utoaji wa taarifa. Katika aya ya 72 mpaka 76 katika kitabu cha hotuba yangu, tumeainisha ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019. Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utatumika ambapo unaanisha majukumu ya ufuatiliaji, uratibu, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati pamoja na upatikanaji wa taarifa za uhakika zitakazotumika kupima mafanikio. Maelezo ya ziada kuhusu ufuatiliaji, tathmini na

utoaji taarifa yapo kwenye kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 57 hadi 58.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majumuisho. Azma ya Serikali ni kuchochea ujenzi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kutekeleza mapendekezo ya vyanzo bunifu vilivyoainishwa katika mkakati wa ugharamiaji, taarifa za Kamati za Bunge na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uchumi wa viwanda, msukumo ni kuanzisha na kufufua viwanda vitakavyotumia malighafi za hapa nchini, vitakavyozalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi na vitakavyozalisha ajira mpya kwa Watanzania na hususan vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara za Serikali na Taasisi zinazojitegemea kwa ushirikiano wao wakati wa maandalizi ya kutayarisha Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019. Aidha, kipekee nawashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Dotto Mgosha James kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wote wa Tanzania kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2018/2019 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango *www.mof.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, wajadili

na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. PHILIP I. MPANGO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2017 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2018/19 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**1.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19.

**2.** **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kushiriki Mkutano huu wa 11 wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa na afya njema, amani na utulivu. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtapokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 na kuishauri serikali kwa uzalendo ili kuhakikisha tunafikia malengo ya Taifa ya "Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu".

3. **Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri. Chini ya usimamizi wao wa dhati, Mipango na Programu mbalimbali za Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, zimetekelezwa kiasi cha kuridhisha na Taifa limepiga hatua kubwa kimaendeleo kuelekea malengo ya Dira yetu ya maendeleo ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025. Aidha, uongozi wao umedhihirisha kwamba, ushindi katika vita dhidi ya rushwa, ufisadi, uzembe na ukwepaji kodi inawezekana. Hivyo, juhudi hizi zinapaswa kuungwa mkono na wananchi wote kwa ujumla.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika mwaka 2017/18 na kujumuika nasi Bungeni katika mkutano huu wa Bunge ambao ni: Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni (CCM); Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Ole Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha (CCM); Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini (CCM); Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM); na Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Jimbo la Longido (CCM). Ushindi walioupata unaonesha imani kubwa ya wananchi kwa Chama cha Mapinduzi. Aidha, naomba kumpongeza Dkt. Adelardus Lubango Kilangi, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchuka fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini (CCM), ambaye amechaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita, Mbunge wa Handeni Vijijini (CCM), kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Vijana wa Bunge la Afrika. Ushindi wao umeleta heshima kubwa katika Taifa letu.

6. **Mheshimiwa Spika,** kipekee ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM) na Makamu wake Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini (CCM) kwa ushauri wao mahiri na wa kizalendo uliotusaidia kuboresha kwa kiasi kikubwa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19.

7. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwako, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kuondokewa na wabunge wenzetu, Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini (CCM) na Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago aliyekuwa Mbunge wa Buyungu (CHADEMA). Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina!

8. **Mheshimiwa Spika,** hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu matano (5): kwanza ni utangulizi, pili ni mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2017 na robo ya kwanza ya 2018; tatu, ni Muhtasari wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18; nne, ni Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19; na tano, ni Majumuisho.

## MWENENDO WA HALI YA UCHUMI 2017

### Uchumi wa Dunia

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2017, Uchumi wa Dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.7 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 3.1 mwaka 2016. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa uwekezaji, biashara na uzalishaji viwandani na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani ya bidhaa na huduma kwa nchi zilizoendelea pamoja na kuimarika kwa uchumi wa nchi zinazoendelea.

10. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2017 mfumuko wa bei wa Dunia uliongezeka kufikia wastani wa asimilia 3.1

ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2016. Ongezeko hili lilitokana na kushuka kwa viwango vya kubadilishia fedha za kigeni, kuondolewa kwa ruzuku, kupanda kwa kodi na kuongezeka kwa wastani wa bei za bidhaa mbalimbali ikiwemo nishati. Mfumuko wa Bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kuwa asilimia 1.7 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 0.8 mwaka 2016. Hata hivyo, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia ulipungua na kuwa asilimia 2.6 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2016. Kupungua kwa mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia kulitokana na kushuka kwa bei za vyakula na mafuta.

**Uchumi wa Afrika na Kikanda**

**11. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa asilimia 2.8 mwaka 2017 ambapo uliongezeka kutoka asilimia 1.4 mwaka 2016. Matarajio ni kufikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2018. Matarajio hayo ya ongezeko la ukuaji wa uchumi yametokana na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji madini na uzalishaji wa mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani.

**12. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2017, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 11.0 ikilinganishwa na asilimia 11.3 mwaka 2016. Kushuka kwa mfumuko wa bei kwa nchi hizo kulichangiwa zaidi na kuimarika kwa sera za fedha na kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni pamoja na upatikanaji mzuri wa chakula uliotokana na hali nzuri ya hewa.

**13. Mheshimiwa Spika,** uchumi wa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2017 ulikua kwa wastani wa asilimia 1.9. Uchumi wa Tanzania ulikua kwa kasi zaidi, ikilinganishwa na nchi nyingine katika Jumuiya hiyo kwa wastani wa asilimia 7.1, ikifuatiwa na Rwanda asilimia 6.1, Kenya asilimia 4.8, Uganda asilimia 4.5, Burundi asilimia 0.0. na Uchumi wa Sudan Kusini ulipungua kwa asilimia 11.1. Uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi

zaidi kufikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2018. Ongezeko la kasi ya ukuaji linatarajiwa kutokana na maboresho yanayoendelea kufanyika, hususan, katika sera na taratibu za uwekezaji na uendeshaji biashara. Sanjari na maboresho ya sera, Serikali za nchi wanachama zimepanga kutekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati ya uimarishaji wa miundombinu ikijumuisha miradi ya bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi bandari ya Tanga (Tanzania) na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge ambayo inaunganisha Tanzania, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Uganda.

14. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2017 na robo ya kwanza (Januari hadi Machi) 2018, mwenendo wa mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki uliendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja isipokuwa kwa nchi ya Burundi. Kati ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Uganda ilikuwa na wastani mdogo zaidi wa mfumuko wa bei wa asilimia 5.0 ikifuatiwa na Tanzania ambayo ilikuwa wastani wa asilimia 5.1, Rwanda asilimia 6.6, Kenya asilimia 7.3 na Burundi asilimia 13.1. Hali hii ilichangiwa na mwenendo imara wa ugavi wa chakula katika ukanda huo pamoja na kutobadilika kwa bei za nishati ya mafuta katika soko la Dunia.

15. **Mheshimiwa Spika,** uchumi wa nchi wanachama wa SADC ulikua kwa asilimia 2.8 mwaka 2017 ikilinganisha na ukuaji halisi wa asilimia 2.7 mwaka 2016. Aidha, wa Mwaka 2018, uchumi wa nchi za SADC unatarajiwa kukua kwa kasi ya asilimia 3.1. Hii itatokana na matarajio ya kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kufuatia mwenendo mzuri wa hali ya hewa katika mwaka 2017.

**Uchumi wa Taifa**

**Ukuaji wa Uchumi na Pato la Taifa**

16. **Mheshimiwa Spika**, Pato halisi la Taifa kwa Mwaka 2017 lilifikia Shilingi milioni 50,525,087 ikilinganishwa na Shilingi milioni 47,173,785 mwaka 2016. Hii ni sawa na ukuaji wa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka

2016. Ukuaji huu ulitokana na jitihada za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu, kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya madini na kuimarika kwa sekta ya kilimo. Katika kipindi husika, shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na: Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 17.5); Usambazaji Maji (asilimia 16.7); Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo (asilimia 16.6), Habari na Mawasiliano (asilimia 14.7) na Ujenzi (asilimia 14.1). Shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na misitu ilikua kwa asilimia 3.6 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2016. Aidha, shughuli za utawala zilipungua kwa asilimia 1.3.

**17.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ya Kilimo, ukuaji ulitokana na kupatikana kwa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mazao, kuongezeka kwa huduma za ugani na upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo. Aidha, kupungua kwa shughuli za utawala kulitokana na kushuka kwa gharama za mishahara ya watumishi wa umma wasiokuwa na sifa, watumishi hewa na makosa mengine.

### Mchango wa sekta za kiuchumi katika Pato la Taifa

**18.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mchango katika Pato la Taifa kwa mwaka 2017, shughuli za huduma ikijumuisha huduma za msingi katika jamii, utalii, ulinzi, habari na fedha zilichangia asilimia 37.5 ikilinganishwa na asilimia 39.2 mwaka 2016. Aidha, shughuli za kilimo zilichangia asilimia 30.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 29.2 mwaka 2016. Vile vile, shughuli za uzalishaji viwandani na ujenzi zilichangia kwa asilimia 26.4 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 24.9 mwaka 2016.

### Wastani wa Pato la Kila Mtu

**19.** **Mheshimiwa Spika**, Pato la wastani la kila mtu Tanzania Bara lilifikia shilingi 2,275,601 kutoka shilingi 2,086,168 mwaka 2016 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 9.1. Kiasi hicho cha Pato la wastani kwa kila mtu kwa mwaka 2017 ni sawa na dola za Marekani 1,021 ikilinganishwa na

dola za Marekani 958 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.5.

**Mwenendo wa Bei**

**20. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017, mwenendo wa mfumuko wa bei ulikuwa tulivu kutokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula nchini, utulivu wa bei za nishati hasa mafuta katika soko la ndani na nje ya nchi na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na za bajeti. Wastani wa mfumuko wa bei (*annual average*) kwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2016. Aidha, mwenendo wa Mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 5.2 mwezi Januari 2017 hadi kufikia asilimia 4.0 mwezi Desemba 2017. Vile vile, katika kipindi cha Januari hadi Aprili mwaka 2018 Mfumuko wa bei umeendelea kupungua toka asilimia 4.0 mwezi Januari hadi asilimia 3.6 mwezi Mei mwaka 2018.

**Ujazi wa Fedha na Karadha**

**21. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka unaoishia Desemba 2017, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)[1] kufikia shilingi bilioni 24,711.3 kutoka shilingi bilioni 22,877.6 Desemba 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.0. Ukuaji huu ulikuwa juu ya kiwango cha ukuaji wa asilimia 3.4 kwa Mwaka ulioishia Desemba 2016. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la rasilimali katika fedha za kigeni kwenye Benki Kuu ya Tanzania ambazo zilikua kwa asilimia 41.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.7 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania za kuongeza ukwasi katika sekta ya fedha.

______________________

[1] M3 = M0 + M1 + M2

Ambapo: M0 ni Fedha Msingi;

M1 ni Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Finyu ambayo inajumuisha fedha msingi (M0) na fedha zilizo kwenye mzungukuko na amana binafsi zilizoko kwenye mabenki na zinazohamishika kirahisi; na

M2 ni Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana ambayo inajumuisha M1 na amana za akiba na zamuda maalum.

M3 ni ujazi wa fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi ambayo inajumuisha M2 na akiba ya fedha za kigeni

### Mwenendo wa Viwango vya Riba

**22. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017, mwenendo wa viwango vya riba uliongezeka, ambapo riba za mikopo zilifikia wastani wa asilimia 18.42 kutoka wastani wa asilimia 15.66 mwaka 2016. Riba za mikopo ya mwaka mmoja ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.24 kutoka wastani wa asilimia 12.87 mwaka 2016. Kwa upande mwingine, riba za amana za muda maalum ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 9.62 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 8.78 mwaka 2016. Aidha, riba za amana za mwaka mmoja zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 10.86 kutoka wastani wa asilimia 11.03 mwaka 2016. Kutokana na mwenendo huu, tofauti kati ya riba za amana na za mikopo za mwaka mmoja iliongezeka kufikia wastani wa asilimia 7.38 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 1.83 mwaka 2016. Riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara imebakia kuwa juu kutokana na benki hizo kuweka tahadhari kubwa kwa wateja wanaoshindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati na kuongezeka kwa mikopo chechefu.

**23. Mheshimiwa Spika,** riba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.26 mwishoni mwa mwaka 2017 kutoka asilimia 13.49 mwaka 2016. Vile vile, riba za dhamana za Serikali zilipungua kufikia wastani wa asilimia 8.19 kwa mwaka 2017 kutoka asilimia 15.12 mwaka 2016.

### Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

**24. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka ulioishia Desemba 2017, mwenendo wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani uliendelea kuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha mwezi Desemba 2017, Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,228.86 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,177.07 katika kipindi kama hicho mwaka 2016, ikiwa ni tofauti ya wastani wa shilingi 57.79. Mwenendo huu ulitokana na kuboreshwa kwa usimamizi, pamoja na utekelezaji wa sera thabiti za bajeti na za fedha (*prudent fiscal and monetary policies)* pamoja na mwenendo mzuri wa urari wa mapato ya fedha za kigeni.

**Amana katika Benki za Biashara**

**25. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2017, amana katika benki za biashara ziliongezeka hadi shilingi bilioni 20,381.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 18,766.5 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.6. Ongezeko hili, lilitokana na jitihada za benki na Serikali kuhimiza wananchi kutumia huduma za benki katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi; na kuendelea kuongezeka kwa matawi ya benki nchini ikiwa ni pamoja na matumizi ya wakala wa benki (*agent banking)*. Katika kipindi hicho, sekta binafsi ilikuwa na jumla ya shilingi bilioni 19,821.3 sawa na asilimia 97.2 kati ya amana zote. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni ukilinganishwa na amana zote ulipungua na kufikia asilimia 29.9 mwaka 2017 kutoka asilimia 31.1 mwaka 2016.

**Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi**

**26. Mheshimiwa Spika,** mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi kwa mwaka 2017 iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 16,883.1 kutoka shilingi bilioni 16,608.9 mwaka 2016. Kiasi hicho ni sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.2 mwaka 2016. Mwenendo huu ulichangiwa na tahadhari zilizochukuliwa na benki za biashara kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu pamoja na benki za biashara kupendelea zaidi kuwekeza katika dhamana za Serikali.

**27. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali kupitia Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza ukwasi kwenye uchumi na kuimarisha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Hatua hizo ni pamoja na kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na mabenki ya biashara (*Statutory Minimum Reserve Requirement-SMR*); kupunguza riba ya Benki Kuu (*discount rate*); kupunguza riba za dhamana za Serikali; serikali kuendelea kulipa malimbikizo ya madeni kwa makandarasi na watoa huduma wa hapa nchini waliokuwa wamekopa katika benki za biashara. Aidha, benki za biashara zimeendelea kutumia mfumo wa kuhifadhi taarifa za wakopaji ili kupunguza vihatarishi katika kutoa mikopo mipya kwa sekta binafsi.

**Ukuzaji Rasilimali**

**28. Mheshimiwa Spika,** ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 17.4 mwaka 2017, kufikia shilingi milioni 30,350,457 kutoka shilingi milioni 25,842,956 mwaka 2016. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2007 uliongezeka kutoka shilingi milioni 13,301,873 mwaka 2016 hadi shilingi milioni 15,900,084 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 26.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 25.0 mwaka 2016. Sekta ya umma ilichangia asilimia 25.1 katika rasilimali za kudumu wakati ambapo sekta binafsi ilichangia asilimia 74.9 mwaka 2017.

**Sekta ya Nje**

**Urari wa Malipo Yote**

**29. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2017, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,649.5 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 305.5 mwaka 2016. Ongezeko hili la ziada lilitokana kwa sehemu kubwa na kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida (*current account balance*) pamoja na kuongezeka fedha kwa ajili ya misaada ya maendeleo pamoja na mikopo kutoka nje.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

**30. Mheshimiwa Spika,** Urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,909.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 38.8. Ongezeko hili, lilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za huduma kama vile usafirishaji na usafiri. Aidha, mapato hayo yatokanayo na huduma yaliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 3,927.6 kutoka dola za Marekani milioni 3,607.5 mwaka 2016. Malipo ya huduma yalipungua kwa asilimia 9.6 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,017.9. Hii ilitokana na kupungua kwa malipo nje ya nchi yanayohusiana na usafirishaji, hususan mizigo.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

**31. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2017, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ilipungua kwa asilimia 43.8 na kufikia dola za Marekani milioni 1,210.5, ikilinganishwa na dola 2,154.6 mwaka 2016. Upungufu huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kushuka kwa uagizaji bidhaa kutoka nje na malipo ya huduma pamoja na ongezeko la fedha za msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

**32. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka kinachoishia Desemba 2017, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani milioni 5,906.2 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 4,325.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kiasi hicho kilikuwa kinaweza kulipia gharama za kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 5.4 na hivyo kupita kiwango kilichowekwa katika hatua za mtangamano wa umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki cha angalau miezi minne na nusu (4.5). Kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni kulitokana na jitihada za Benki Kuu kuendelea kununua fedha za kigeni kutoka katika soko la ndani, upatikanaji wa fedha za mikopo ya kibiashara (external non-concessional loans) na kushuka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

**Mabadiliko ya Maisha ya Watu**

**33. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2018, Tanzania ina wastani wa ongezeko la watu la asilimia 3.1 kwa Mwaka. Makadirio haya yamezingatia; wastani wa umri wa kuishi, viwango vya vifo miongoni mwa watoto wachanga, kasi ya uhamiaji na maambuzi ya virusi vya UKIMWI. Idadi ya watu inakadiriwa kuongezeka kutoka watu milioni 49.0 mwaka 2016 hadi watu milioni 52.6 mwaka 2017 na matarajio ni kufikia watu milioni 54.2 mwaka 2018. Katika kuhakikisha kuwa idadi ya watu inaendana na kuongezeka kwa uzalishaji na tija katika uchumi, pana haja ya kuongeza juhudi za kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa huduma mbalimbali

za jamii zikiwemo; elimumsingi bila ada, mafunzo na huduma za afya ya uzazi wa mpango, fursa za ajira, upatikanaji wa maji safi na miundombinu ya maji taka, miundombinu ya barabara, umeme vijijini pamoja na uboreshaji wa nyumba na makazi na usafi wa mazingira.

**34.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia makadirio hayo wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka wastani wa miaka 62.2 mwaka 2013 hadi miaka 64.4 mwaka 2017. Matarajio ni kuendelea kuboresha huduma za kijamii ili mwaka 2020 Mtanzania aweze kuishi kwa wastani wa miaka 66.1. Vile vile, viwango vya vifo vimeendelea kupungua kutoka wastani wa vifo 9.0 kwa kila watu 1,000 mwaka 2013 hadi vifo 7.2 mwaka 2017 na matarajio ni kuendelea kupungua hadi vifo 6.8 kwa mwaka 2018. Vile vile, wastani wa vizazi hai ulipungua kutoka wastani wa vizazi 39.2 kwa kila watu 1,000 mwaka 2013 hadi vizazi 37.6 mwaka 2017 na matarajio ni kuendelea kupungua hadi vizazi 37.2 mwaka 2018. Wastani wa vizazi kwa wanawake kati ya miaka 15 hadi 49 ilipungua kutoka wastani wa watoto 5.3 mwaka 2013 hadi watoto 5.1 mwaka 2017. Aidha, vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka vifo 42.8 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2013 hadi kufikia watoto 34.5 mwaka 2017 na matarajio ni kuendelea kupungua hadi kufikia 32.6 mwaka 2018.

**35.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza sera na mipango madhubuti ya kuboresha maisha ya watu na kupunguza hali ya umaskini nchini. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (HBS) umeonesha umaskini umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 24.6 mwaka 2015/16. Malengo ya Serikali ni kuendelea kupunguza kiwango cha umaskini hadi kufikia asilimia 16.7 na asilimia 12.7 mwaka 2020 na 2025 kwa mtiririko huo. Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha upatikanaji wa Takwimu mbalimbali hususan zitakazotoa viashiria vinavyotumika kutathmini mwenendo wa hali ya umasikini nchini kupitia Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017/18 unaoendelea nchi nzima. Utafiti huu ambao

hufanyika kila baada ya miaka mitano utatoa picha halisi ya hali ya umaskini nchini kwa sasa.

**36.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha utoaji wa huduma za jamii, hususan huduma za afya, elimu, maji na upatikanaji wa umeme.

**37.** **Mheshimiwa Spika**, katika huduma za **Afya:** Shughuli za utoaji huduma za afya na ustawi wa jamii zimeendelea kuimarika nchini kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali. Aidha, Serikali inaendelea na uhamasishaji na utoaji wa elimu ya vita dhidi ya Malaria na maambukizi ya virusi vya Ukimwi. Maambukizi ya Malaria yamepungua kutoka asilimia 14.4 mwaka 2016 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017 na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa watu wenye umri wa miaka 15 - 49 yameendelea kupungua kutoka asilimia 5.8 mwaka 2007/08 hadi asilimia 4.8 mwaka 2016/17.

**38.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Elimu:** Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ambazo zimepelekea idadi ya wanafunzi waliojiandikisha kujiunga katika shule za msingi na sekondari kuongezeka. Wanafunzi wa shule za msingi waliongezeka kufikia 9,317,791 mwaka 2017 ikilinganishwa na wanafunzi 8,639,202 mwaka 2016; na kwa upande wa wanafunzi wa sekondari waliongezeka kufikia 1,908,857 mwaka 2017 ikilinganishwa na wanafunzi 1,806,955 mwaka 2016.

**39.** **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa **Maji**: Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini na mijini. Hadi kufikia Januari 2018, upatikanaji wa maji vijijini umefikia asilimia 56.9 na asilimia asilimia asilimia mijini, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama umeongezeka na kufikia asilimia 72 hadi mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 51.8 mwaka 2007. Aidha, idadi ya wakazi wanaoishi ndani ya umbali wa kilomita moja kutoka kwenye vyanzo vya maji safi na salama ya kunywa imeongezeka hadi kufikia asilimia 78 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 57 mwaka 2007.

**40.** **Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya **Nishati**: Serikali imeweka jitihada za kusambaza umeme kwa kasi kwa wakazi wa vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (Rural Energy Agency - REA). Utafiti wa *Energy Access Situation Survey* wa mwaka 2016 umeonesha kuwa uwiano wa idadi ya watu wanaofaidika na huduma ya umeme nchini ilikuwa asilimia 67.5 mwaka 2016. Hata hivyo asilimia 68.4 ya kaya za vijijini zinategemea umeme wa jua na asilimia 34.5 zinategemea umeme unaozalishwa na TANESCO. Matarajio ni kuongeza kasi ya uzalishaji wa umeme wa gharama nafuu ambao unatokana na gesi asilia na kusambaza kwa wananchi wengi hususan katika ngazi ya kaya.

**41.** **Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu hali ya uchumi yapo katika kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2017.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2017/18

### Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2017/18

**42.** **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2017/18 ulikuwa ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ambao umejielekeza katika kuchochea mageuzi ya uchumi kupitia ujenzi wa viwanda na kuufungamanisha na maendeleo ya watu. Hivyo, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/18 ulijikita katika maeneo makuu manne ya kipaumbele, ambayo ni:-

(i) Viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda;
(ii) Kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu;
(iii) Kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na
(iv) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 upo katika hatua

mbalimbali na umefafanuliwa kwa kina katika hotuba za mipango na bajeti za Mawaziri wa sekta husika. Hivyo, nitaelezea hatua zilizofikiwa kwa baadhi tu ya miradi ya maendeleo wa Mwaka 2017/18. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

**Miradi ya Kielelezo**

**44. Mheshimiwa Spika,** miradi hii imepewa msukumo wa kipekee kwa kuzingatia mchango wake muhimu katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii bila kusahau maendeleo ya viwanda nchini. Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**(i) Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Standard Gauge:** kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300), utekelezaji umefikia asilimia 10. Kwa kipande cha Morogoro – Makutupora (Km 422) malipo ya awali ya mkandarasi yamekamilika na anaendelea na maandalizi ya ujenzi. Vile vile, taratibu za kutafuta fedha zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za Makutupora - Tabora (Km 295), Tabora - Isaka (Km 133), Isaka - Mwanza (Km 250), Tabora – Uvinza – Kigoma (km 411) na Kaliua – Mpanda – Karema (km 321).

**(ii) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**: kwa mwaka 2017/18, Serikali imepokea ndege moja aina ya Bombardier Q400 na kukamilisha malipo ya asilimia 30 ya gharama kwa ndege mbili za aina ya CS 300 na malipo ya asilimia 52 kwa ndege moja kubwa aina ya Boeing 787.

**(iii) Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) – Bandari ya Tanga (Tanzania):** upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kupakulia mafuta umekamilika na wananchi wa Chongoleani - Tanga watakaopisha ujenzi wa bomba wamelipwa fidia; Mabunge ya nchi za Tanzania na Uganda yameridhia mkataba wa *Inter Governmental Agreement- IGA*; na kuendelea na majadiliano ya HGA pamoja na maandalizi ya majadiliano ya mkataba wa ubia (*Shareholding Agreement-SHA)*.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme Mto Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*):** kuendelea na uchambuzi wa zabuni zilizowasilishwa za wakandarasi wa ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi wa njia ya msongo wa Kv 33 kutoka Dakawa hadi eneo la mradi.

**(v) Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi:** Jumla ya hekta 1,000 kati ya 1,200 zimelimwa ambapo hekta 860 zimepandwa miwa; hekta 800 kati ya 1,200 za wakulima binafsi zimelimwa ambapo hekta 650 zimepandwa miwa; kuendelea kufanya maandalizi ya kununua miwa kutoka kwa wakulima wadogo; na kuendelea na ujenzi wa kiwanda.

**(vi) Kusomesha Wanafunzi kwa Wingi Kwenye Fani na Ujuzi Adimu na Maalum kwa ajili ya Maendeleo ya Watu na Viwanda na kukuza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu:** katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili - Kampasi ya Mloganzila: wanafunzi 1,449 wamedahiliwa katika ngazi za stashahada, shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu katika fani za afya ya kinywa na meno, upandikizaji wa ini, upasuaji, afya ya akili, ukunga, uhandisi wa vifaa tiba (*medical engineering*), tiba ya mionzi na sayansi ya maabara. Aidha, watumishi 912 katika vyuo vya: Chuo Kikuu cha Dodoma (377), Chuo Kikuu cha Ardhi (25), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (105), Hospitali ya Taifa Muhimbili (7), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (7), Hospitali ya Benjamin Mkapa – Dodoma (3), Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe (12) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (376) wapo mafunzoni katika ngazi za stashahada, shahada ya kwanza, shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu. Vile vile, watafiti 27 katika Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) wapo masomoni katika ngazi ya shahada ya uzamivu (4) na shahada ya uzamili (23).

**Kujenga Msingi wa Uchumi wa Viwanda**

**45. Mheshimiwa Spika,** miradi ya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda inalenga kuendelea kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini, hususan za kilimo, madini na gesi asilia. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

kuanzisha viwanda vipya vidogo vya aina mbalimbali 429 kupitia **SIDO** ambavyo vimezalisha ajira mpya 1,287; kuendelea na uunganishaji wa matrekta mapya katika kiwanda cha **TAMCO – Kibaha**; kuandaa utaratibu wa uwekezaji unaofaa katika kiwanda cha **General Tyre – Arusha**; kutafuta mbia wa kuwekeza katika Mradi wa Magadi Soda **Bonde la Engaruka – Arusha**; na kuboresha Shirika la utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania **(TIRDO)** kwa kuanzisha na kuimarisha maabara (maabara ya mafuta na gesi, makaa ya mawe na chuma) ili kufikia viwango vya kimataifa.

**46.** **Mheshimiwa Spika,** Maeneo mengine katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ni pamoja na kuendeleza viwanda vya ngozi na pamba hadi nguo. **Ngozi**: vikijumuisha kiwanda cha kutengeneza viatu na bidhaa za ngozi katika Gereza la Karanga (Moshi), Kiwanda cha Viatu cha Bora, Woiso Shoes Company Ltd na Kiwanda cha Mwanza Tennaries Ltd. **Pamba hadi Nguo:** kuboresha uzalishaji katika kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Dar Es Salaam; Kiwanda cha Morogoro Canvas Mill; na Vinu vya Kuchambulia Pamba vya Nyanza Cooperative Union. Vile vile, Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji binafsi hususan katika viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusindika nyama, maziwa, maji, misitu, chokaa, mawe ya urembo, gypsum na mazao ya chakula na matunda.

**Ujenzi wa Miundombinu na Mazingira Wezeshi**

**47.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha miundombinu na huduma za kuchochea uchumi wa viwanda. Miongoni mwa miradi hii ni: Ujenzi wa barabara za kuunganisha makao makuu ya mikoa na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani: barabara za Dodoma – Babati km 251.4 (ujenzi umekamilika), Sumbawanga-Kanazi km 75.0 (ujenzi umekamilika), Kanazi - Kizi-Kibaoni km 76.6 (ujenzi umekamilika), Sitalike-Mpanda km 36.9 (ujenzi umekamilika), Kyaka – Bugene km 59.1 (ujenzi umekamilika), Uyovu – Bwanga km 43 (ujenzi umekamilika)

na ujenzi wa madaraja ya Kilombero (Magufuli) na Kavuu umekamilika. Vile vile, ujenzi wa barabara ya juu ya TAZARA umefikia asilimia 88.82 na ile ya Ubungo *Interchange* inaendelea na maandalizi ya ujenzi.

**48. Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imeendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo: barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi km 413 (sehemu ya Kidahwe - Kasulu km 63 ujenzi umefikia asilimia 56); barabara ya Tabora –Ipole – Koga – Mpanda km 373 (ujenzi umekamilika kwa asilimia 79.1 sehemu ya Tabora – Sikonge km 30 na kusainiwa kwa mikataba kwa vipande vya Sikonge – Ipole – Koga - Mpanda km 343); Daraja la Selander (upembuzi yakinifu unaendelea); na kwa upande wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (awamu ya II, III na IV) jijini Dar es Salaam, mradi upo katika hatua za awali za maandalizi ya ujenzi.

**49. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bandari, hatua iliyofikiwa katika kutekeleza miradi ni: kusainiwa kwa mkataba na kuanza ujenzi kwa bandari ya Dar es Salaam); kukamilika kwa asilimia 20 ya ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300 (*multipurpose terminal*) katika bandari ya Mtwara; kukamilisha mapitio ya upembuzi yakinifu ili kubaini kama mradi unaweza kutekelezwa kwa mfumo wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) kwa bandari Tanga; kuendelea na majadiliano ya uendelezaji wa bandari kati ya Serikali na wawezakaji wa bandari Bagamoyo; kuanza kwa ujenzi wa bandari kavu ya Ruvu; na kuendelea na ujenzi wa gati za Nyamirembe Chato na Magarine katika Ziwa Victoria, gati la Kalya/Sibwesa katika Ziwa Tanganyika na gati la Ndumbi katika Ziwa Nyasa.

**50. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kujenga na kukarabati viwanja vya ndege nchini. Hatua zilizofikiwa katika baadhi ya viwanja hivyo ni kama ifuatavyo: Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa wa Julius Nyerere, ujenzi wa jengo la abiria *(terminal III)* umefikia asilimia 72. Aidha, katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege umeongezwa kwa mita 500 na upanuzi wa maegesho ya ndege umekamilika. Vile vile,

katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, usanifu wa kiwanja unaendelea.

**51.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/18 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme (*installed capacity*) iliyopo nchini umeongezeka kutoka MW 1,450 mwaka 2016/17 na kufikia MW 1,517.47 mwezi Mei, 2018 sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa mitambo sita (6) ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi II .

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeendelea kukamilisha utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA II) kwa kumalizia kazi za nyongeza (*additional scope*) na kuunganisha wateja ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2017 Mradi huo ulikuwa umekamilika kwa asilimia 99. Mradi huu umeweza kufikisha miundombinu katika vijiji 2,598 kati ya 2,697 sawa na asilimia 96.3 na hivyo kuwezesha kuwaunganishia umeme jumla ya wateja 178,641 ambao ni sawa na asilimia 71.46 ya matarajio ya awali ya wateja 250,000. Uunganishwaji huu wa wateja umechangia ongezeko la upatikanaji wa huduma za umeme vijijini (*access*) kufikia asilimia 49.5.

**53.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha sekta ndogo ya madini, Serikali imetekeleza yafuatayo: kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake; kujenga ukuta wa machimbo ya Tanzanite – Mirerani; na kukamilika kwa ukadiriaji wa mashapo ya dhahabu katika leseni za wachimbaji wadogo katika maeneo ya Mpanda (Kapanda-Sikitiko); Mara (Buhemba-Rwabasi); na Tanga (Mukulumuzi, Kiomoni na Kange).

**Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu**

**54.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi unaakisi maendeleo ya watu, Serikali inaendelea kuimarisha sekta za **Elimu** na **Mafunzo ya Ufundi, Afya na Maendeleo ya Jamii** na **Maji**. Katika sekta ya **Elimu na Mafunzo ya Ufundi** Serikali inaendelea: kugharamia Elimumsingi bila ada; kuongeza wigo wa ruzuku na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; kuongeza vifaa kwa

wanafunzi wenye mahitaji maalum; kukarabati na kupanua Maktaba ya Mkoa – Dodoma; na kujenga vyuo vitano vya VETA katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe, Rukwa na Kagera.

**55.** **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya **Afya** Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma zinazotolewa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo ambapo upatikanaji wake umefikia asilimia 92 kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Vile vile, upatikanaji wa dawa muhimu 135 katika Bohari Kuu ya Dawa (MSD) umefikia wastani asilimia 81. Sambamba na hayo, Serikali imeongeza udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza hususan kifua kikuu na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI hasa kwa vijana.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya **Maji,** Serikali imeendelea kuboresha na kupanua huduma za maji vijijini na mijini. Katika kutekeleza azma hiyo, miradi mbalimbali ya maji imetekelezwa ikiwemo: kujenga miundombinu ya maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama, Nzega, Igunga, Tabora hadi Sikonge; na kujenga na kuimarisha hifadhi ya vyanzo vya maji, upandaji miti, kuhimiza matumizi ya teknolojia jadidifu na uhifadhi wa mazingira.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza zoezi la kuhamishia shughuli za Serikali Kuu Dodoma. Awamu ya kwanza na ya pili imekamilika ambapo jumla ya watumishi wa umma 3,829 wamehamia na awamu ya tatu inaendelea. Aidha, katika mwendelezo wa jitihada za kuboresha mji wa Dodoma kuwa wa kisasa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameupandisha hadhi Mji wa Dodoma kuwa Jiji kuanzia tarehe 26 Aprili 2018. Vile vile, Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu upatikanaji wa maeneo

ya kujenga majengo ya Serikali kwa kuzingatia Mpango wa Ardhi wa Jiji la Dodoma.

**Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango**

**58.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Mpango unatekelezwa kwa ufanisi, Serikali inaendelea kutumia Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 ambao unaelekeza namna bora ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mkakati huo unaonesha mpango kazi, ugharamiaji, ufuatiliaji na ufanyaji tathmini pamoja na mbinu mbalimbali za mawasiliano. Mkakati huo wa utekelezaji unapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz).

**Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo**

**59.** **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2017/18, Serikali ilipanga kutumia Shilingi bilioni 11,999.59 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo, ambapo, Shilingi bilioni 8,969.75 zilikuwa za ndani na bilioni 3,029.85 za nje. Hadi Aprili 2018, fedha za bajeti ya maendeleo zilizotolewa ni Shilingi bilioni 5,123.2, sawa na asilimia 42.7 ya bajeti ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 775.8 ni fedha za nje ambapo shilingi bilioni 325.9 zilipokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kupelekwa moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo ya sekta za kilimo, afya, nishati, elimu, mazingira na maliasili na utalii inayotekelezwa na Wizara, Idara zinazojitegemea na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**60.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na: Kufanya mapitio ya sera, sheria na taratibu zinazochochea ushiriki wa sekta binafsi; kutenga maeneo mahsusi ya uwekezaji (EPZ, SEZ na kukamilisha taratibu za kuanzisha *land bank* chini ya TIC) ili kupunguza usumbufu kwa sekta binafsi; kujenga miundombinu wezeshi (barabara, umeme, maji na reli) ili kurahisha uwekezaji; na kuimarisha mifuko maalum ya kuchochea ushiriki wa sekta binafsi, kwa mfano *SAGCOT Catalytic Fund na PPP Facilitation Fund*.

**Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya 2017/18 na hatua za kukabiliana nazo.**

**61.** **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/18 umekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa Mikopo na misaada kwa wakati; kutofikiwa kwa malengo ya mapato mengine; na ushiriki mdogo wa sekta binafsi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: kuimarisha ushiriki wa wadau hususan washirika wa maendeleo kwa kufikia muafaka wa taratibu za kufuata kupitia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Corporation Framework – DCF); kuweka mpango kabambe wa kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuchochea ushiriki mpana wa Sekta Binafsi; kubainisha miradi itakayotekelezwa kwa mfumo wa ubia; kuwa na mfumo shirikishi wa majadiliano na wabia; na kuweka taratibu zitakazoongeza upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

**62.** **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yapo katika kitabu cha Mpango (Sura ya Tatu).

**Maeneo na Miradi ya Kipaumbele 2018/19**

**63.** **Mheshimiwa Spika,** Mpango huu ni wa tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 wenye dhima ya *Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu.* Katika kufikia malengo na shabaha za Mpango, msisitizo unaelekezwa kwenye maeneo makuu manne ambayo ni:

**(a)** **Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda**: Lengo ni kuendelea kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini, hususan za kilimo, madini na gesi asilia. Katika eneo hili, miradi itakayopewa msukumo wa kipekee ni pamoja na: Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma; Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga; Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari

Mkulazi; Ujenzi wa mtambo wa kusindika Gesi asilia kuwa kimiminika; uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; na Eneo Maalum la Uwekezaji Kurasini. Aidha, Serikali itaendelea na: ujenzi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta – TAMCO, Kibaha; kukamilisha maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Viwanda vya Nguo TAMCO; Kuboresha Shirika la Nyumbu; kukamilisha maandalizi ya awali ya utekelezaji wa Mradi wa Magadi Soda - Bonde la Engaruka; Kufufua Kiwanda cha General Tyre – Arusha; kuboresha Kituo cha zana za Kilimo na Ufundi Vijijini – CAMARTEC, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania-TIRDO, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo –TEMDO; na Uendelezaji wa Viwanda Vidogo – SIDO.

Vile vile, katika kuweka misingi ya uchumi wa viwanda, Serikali inaendelea kuimarisha sekta za **Kilimo**: kwa kusaidia upatikanaji wa maafisa ugani, pembejeo na masoko; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; kuimarisha vyuo vya mafunzo ya kilimo; kutafiti mbegu bora zinazotoa mazao kwa wingi. Kwa upande wa sekta ya **Mifugo**: serikali inaendelea na usimamizi wa ardhi na upatikananji wa malisho; kutoa tiba na kuthibiti magonjwa ya mifugo. Katika sekta ya **Uvuvi**: Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya kufugia samaki; kuimarisha na kuendeleza ulinzi wa rasimali za uvuvi na mazingira; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi. Katika eneo la **Misitu**: Serikali itaimarisha mapori tengefu na vitengo vya kupambana na ujangili nchini; usimamizi endelevu wa maliasili; na kusaidia uendelezaji wa misitu binafsi na mnyororo wa thamani. Katika sekta ya **Madini**: Serikali itaendelea kusimamia rasilimali za madini; ujenzi wa *smelters* na *refineries* na ujenzi wa vituo vya umahiri.

**(b) Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu:** Eneo hili linalenga kuendeleza mafanikio ya ustawi wa maisha ya watanzania hasa wa vijijini. Msukumo utakuwa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya hususan huduma za kibingwa; elimu na ujuzi; huduma za ustawi wa jamii; upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe bora; kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama vijijini na mijini; kusimamia rasilimali za maji nchini;

na kuimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi unaakisi maisha ya watu, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ya **Elimu**: elimumsingi bila ada; Ukarabati wa Maktaba za Mikoa; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu; Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu; Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH; Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi Vya Wilaya na Mikoa; Mafunzo kwa Vitendo na Vyakula Vyuoni; Kuendeleza Elimu ya Ualimu; Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Ujenzi na Ukarabati wa miundombinu ya vyuo vikuu; Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH; Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini. Kwa upande wa **Afya**: kuboresha Hospitali za Rufaa na mikoa pamoja na Taasisi za Utafiti katika sekta ya afya. Katika eneo la **Maji Safi na Usafi wa Mazingira**: Kuboresha Huduma za Maji Dar es Salaam; Maji kutoka Ziwa Victoria; Miradi ya Maji ya Kitaifa; Kuboresha Huduma za Maji Vijijini; Kuboresha Huduma za Maji Mijini; Ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati ya Kidunda, Farkwa na Ndembera.

**(c) Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara:** Eneo hili linalenga kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu, ikijumuisha miundombinu ya nishati, usafirishaji (reli, barabara, madaraja, viwanja vya ndege na bandari) na ununuzi na ukarabati wa meli na vivuko. Miradi iliyopewa msukumo wa kipekee katika eneo hili ni pamoja na: ujenzi wa bwawa na mtambo wa kufua umeme wa *Rufiji Hydro Power Project*; ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda - bandari ya Tanga; kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi asilia kuwa kimiminika; kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*; na kuboresha Shirika la Ndege Tanzania.

Aidha, Serikali itaendelea: kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Reli; kujenga na kukarabati Barabara zenye kufungua Fursa za Kiuchumi na zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani; kujenga miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (awamu ya II, III na IV) katika jiji la Dar es Salaam; kujenga Barabara

za Juu (Flyover) jijini Dar es Salaam na kujenga Barabara za vijijini na mijini. Vile vile, Serikali itaendelea: kujenga na kukarabati madaraja; kuboresha usafiri majini na anga; kujenga na kukarabati Bandari; kuboresha huduma ya teknolojia ya habari na mawasiliano; kujenga miundombinu ya kuzalisha na kusafirisha umeme; kujenga miundombinu ya usambazaji wa umeme mijini na vijijini. Aidha, katika kuhakikisha tunaweka mazingira bora ya uwekezaji na biashara, Serikali itaendelea kutekeleza: Programu ya Umilikishaji wa Ardhi; Programu ya Kupanga na Kupima Ardhi; mfumo wa ugawaji na usimamizi wa ardhi; Mradi wa Matumizi Bora ya Ardhi na kuendeleza ushirikiano wa kikanda na kimataifa hususan kwa njia ya diplomasia ya kiuchumi, hii itasaidia kuvutia uwekezaji na kupanua masoko.

**(d) Kuimarisha Utekelezaji wa Mpango na Miradi:** Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha kwa maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi kwa kutekeleza kikamilifu mapendekezo ya Mkakati wa ugharamiaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo; kuweka vigezo vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji; kuimarisha mifumo ya kitaasisi kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma; kujenga uwezo wa wataalam katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuimarisha mifumo ya uhifadhi na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi kulingana na thamani ya fedha (value for money).

Katika kufikia malengo ya Mpango, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi hususan ya ndani katika utekelezaji wa Mpango na Ujenzi wa Viwanda. Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo, kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni za ushiriki wa sekta binafsi kutenga maeneo mahsusi ya uwekezaji, kujenga miundombinu wezeshi itakayorahisisha uwekezaji, kuimarisha mifuko maalum ya kuchochea ushiriki wa sekta binafsi, kuimarisha Kituo cha Uwekezaji - TIC, na

kuweka utaratibu utakaoboresha upatikanaji mikopo ya muda mrefu kwa gharama nafuu.
Serikali itaendelea kuhamasisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na mashirika ya umma kuwekeza katika maeneo ya kipaumbele hususan viwanda. Mashirika ya Umma yanahusishwa katika uwekezaji wa miradi mikubwa ikiwemo ya miundombinu (bandari, barabara, mawasiliano, reli na ujenzi wa viwanja vya ndege), nishati, na maeneo mengine ya kimkakati (viwanda vya chuma, madini, makaa ya mawe) ambayo yameanishwa kwenye mpango huu kama maeneo ya kipaumbele.

**(e) Kuhamishia Makao Makuu ya Shughuli za Serikali Kuu Dodoma**: katika mwaka 2018/19 Serikali itaendelea na utekelezaji wa azma ya kuhamishia shughuli za Serikali makao makuu Dodoma. Katika utekelezaji wa azma hii, Serikali imejipanga kuijenga Dodoma kuwa jiji bora na la kisasa. Ili kufikia azma hiyo, Serikali inashirikiana na wadau ikiwemo sekta binafsi na mashirika ya kimataifa kujenga jiji la Dodoma. Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu upatikanaji wa maeneo ya kujenga ofisi na nyumba za viongozi wa Serikali kwa kuzingatia mahitaji na maboresho ya mpango wa ardhi katika jiji la Dodoma.

**64. Mheshimiwa Spika*,*** maelezo ya kina kuhusu Miradi ya Kipaumbele yapo katika Sura ya Nne ya Kitabu cha Mpango.

**Vihatarishi Vinavyoweza Kuathiri Utekelezaji wa Mpango**

**65. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaweza kukabiliwa na vihatarishi mbalimbali vya ndani na nje. Vihatarishi vya ndani ni pamoja na: Upungufu wa rasilimali fedha; Migogoro ya umiliki wa ardhi; Ushiriki wa sekta binafsi usiokidhi; Kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu; Uharibifu wa mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, vihatarishi vya nje vinajumuisha: mitikisiko ya kiuchumi na kisiasa ya kikanda na kimataifa; matukio asilia; na siasa za kimaeneo ikiwemo vita na migogoro.

**66.** **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango huu, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeweka tahadhari kwa kuchukua hatua zifuatazo:- kuongeza ukusanyaji wa mapato, kushirikiana na wadau kubuni vyanzo vipya na kuimarisha nidhamu katika usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali inaendelea kujadiliana na Sekta Binafsi katika kukuza uwekezaji, kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi katika uzalishaji ili kuongeza uzalishaji na kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

## Ugharamiaji wa Mpango 2018/19

### Sekta ya Umma

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19, Serikali imetenga Shilingi trilioni 12.0 ambapo Shilingi trilioni 9.8 ni fedha za ndani na Shilingi trilioni 2.1 ni fedha za nje. Kiasi hiki cha fedha ni sawa na asilimia 37 ya bajeti yote. Fedha za kugharamia miradi ya maendeleo zitatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo mapato yatokanayo na kodi, mapato yasiyo ya kodi, mikopo na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, kiasi kilichotengwa na Serikali hakihusishi uwekezaji wa moja kwa moja wa Sekta Binafsi na ubia kati ya sekta ya Umma na Binafsi.

### Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

**68.** **Mheshimiwa Spika,** ugharamiaji wa miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi utatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Ubia Na. 18 ya mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014. Vile vile, katika kuvutia uwekezaji, Serikali itaendelea kuboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini na kuimarisha mapato. Serikali itaendelea kuimarisha mfuko wa kuwezesha maandalizi ya miradi ya ubia kati ya sekta za umma na binafsi (*PPP Facilitation Fund*) ili kugharamia uandaaji wa upembuzi yakinifu kwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa.

### Uwekezaji wa Mashirika ya Umma

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutumia Mashirika ya Umma katika kugharamia miradi ya maendeleo.

Katika kuongeza mapato yatokanayo na Mashirika ya Umma Serikali itahakikisha inasimamia matakwa ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2015 na Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015. Hii itahakikisha kwamba taasisi na mashirika ya umma yote yenye wajibu wa kuwasilisha asilimia 15 ya mapato ghafi yanawasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha Bodi za wakurugenzi wa Mashirika ya Umma zinaimarishwa kwa kuteua wajumbe wa bodi wenye sifa stahiki kulingana na majukumu ya taasisi husika.

**Ugharamiaji wa Mpango kwa Kutumia Vyanzo Bunifu**

**70. Mheshimiwa Spika,** katika kutanzua changamoto za upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango, njia mbalimbali za upatikanaji wa rasilimali fedha zimeainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21 na Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango 2016/17 – 2020/21. Katika mwaka 2018/19 Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kufanyia kazi vyanzo hivyo vilivyopendekezwa ili utekelezaji wake uanze kutumika. Vyanzo hivyo ni pamoja na: kuimarisha utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi; hatifungani za Serikali za mitaa; uuzaji wa dhamana za serikali katika masoko ya kimataifa; uvuvi bahari kuu; na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi.

**71. Mheshimiwa Spika,** taarifa za kina kuhusu ugharamiaji wa miradi ya maendeleo zinapatika katika Sura ya Tano ya kitabu cha Mpango.

**Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa**

**72. Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 utazingatia Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mfumo huo unaainisha majukumu ya ufuatiliaji, uratibu, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati pamoja na upatikanaji wa taarifa za uhakika zitakazotumika kupima mafanikio.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19, Serikali itafanya tathmini ya muda wa kati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Tathmini hii itakuwa msingi wa kupima utekelezaji halisi wa Mpango, kuainisha changamoto za utekelezaji na hatimaye Serikali kuchukua hatua stahiki katika kutatua changamoto hizo. Matokeo ya tathmini hiyo yatatoa mapendekezo ya mabadiliko yanayohitajika ili kuhakikisha malengo ya Mpango yanafikiwa kama yalivyopangwa.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya Mpango kwa kushirikiana na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali zinazotekeleza miradi ya maendeleo. Katika kufanikisha utekelezaji wa mapendekezo yatakayotolewa katika ufuatiliaji na tathmini Serikali itaunda Kamati Maalum ya Ushauri (*steering committee*) na Sekretarieti ya Kamati hiyo itakuwa Wizara ya Fedha na Mipango.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19 Serikali itaendelea kutumia njia mbalimbali ili kuhakikisha kuwa wadau wanaelewa mipango ya Serikali na majukumu yao katika kuitekeleza. Wadau watapewa taarifa kupitia vyombo vya habari ikiwemo luninga, redio, magazeti na tovuti baada ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 kuidhinishwa na Bunge.

**76.** **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa yapo katika kitabu cha Mpango (Sura ya Sita).

## MAJUMUISHO NA HITIMISHO

### Majumuisho

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Azma ya Serikali ni kuchochea ujenzi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na Maendeleo ya Watu. Hata hivyo, kuna changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utekelezaji wa Mipango ya Serikali katika kufikia azma yake. Changamoto hizo ni pamoja na kutofikiwa kwa malengo ya mapato; Mikopo na misaada

kutopatikana kwa wakati; na ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Serikali inaendelea kufanya majadiliano na wadau wa maendeleo na pia imeandaa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo ili kuhakikisha misaada na mikopo inapatikana kama ilivyoahidiwa na kwa wakati. Vile vile, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kutekeleza mapendekezo ya vyanzo bunifu vilivyoanishwa katika makakati wa ugharamiaji; taarifa za kamati za Bunge na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** katika kujenga uchumi wa viwanda, msukumo ni kuanzisha na kufufua viwanda vitakavyotumia malighafi za hapa nchini, vitakavyozalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi, na vitakavyozalisha ajira mpya kwa Watanzania hususan vijana. Miongoni mwa viwanda hivyo ni pamoja na vile vitakavyotumia malighafi za kilimo, mifugo misitu na madini. Aidha, Serikali itaendelea kujizatiti katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuendelea kudhibiti mianya ya ukwepaji wa kodi na kuweka mkazo katika usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ili zitumike zaidi kugharamia miradi ya maendeleo na kuboresha upatikanaji wa huduma za kijamii kwa wananchi.

**Hitimisho**

**79.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb), Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara za Serikali na Taasisi zinazojitegemea kwa ushirikiano wao wakati wa maandalizi ya kutayarisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2018/19. Aidha, kipekee nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bw. Doto James kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku za Wizara.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya Hali ya uchumi 2017 na

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2018/19 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango www.mof.go.tz.

**81. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, wajadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19.

**82. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa wasilisho lako. Hoja imeungwa mkono. Katika hatua hii hoja imewasilishwa lakini mtakuja kuijadili kwa pamoja na Bajeti Kuu ya Serikali ambayo itawasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango baadaye leo saa 10.00 jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijachukua hatua inayofuata, nimwite Waziri wa Kilimo atoe maelezo mafupi tu kuhusiana na mwongozo nilioombwa na Mheshimiwa Boniface Getere, Mbunge wa Bunda kuhusiana na uuzaji wa pamba katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Hilo la Mheshimiwa Mbarouk, kwa upande wa Wizara ya Afya, Waziri wa Afya, atalitolea maelezo mafupi siku ya Jumatatu, *inshallah*. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Dkt. Tizeba.

**Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Mwongozo wa Mheshimiwa Boniface M. Getere, Mbunge wa Bunda juu ya Uuzaji wa Zao la Pamba**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi namna gani pamba inauzwa na kununuliwa katika msimu unaondelea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha ushirika na kwa kadri itakavyowezekana mazao matano makuu ya kipaumbele yauzwe kupitia mfumo wa ushirika. Kwa sasa wakulima wetu wanakosa sauti katika mambo mengi kwa sababu ya mazao

yao kuuzwa katika mifumo ambayo siyo rasmi. Kwa hiyo, tunajitahidi tuweke utaratibu ulio rasmi katika kuuza mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba inayouzwa sasa hivi tulitoa ushauri kwamba kwa kadri inavyowezekana, wakulima wanaoweza kufungua akaunti katika benki, wafungue ili wawe na usalama wa fedha zao, lakini pia tuweze kuwa na *record* nzuri ya kiasi gani mtu aliuza na kadhalika. Jambo hili baada ya kulitafakari na kwa kuangalia hali halisi ya uzalishaji wa pamba ilivyo katika vijiji, vipo vijiji vipo mbali sana na taasisi za fedha kama benki na hata fedha za mitandao kwa manaa ya M-pesa, Tigopesa na zenyewe wakati mwingine havipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuangalia aina ya wakulima waliohusika katika kulima pamba; wapo wengine ni watoto wadogo wa shule za msingi lakini wamelima, tukaona kurahisisha na kutotengeneza mazingira magumu kwa makundi haya mbalimbali kuuza pamba yao na kulipwa, basi twende na mifumo yote miwili kwamba wale ambao kwa namna yoyote hawawezi au itawatengenezea usumbufu mkubwa sana kama wakilazimika kufungua akaunti, basi walipwe fedha moja kwa moja katika vituo wanavyouzia pamba. Wale ambao wanaweza kufungua akaunti au wana simu za mkononi wakaweza kulipwa kwa namna hizi za simu za mkononi na kadhalika basi na wao walipwe kwa utaratibu huo wakati tukiendelea kushawishi matumizi ya benki katika malipo ya fedha za wakulima wanapouza mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusisitiza tena tangazo ambalo nimeshalitoa siyo mara moja wala mara mbili kwamba wananchi ambao kwa mazingira waliyopo au hata kwa kiasi tu cha zao wanalouza ni vigumu sana kumshawishi akafungue akaunti, basi waruhusiwe kulipwa moja kwa moja katika vituo wanapouza pamba. Rai yetu na tunaloendelea kusisitiza, wakulima wasikopwe. Mtu asinunue pamba halafu akakaa siku, tatu, nne au tano kabla ya kuwalipwa. Kwa jambo hili, tunaitaka Bodi ya

Pamba na Mamlaka zote za Mikoa na Wilaya zilisimamie kwa makini ili wafanyabishara wanaponunua pamba wawalipe wakulima siku hiyo hiyo kwa kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yako mazuri na ndiyo Serikali inatoa matumaini kwa Watanzania wanaohangaika na zao lao la pamba. Ingependeza maelezo kama haya yanatolewa mapema ili kuzuia hii mikanganyiko. Umeliweka vizuri sana, tunakushukuru, mlisimamie, ushirika huu tunataka ushamiri lakini siyo kwa kulazimishwa. Wenyewe wataona faida, Serikali iendelee kuujengea mazingira mazuri tu, lakini tusiwalazimishe wananchi wetu, wanahangaika na zao lao na mazao mengine na wanaelewa sana mazingira yao lakini tutafanikiwa tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, hoja hii mtaijadili pamoja na hoja ya Bajeti ya Serikali ambayo itawasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango baadaye mchana huu au alasiri. Kwa hiyo, sina matangazo hapa, narudia tu ule mwongozo kuhusiana na nilichoombwa Mheshimiwa Mbarouk utatolewa siku ya Jumatatu na Waziri wa Afya. Tujitahidi basi kati ya sasa na saa 10.00 tutakaoweza twende pale *Nyerere Square* tuunge mkono jitihada za Wizara ya Afya kwa suala la utoaji wa damu kusaidia akina mama wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 leo jioni.

*(Saa 5.53 Asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

## Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bila kupoteza muda, sasa nimkaribishe Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. Karibu sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. Bunge hili sasa liko tayari kukusikiliza kwa hotuba yako ya Bajeti na nikuhakikishie nchi nzima ya Tanzania wanakusikiliza. Karibu sana, una muda usiozidi saa mbili kamili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/2019. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vinne: Cha kwanza ni Makadirio ya Mapato; cha pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali; kitabu cha tatu, ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kitabu cha nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2018 ambayo ni sehemu ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni heshima kubwa na upendeleo wa hali ya juu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti ya tatu ya Serikali ya Awamu ya Tano. Hivyo, namshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu neema nyingi, utulivu na amani na kuniwezesha kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa wananchi wa Tanzania kwa mara ya tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kiongozi wetu shupavu, kiongozi anayeaminiwa na kutumainiwa na wananchi hasa wanyonge; kiongozi anayechukia na kupiga vita rushwa, ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma kwa vitendo; Rais anayejipambanua kwa kufanya maamuzi magumu ya kulinda rasilimali za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa kazi kubwa ambazo ameendelea kuzifanya tangu aliposhika hatamu za uongozi wa Taifa letu ambazo zimepelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa sana katika kipindi kifupi cha utawala wake wa miaka miwili na nusu tu. Napenda niyataje mambo kadhaa aliyodhubutu kutenda na kuiletea nchi yetu mafanikio makubwa. *(Makofi)*

(i) Rais wetu ametekeleza ndoto ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na uamuzi wa Chama Tawala wa mwaka 1972 wa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali Dodoma. *(Makofi/Vigelegele)*

(ii) Rais wetu amejenga ukuta wenye mzingo wa kilometa 24.5 kuzunguka machimbo ya madini ya tanzanite Mererani, Wilaya ya Simanjiro uliogharimu shilingi bilioni 5.42. Lengo likiwa ni kudhibiti uchimbaji wa uuzaji holela wa madini hayo yanayopatikana Tanzania pekee na kuliingizia Taifa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari mpaka Machi, 2018 Serikali imefanikiwa kukusanya mrabaha wa shilingi milioni 714.6 na kati ya kiasi hicho shilingi milioni 614 kilitokana na makusanyo kutoka kwa wachimbaji wadogo. Kiasi hicho kilichokusanywa kutoka kwa wachimbaji wadogo kinazidi jumla ya makusanyo ya mrabaha kwa miaka mitatu iliyopita. *(Makofi)*

(iii) Mheshimiwa Rais amezuia usafirishaji wa makontena 277 ya makinikia nje ya nchi yenye thamani kati ya shilingi bilioni 829.4 na shilingi bilioni 1,438.8 na kuagiza kutungwa kwa sheria mpya za mfano katika Bara la Afrika kuwezesha nchi zenye maliasili kunufaika na rasilimali hizo.

Sheria hizo ambazo zilipitishwa na Bunge lako Tukufu kwanza ni Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017; pili, ni Sheria ya Mapitio ya Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017; na tatu, ni Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2017. *(Makofi)*

(iv) Rais wetu ametoa Elimu ya Msingi bila ada ambapo kila mwezi Serikali inalipa shilingi bilioni 20.8. Kutokana na hatua hiyo, uandikishaji wa wanafunzi wa Darasa la Kwanza umeongezeka kutoka watoto 1,568,378 mwaka 2015 hadi watoto 2,078,379 mwaka 2018. Aidha, uandikishaji wa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza nao umeongezeka kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 562,695 mwaka 2018. *(Makofi)*

(v) Katika sekta ya afya amethubutu kuongeza bajeti zaidi ya mara nane kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kufikia shilingi bilioni 269 mwaka 2017/2018 kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016. *(Makofi)*

(vi) Mheshimiwa Rais amefanya maamuzi magumu ya kununua ndege mpya tatu aina ya *Bombardier Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja ambazo tayari ziko nchini na zinafanya safari za ndani. *(Makofi)*

Aidha, ndege kubwa nyingine tatu, moja aina ya *Boing 787-8 Dreamliner* zenye uwezo wa kubeba abiria 262 na ndege mbili aina ya *Bombardier C.300* zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja zitawasili nchini baadaye mwaka huu. Kadhalika Serikali imekamilisha taratibu za kupata ndege ya pili kubwa aina ya *Boing 787-8, Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262 na malipo ya awali yamekamilika. *(Makofi/Vigelegele)*

(vii) Mheshimiwa Rais, amedhibiti matumizi yasiyo ya lazima, ameondoa watumishi hewa 19,708 waliokuwa wanalipwa mshahara wa jumla ya shilingi bilioni 19.8 kwa mwezi na watumishi 14,404 wenye vyeti vya kughushi

waliokuwa wanalipwa mshahara wa jumla ya shilingi bilioni 15.5 kwa mwezi ambazo zote zimeokolewa. Aidha, nidhamu katika utumishi wa umma imeimarika na ameanzisha Mahakama ya Mafisadi ili kupambana na mafisadi wanaonyonya uchumi wa nchi. *(Makofi/Vigelegele)*

(viii) Mheshimiwa Rais ameanza ujenzi wa reli ya kati ya kisasa, awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kilometa 205 na awamu ya pili kutoka Morogoro mpaka Makutupora kilometa 422 tayari zinatekelezwa. Awamu zote mbili zitagharimu takribani dola za Marekani bilioni 3.14. *(Makofi/Vigelegele)*

(ix) Mheshimiwa Rais amefanya uamuzi wa kuanza ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme katika Mto Rufiji utakaozalisha *megawatt* 2100 utakapokamilika na umeanza kutekelezwa katika hatua za awali. *(Makofi/Vigelegele)*

(x) Mheshimiwa Rais ameimarisha ukusanyaji na mapato na kudhibiti ukwepaji kodi. Hatua ambazo zimewezesha Serikali kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 kwa mwezi hadi wastani wa shilingi trilioni 1.3 kwa mwezi. *(Makofi)*

(xi) Mheshimiwa Rais ameendeleza utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini *(REA)* ambapo ndani ya miaka miwili na nusu ya utawala wake jumla ya vijiji 557 vimeunganishwa na umeme. *(Makofi/Vigelegele)*

Aidha, amesitisha miradi ya wazalishaji binafsi wa umeme *(independed power producers)* ambayo ilikuwa inaigharimu Serikali fedha nyingi kwa maana ya *capacity charges*.

(xii) Vilevile bila yeye Mheshimiwa Rais mradi wa bomba la mradi wa mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Bandari ya Tanga usingepatikana na tayari ujenzi unaendelea. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, haya yote ni ushahidi usio na mashaka kwamba Tanzania chini ya Rais Magufuli imeshika kasi ya maendeleo. Hivyo, ni wajibu wa kila Mtanzania kuchangia katika jitihada hizi za Mheshimiwa Rais kujenga Tanzania mpya. Maeneo matatu ya msingi sana kwa kila mwananchi kuwajibika ni kwanza, ni uzalendo kwa nchi yetu; pili, ni kupiga vita wizi, ubadhirifu na ufisadi; na tatu, ni kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kumshukuru kwa moyo wangu wote kwa kuendelea kuniamini na kuniongoza katika kazi zangu za Uwaziri wa Fedha na Mipango. Hata pale nilipoelemewa na kazi na kulaumiwa kwamba Waziri huyu ni bahili mno katika kutoa fedha na baadhi wakinipaka tope la kiburi, alinitia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Rais, kwa nini alinitwika mimi kazi hii nzito kama msalaba wa zege tena bila matumaini ya kutokea mtu mfano wa Simon wa Kirene katika Biblia wa kuja kunipokea mzigo huu? Naye alinijibu kwamba Mungu atawatuma Malaika wake watakusaidia na akaongeza kwamba lazima watu wachache tuwe tayari kuumia kwa faida ya Watanzania wengi maskini. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kuwa majibu hayo yalinichoma na kunikumbusha sala ya wana O*pus Dei* katika mateso inayosema: "Mapenzi ya Mungu yenye haki na yanayopendeza sana yafanyike, yatimizwe, yasifiwe na kutukuzwa kuliko vitu vyote milele" Amina, Amina. Baada ya hapo, nilipata amani ya kuendelea katika utumishi huu. Ahsante sana Mheshimiwa Rais, najua unanisikiliza. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia Rais kuongoza Taifa letu kwa hekima na uadilifu. Kadhalika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza Zanzibar kwa busara, jambo ambalo limepelekea wananchi wa Zanzibar kuishi katika hali ya amani na utulivu mkubwa kwa kipindi cha miaka saba na nusu sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuwa *captain* hodari wa timu ya Serikali hapa Bungeni na kumsaidia Rais kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala CCM ya mwaka 2015 - 2020. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza Wakuu wa mihimili mingine ya dola nikianza na wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Kongwa kwa kuliongoza Bunge hili kwa umahiri. Pia nampongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa kazi nzuri ya kuongeza chombo cha utoaji haki. Napenda vilevile kumpongeza Mheshimiwa Balozi Mhandisi John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi, ambaye pia ni Mkuu wa Utumishi wa Umma na Katibu wa Baraza la Mawaziri kwa utumishi uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema pia niwapongeze Waheshimiwa wenzi wa Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa umuhimu wao wa kipekee. Naomba uniruhusu niwataje kwa majina yao: Mwalimu Janeth Magufuli, Bwana Ameir Hafidh Ameir, Mama Mwanamwema Shein, Mwalimu Mary Majaliwa, Dkt. Fatuma Ramadhan Mganga na Mama Marina Juma. Tunawapongeza na kuwashukuru kwa kuwawezesha Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa kutekeleza vizuri majukumu yao kwa utulivu, hamasa na tabasamu kutokana na mapenzi makubwa wanayopata nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze na kuwashukuru Wakuu wote wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,

Mkuu wa Majeshi, Inspekta Jenerali wa Polisi, Kamishna Jenerali wa Magereza, Kamishna Jenerali la Uhamiaji, Mkuu wa Usalama wa Taifa, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji. Mimi na Watanzania wenzangu tunawapongeza kwa dhati kabisa viongozi hawa pamoja na Makamanda, Askari na watumishi wote wa vyombo hivi nyeti kwa kuendelea kuilinda nchi yetu kwa ushupavu, kudumisha amani na usalama na kuwawezesha wananchi wote wa Tanzania kufanya shughuli za maendeleo kwa utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Adelaus Lubango Kilangi kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Namshukuru kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 na Muswada wa Sheria ya Matumizi wa Mwaka 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia fursa hii kutoa shukrani mahsusi kwa Kamati ya Kudumu ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abrahaman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijiji na Makamu wake Jitu Soni, Mbunge wa Babati Vijijini. Maoni na ushauri wao uliotolewa na Kamati ya Bajeti wakati wa kuchambua mapendekezo ya bajeti ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, ulikuwa wa kizalendo na wenye tija. Aidha, nawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa michango yao waliyoitoa kupitia Vikao vya Kamati za Kisekta katika kuboresha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 ili kuwapatia wananchi wa Tanzania huduma bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa mwaka 2017/2018, dhima ya bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa ni kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii. Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia

uhalisia wa nchi yetu ambao sisi wote tunaufahamu kwa maana ya changamoto kuu za kiuchumi na kijamii zinazotukabili, fursa tulizonazo, mafanikio hadi sasa na malengo yetu kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na malengo yetu lazima yaende pamoja na wajibu upande wa Serikali, sekta binafsi, wadau wengine na mwananchi mmoja mmoja kwa kuzipatia majibu changamoto tulizonazo na kuchangia ipasavyo katika jitihada za kulipeleka Taifa letu mbele. Tutafanya hivyo ikiwa kila mwananchi atafanya kazi na kutumia uwezo wake wote kwa ajili ya maendeleo yake na ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni muhimu pia tuendelee kujenga na kutumia ubia wa kimkakati *(harness strategic partnerships).* Ujumbe wangu kwa Watanzania kupitia bajeti hii ni kuwa lazima tuendelee kufanya chaguo gumu *(tough choices)* katika kuelekeza rasilimali kidogo tunazozikusanya. Ukweli ni kuwa mabadiliko ni magumu na mara nyingi yanapingwa. Hivyo ni lazima tuwe imara, tukusudie kufanikiwa na tutumie vizuri fursa na uwezo wa Watanzania, sekta binafsi na Serikali ili kufikia azma yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa bajeti wa mwaka 2017/2018. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 mapato kutoka vyanzo vyote yalifikia shilingi trilioni 21.89 sawa na asilimia 69 ya lengo la mwaka. Kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji kumetokana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukwepaji wa kodi, ugumu wa kutoza kodi wafanyabiashara waliopo katika sekta isiyo rasmi kwa vile hawana sehemu rasmi na za kudumu za kufanyia biashara na hawatunzi kumbukumbu; lakini pia mazingira yasiyo rafiki ya ulipaji wa kodi na mlolongo wa kodi na tozo, vipo viwango vikubwa vya kodi, urasimu katika taratibu za kulipa kodi na ugumu na gharama kubwa za kulipa kodi. Pia kuna matumizi hafifu ya mashine za kielektroniki za kutolea risiti, udhaifu katika usimamizi wa uvujaji wa rasilimali za nchi na mchango mdogo na utegemezi wa mashirika ya umma katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo ya ndani, Serikali ilikopa jumla ya shilingi trilioni 4.96 kutoka soko la ndani sawa na asilimia 80 ya zilizotarajiwa kukopwa. Aidha, Serikali ilikopa kutoka soko la nje shilingi bilioni 224 sawa na asilimia 14 ya lengo. Fedha hizi zimeelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati. Aidha, Mei, 2018 Serikali ilipokea mkopo wa kibiashara kiasi cha shilingi trilioni 1.15. Kwa upande wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa kutoka kwa washirika wa maendeleo ilikuwa shilingi trilioni 1.87 sawa na asilimia 47 ya makadirio ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa matumizi. Katika kipindi cha Julai, 2017 mpaka Aprili, 2018, Serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 21.68 sawa na asilimia 68.4 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 16.56 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha mishahara ya watumishi wa umma lakini pia kugharamia deni la Serikali. Hadi kufikia Aprili, 2018 Serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 5.12 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi trilioni 4.35 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 775.8 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti 2017/2018 hadi kufikia Aprili, 2018. Kwanza, shilingi bilioni 59 zimetolewa katika Halmashauri za Wilaya 110 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya na shilingi bilioni 24.1 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali za mikoa 24. Shilingi bilioni 125.7 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi; shilingi bilioni 156.1 imetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini; kiasi cha shilingi bilioni 404.9 kimetolewa kwa ajili ya miradi ya nishati vijijini, umeme wa joto ardhi, uzalishaji wa umeme katika vyanzo mbalimbali na usambazaji wa gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya kutoa elimu msingi bila ada na kugharamia mikopo ya wanafunzi

wa elimu ya juu, Serikali imetoa shilingi bilioni 618. Serikali imeendelea kutekeleza ujenzi wa miundombinu ili kupanua fursa za uchumi, kilimo, biashara na viwanda ikiwemo barabara zinazounganisha mikoa na nchi jirani na barabara zinazopunguza msongamano katika majiji, barabara za vijijini, reli, viwanja vya ndege na bandari. Katika eneo hili kiasi cha shilingi trilioni 1.87 kimetolewa. Pia Serikali imeendelea kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi wa umma, wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ambapo kiasi cha shilingi trilioni 1.17 kimelipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa deni la Serikali; katika kudhibiti kuongezeka kwa gharama za mikopo, Serikali ilijikita zaidi kukopa kwenye mikopo yenye masharti ya kati *(Semi Concessional Loans)* hasa mikopo inayowezesha uagizaji wa vifaa na mitambo kutoka nchi inayokopesha *(Export Credit Agency)* na pale ilipolazimu, mikopo ya masharti ya kibiashara ilikopwa kwa uangalifu mkubwa ikiwemo kuhakikisha kwamba mikopo hiyo inatumika kwenye maeneo ambayo yanachochea ukuaji wa uchumi. Hadi Aprili, 2018, deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 49.65 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 13.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 43.79 Aprili, 2017. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 14.05 na deni la nje shilingi trilioni 35.6 sawa na asilimia 71.7 ya deni lote. Ongezeko la deni hilo limetokana na mikopo ya zamani na inayoendelea kupokelewa na malimbikizo ya riba ya deni la nje.

Mheshimiwa Spika, mikopo nafuu kutoka Mashirika ya Fedha za Kimataifa imeendelea kuwa chanzo kikubwa cha mikopo kutoka nje ambayo imechangia asilimia 59.6 ya deni lote la nje. Mikopo yenye masharti ya kibiashara imechangia asilimia 25.5, wakati mikopo kutoka nchi wahisani imechangia asilimia 11.9. Mikopo hii imetumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, deni la Serikali limekuwa likiongezeka. Hata hivyo, deni hili limeendelea kuwa himilivu. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba, 2017

inaonesha kuwa deni ni himilivu. Uwiano wa deni kwa thamani ya sasa *(present value),* kwa pato la Taifa ni asilimia 34.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 56. Thamani ya deni la nje kwa mauzo ya nje ilikuwa ni asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150. Thamani ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 117.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250. Ulipaji wa deni la nje kwa mapato yatokanayo na mauzo nje, asilimia 9.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ulifikia asilimia 13.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza tena kwamba hakuna dhambi kwa nchi kukopa kwa busara *(prudently).* Mambo ya muhimu ya kujiridhisha nayo ni kuwa mikopo hiyo inatumika kujenga uwezo zaidi wa kuzalisha mali *(productive capacity)* na kurejesha mikopo hiyo kwa kuzingatia uwezo wa uchumi kuhimili mzigo wa madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya malimbikizo ya madai, Serikali imeandaa mkakati wa kulipa madeni na kuzuia ulimbikizaji wa madeni yakiwemo yale ya watumishi, wazabuni na watoa huduma pamoja na madai ya wakandarasi. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kulipia madai yaliyohakikiwa. Katika ulipaji wa madeni, kipaumbele kitatolewa kwa madeni yanayogusa watoa huduma wengi na yale yanayoongezeka kutokana na riba.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba hakuna madeni mapya yanayozalishwa, kila Afisa Masuuli atapaswa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Mikataba yote ya ujenzi wa miundombinu itazingatia viwango vya bajeti vilivyowekwa katika fungu. Fungu husika lisiingie mikataba nje ya viwango hivyo bila kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

(ii) Kutoa kipaumbele kwa ukamilishaji wa miradi inayoendelea kabla ya kuanzisha miradi mipya. *(Makofi)*

(iii) Maafisa Masuuli wasiingie makubaliano ya kupatiwa huduma au bidhaa bila ya kuwa na fedha au kibali cha maandishi kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na miadi yoyote lazima iingizwe kwenye mfumo wa *Integrated Financial Management System*. *(Makofi)*

(iv) Madai ya watoa huduma wote na wakandarasi lazima yafanyike baada ya kupata hati ya ununuzi *(LPO)* kutoka kwenye mfumo wa *IFMS* pamoja na kuwepo kwa ridhaa ya matumizi kwa vifungu husika vya matumizi. Hivyo, Serikali inasisitiza kwamba *LPO* zilizotoka kwenye mfumo wa malipo wa Serikali *(IFMS)* ndiyo zitumike kama msingi wa malipo kwa watoa huduma.

(v) Maafisa Masuuli wazingatie matumizi ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 na Waraka wa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, sera za bajeti kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019, nikianza na shabaha za uchumi jumla na za bajeti. Shabaha za uchumi jumla, katika kipindi cha mwaka ujao zitakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 7.1 mwaka 2017. *(Makofi)*

(ii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja. *(Makofi)*

(iii) Mapato ya ndani yafikie asilimia 15.8 ya pato la Taifa mwaka 2018/2019 kutoka matarajio ya asilimia 15.3 mwaka 2017/2018 na uwiano halisi wa asilimia 15.6 mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

(iv) Mapato ya kodi yafikie asilimia 13.6 ya pato la Taifa 2018/2019 kutoka matarajio ya asilimia 13 mwaka 2017/2018 na uwiano halisi wa asilimia 13.3 mwaka 2016/2017.

(v) Matumizi ya Serikali yatafika asilimia 24.5 ya pato la Taifa 2018/2019 kutoka matarajio ya asilimia 23 mwaka 2017/2018 na matumizi halisi asilimia 22.2 mwaka 2016/2017 na nakisi ya bajeti kufikia asilimia 3.2 ya pato la Taifa mwaka 2018/2019 kutoka matarajio ya asilimia 2.1 mwaka 2017/2018 na uwiano halisi wa asilimia 1.5 mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera na mikakati ya kuongeza mapato. Ili kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, Sera ya Mapato kwa mwaka ujao wa fedha zinalenga katika kuongeza wigo wa kodi, kuimarisha usimamizi wa vyanzo vilivyopo hasa kwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki na hatua nyingine za kiutawala.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza wigo wa kodi, yapo maeneo makuu mawili yatakayozingatiwa na Serikali ambayo ni kurasimisha sekta isiyo rasmi na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kupata vyanzo vipya vya mapato vitokanavyo na uwekezaji huu. Zipo hatua za urasimishaji zilizoanza kufanyika, mfano uthamanishaji wa majengo na upimaji wa viwanja zoezi linaendelea nchi nzima. Serikali itaongeza kasi ya urasimishaji ikiwa ni pamoja na kuwepo mbinu bunifu, rafiki, shirikishi na za kimkakati.

Mheshimiwa Spika, mazingira bora ndiyo msingi mkuu wa kuvutia biashara na uwekezaji ikiwemo kuboresha miundombinu msingi, vivutio vya kikodi, sera zisizobadilika *(policy consistency and creditability),* upatikanaji wa ardhi na taratibu za kisheria na usimamizi. Pale mazingira yanapokuwa mazuri uwekezaji, uzalishaji, ajira na miamala ya kibiashara inaongezeka na hivyo kupelekea kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi ambao tumefanya Serikalini mwaka 2017/2018 ulibaini changamoto kuhusiana na mazingira ya biashara ya uwekezaji kama ifuatavyo:-

(i) Migongano ya sheria, kanuni na taratibu zinazotumiwa na mamlaka mbalimbali.

(ii) Gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara kutokana na wingi wa kodi, ada na tozo zinazoambatana na taratibu ngumu na nyingi zenye urasimu usio na tija na hivyo kutoa mianya na mazingira ya rushwa. *(Makofi)*

(iii) Mwingiliano wa majukumu na wingi wa mamlaka za udhibiti katika kuidhinisha na kutoa hati, vibali na vyeti vyenye shughuli za uwekezaji na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Serikali imeandaa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara *(Blue Print for Regulatory Reforms to Improve Business Environment for Tanzania).* Miongoni mwa mapendekezo ya Serikali katika mpango huo ambayo yatatekelezwa kwa nguvu zaidi kuanzia mwaka ujao wa fedha ni kurahisisha taratibu za kulipa kodi, tozo na ada mbalimbali na kupunguza muda na mlolongo mrefu wa kusajiri makampuni na biashara. Serikali ya Awamu ya Tano inaamini kuwa maendeleo endelevu yatapatikana kwa haraka zaidi katika mazingira yenye ushirikiano wa kweli na wa dhati kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyopo, Serikali itaendelea na zoezi la uunganishaji wa Wizara, Idara, Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato *(Government Electronic Payment Getway)* ili kuboresha ukusanyaji na udhibiti wa upotevu wa mapato ya Serikali. Mfumo huu ulianzishwa 2017 na kupitishwa

na Bunge kupitia Marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Umma, Sura 348 ambayo iliziagiza Taasisi zote za Serikali kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa *GEPG.* Hadi Mei, 2018, jumla ya taasisi 234 zinazokusanya maduhuli zikijumuisha Halmashauri zote 185 zimeunganishwa kwenye mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuagiza Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali zilizobaki zihakikishe kwamba zimeunganishwa na kuanza kutumia mfumo huo wa *GEPG* kabla ya Juni, 2019. Mbali na mfumo huo, nawakumbusha Maafisa Masuuli wote kuhakikishwa kuwa ukusanyaji wa maduhuli unafanyika kwa kutumia mashine za kielektroniki *(EFDS)* pamoja na benki na siyo risiti za kuandikwa kwa mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua nyingine za kiutawala za kuongeza mapato ya Serikali, naelekeza yafuatayo:-

(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ichukue hatua za makusudi za kuboresha mahusiano kati yake na walipa kodi kwa lengo la kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa walipa kodi kuwa *TRA* inatumia nguvu na vitisho kudai kodi. *(Makofi)*

(ii) Ofisi ya Msajili wa Hazina iimarishe usimamizi na ukaguzi kwenye kampuni ambazo Serikali ina hisa ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata gawio stahiki katika uwekezaji wake. *(Makofi)*

(iii) Naagiza kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zijiekeleze kwenye miradi itakayochochea upatikanaji wa mapato katika mamlaka hizo, hususan viwanda, masoko na machinjio ya kisasa, stendi za mabasi, stendi za maegesho ya maroli kwenye mipaka ya nchi jirani na maghara ya kuhifadhi nafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera za Matumizi. Katika mwaka ujao wa fedha Sera zitajumuisha:-

(i) Kudhibiti nakisi ya bajeti isizidi asilimia 3.2 ya pato la Taifa na kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele na yenye tija ili kuchochea ukuaji wa kilimo na viwanda;

(ii) Kupanua fursa za ajira, kujenga na kuboresha miundombinu ya uchumi na kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za jamii;

(iii) Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuendelea kupunguza matumizi yasiyo ya lazima;

(iv) Kudhibiti ulimbikizaji wa madai.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele katika bajeti hii yatakuwa yafuatayo:-

(i) Kilimo. Fedha zitaelekezwa zaidi kuboresha miundombinu ya umwagiliaji; maghala na masoko; kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo; kupanua huduma za ugani; kuboresha mfumo wa utafiti na utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wananchi; na uendelezaji wa sekta ndogo ya uvuvi na mifugo. Mkazo umewekwa katika sekta hii kwa kuzingatia kuwa ni sekta inayotegemewa na wananchi wengi na ndiyo inayotupatia malighafi kwa ajili ya viwanda, kutuhakikishia usalama wa chakula na kuongezeka kwa kipato kwa wananchi. *(Makofi)*

(ii) Viwanda. Katika kuchochea ukuaji wa viwanda nchini, Serikali itaekeleza nguvu zake katika kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi hususan viwanda vya nguo, ngozi na nyama, samaki, mafuta ya kula, madawa na vifaa tiba, vyakula vya binadamu na mifugo na katika sekta ya madini. Aidha, uendelezaji wa viwanda na kilimo utapaswa kuzingatia uendelevu wa mazingira. *(Makofi)*

(iii) Huduma za jamii hususani maji. Hili ni eneo muhimu na kazi itakuwa kuongeza upatikanaji na usambazaji wa maji safi hasa vijijini na kuondosha maji taka, uchimbaji wa visima katika maeneo kame nchini na ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati. *(Makofi)*

Kwa upande wa elimu Serikali itaendelea kugharamia elimu msingi bila ada, kuongeza idadi ya wataalam katika fani adimu kwenye maeneo ya madini, mafuta na gesi, madaktari bingwa hususani moyo na figo pamoja na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Kwa upande wa afya, rasilimali fedha zitaelekezwa kuongeza usambazaji wa dawa, vifaatiba, vitendanishi na uboreshaji wa huduma katika vituo vya afya, aahanati na hospital za rufaa. Vilevile katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaelekeza fedha zaidi za *LGCD* kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa na halmashauri hususani miradi ya elimu na afya.

Aidha, Serikali itaweka msukumo kuimarisha upatikanaji wa lishe bora kwa mama na mtoto hususani kwa siku 1,000 za mtoto tangu kutungwa kwa mimba, ili kuondokana na changamoto za kuwa na watoto wenye udumavu na hivyo kukua vema kimwili na kiakili. Aidha, mahitaji ya makundi maalum katika jamii yetu, wanawake, vijana, watoto, watu wenye ulemavu na wazee yataendelea kuangaliwa kipekee. *(Makofi)*

(iv) Kujenga na kukarabati miundombinu wezeshi hususani kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali; kuendelea na ujenzi mpya wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa; ujenzi wa barabara za kuunganisha mikoa na zile za vijijini; na kuimarisha usafiri wa anga na majini.

(v) Maeneo mengine ya kipaumbele ni kurahisisha umiliki wa ardhi, kuimarisha huduma za mawasiliano, kifedha na utalii na kuimarisha ulinzi, usalama, utawala bora na utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, hatua za mapato na maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali. Napenda kuwasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali na pia taratibu za ukusanyaji na usimamiaji wa mapato ya Serikali. Marekebisho haya yanalenga pamoja na mambo mengine kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, hususani katika sekta ya kilimo, viwanda, utalii, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, marekebisho haya yamezingatia dhamira ya Serikali ya kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wenye kutabirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko ya Thamani, Sura 148. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya madawa ya binadamu vitakavyotengenezwa mahsusi kwa ajili ya viwanda vinavyozalisha dawa hapa nchini. Aidha, vifungashio hivyo vitakuwa na machapisho ya majina ya viwanda husika vya utengenezaji madawa ili kuhakikisha kwamba vinatumiwa na viwanda hivyo na siyo vinginevyo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuvilinda viwanda vinavyotengeneza madawa hapa nchini ili viweze kumudu ushindani na kuongeza uzalishaji.*(Makofi)*

(ii) Napendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye virutubisho vinavyotumika kutengeneza vyakula vya mifugo (*animal and poultry feeds additives*) vinavyotengezwa kutoka nje. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wafugaji na kuhamasisha ufugaji bora ili kuongeza mchango wa sekta hii katika uchumi. *(Makofi)*

(iii) Napendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 6(2)(a) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na

masuala ya fedha, kutoa msamaha wa kodi kwa miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa mikopo ya kibiashara. *(Makofi)*

Hivi sasa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inakataza kusamehe kodi kwenye mikopo ya kibiashara hali ambayo imesababisha kukwama kwa utekelezaji wa miradi muhimu ya Serikali kama vile miradi ya maji, barabara na kadhalika. Hivyo, marekebisho yanayopendekezwa, yatawezesha utekelezaji wa miradi ya Serikali kwa wakati uliopangwa. *(Makofi/Vigelegele)*

(iv) Napendekeza kufanya marebisho kwenye kifungu cha 6(2)(a) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, ili kumpa Waziri wa Fedha mamlaka ya kusamehe kodi hiyo pale ambapo kuna mkataba uliosainiwa baina ya Serikali ya Tanzania na taasisi ya fedha au Benki ambayo ni mwakilishi wa Serikali nyingine aliyepewa dhamana na Serikali hiyo kuingia mkataba na kusimamia utekelezaji wa miradi husika. *(Makofi)*

Hivi sasa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inampa mamlaka Waziri huyo kusamehe kodi pale ambapo kuna mkataba baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya nchi nyingine unaotoa msamaha wa kodi. Hivyo, miradi mingi inayohusika na mikataba ya misaada au mikopo kupitia mabenki na taasisi za fedha imekwama utekelezaji wake. Kwa msingi huo, marekebisho hayo yanalenga katika kuondoa ukwamishaji na ucheleshaji wa utekelezaji wa miradi mingi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za washirika wa maendeleo kupitia mikataba inayosainiwa na Serikali yetu na Benki au taasisi za fedha za Serikali za nchi nyingine. *(Makofi)*

(v) Napendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike.... *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, narudia...

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM, CCM.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

**MBUNGE FULANI:** Rudia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge hawajakusikia vizuri, weka vizuri kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike *(sanitary pads), HS Code 9619.00.10.* *(Makofi/Vigelegele)*

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM, CCM.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hii muhimu kwa bei nafuu kwa ajili ya kulinda afya ya mama na mtoto wa kike, hasa watoto waliopo shuleni na vijijini. Ni matarajio ya Serikali kuwa wazalishaji na wauzaji wa taulo za kike wataziuza bei nafuu baada ya kusamehewa kodi hii. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 219.1

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ili kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni (*Corporate Income Tax)* kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa miaka mitano. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, narudia, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ili kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni *(Corporate Income Tax)* kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa miaka

mitano kuanzia mwaka 2018/2019 mpaka mwaka 2022/2023. Hii itahusu wawekezaji wapya wa viwanda vya madawa ya binadamu na viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaingia mkataba wa makubaliano *(performance agreement)* na kila mwekezaji ambao utaainisha wajibu wa kila upande. Lengo la hatua hii ni kuongeza uwekezaji katika sekta ya madawa ya binadamu na usindikaji wa ngozi, ambao kwa sasa haufanyiki nchini na pia kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Aidha, hatua hii itapunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza dawa hizo kutoka nje na kuhamasisha uzalishaji wa madawa mengi hapa nchini. *(Makofi/ Vigelegele)*

(ii) Napendekeza kufuta kifungu cha 10A cha Sheria ya Kodi ya Mapato, kinachomtakaza Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kutoa msamaha wa kodi kwenye miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ya kibiashara *(non-concessional loans).* Lengo la hatua hii ni kumpa mamlaka Waziri huyo kutoa msamaha wa kodi ya mapato kwa miradi hiyo ambayo imekuwa na changamoto katika utekelezaji wakati Serikali inapopata mikopo ya aina hiyo. *(Makofi)*

(iii) Kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato ili kutoa msamaha wa kodi ya Zuio inayotozwa kwenye riba kwa mikopo inayotolewa kwa Serikali na benki, taasisi za fedha na wahisani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za miradi ya kodi ya mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 220.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147. Kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kifungu 124 (2), marekebisho ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa *(specific duty rate)* zisizo za petroli, yanaweka kufanyika kila

mwaka ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Hata hivyo, ili kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda, napendekeza kutofanya mabadiliko ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa zisizo za petroli zinazozalishwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia, napendekeza kutofanya mabadiliko ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa zisizo za petroli zinazozalishwa hapa nchini na kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa zisizo za petrol zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo:-

(i) Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji baridi utaendelea kutozwa kwa kiwango cha Sh.61 kwa lita. *(Makofi)*

(ii) Ushuru wa Bidhaa kwenye maji ya kunywa yaliyosindikwa kwa chupa yaliyoagizwa kutoka nje utaongezeka kutoka Sh.61 kwa lita hadi Sh.64.05 kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.3.05 kwa lita. Aidha, ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa hapa nchini utaendelea kutozwa kwa kiwango cha sasa cha Sh.58 kwa lita. *(Makofi/ Vigelegele)*

(iii) Ushuru wa Bidhaa kwenye maji ya matunda yaani *juice* iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini *(local juices)* hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha Sh.9 kwa lita. *(Makofi)*

(iv) Ushuru wa Bidhaa kwenye maji ya matunda yaani *juice* iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini (*imported juices)* utaongezeka kutoka Sh.221 kwa lita hadi Sh.232 kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.11 kwa lita. *(Makofi)*

(v) Ushuru wa Bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa *(beer from local unmalted cereals)*

hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha Sh.450 kwa lita. *(Makofi)*

(vi) Ushuru wa Bidhaa kwenye bia zinazoagizwa kutoka nje ya nchi utaongezeka kutoka Sh.765 kwa lita hadi Sh.803.25 kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.38.25 kwa lita. *(Makofi)*

(vii) Ushuru wa Bidhaa kwenye bia zisizo za kilevi ikijumuisha vinywaji vya kuongeza nguvu vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi utaongezeka kutoka Sh.561 kwa lita hadi Sh.589.05 kwa lita. Aidha, ushuru wa bidhaa kwenye bia zisizo za kilevi, ikijumuisha vinywaji vya kuongeza nguvu vinavyozalishwa hapa nchini, utaendelea kutozwa kwa viwango vya sasa vya Sh.561 kwa lita. *(Makofi)*

(viii) Kuanzisha Ushuru wa Bidhaa wa Sh.200 kwa lita kwenye mvinyo unatengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda kama ndizi, rozela, choya, nyanya na kadhalika yanayozalishwa hapa nchini tofauti na zabibu kwa kiwango kinachozidi asilimia 75.

(ix) Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 hautaongezeka na utandelea kutozwa kwa kiwango cha Sh.200 kwa lita. *(Makofi)*

(x) Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 utaongezeka kutoka Sh.2,349 kwa lita hadi Sh.2,466 kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.117 kwa lita. *(Makofi)*

(xi) Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyoagizwa kutoka nje utaongezeka kutoka Sh.3,481 kwa lita hadi Sh.3,655.05 kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.174.05 kwa lita. Aidha, ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyozalishwa nchini hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha Sh.3,315 kwa lita.

(xii) Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 hautaongezeka na utandelea kutozwa kwa kiwango cha Sh.12,447 kwa kila sigara 1,000.

(xiii) Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zenye kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha sasa cha Sh.29,429 kwa kila sigara 1,000.

(xiv) Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zenye sifa tofauti na nilizozitaja utaongezeka kutoka Sh.53,235 hadi Sh.55,896.75 kwa kila sigara 1,000 ikiwa ni ongezeko la Sh.2,661.75 kwa kila sigara 1,000.

(xv) Ushuru wa Bidhaa kwenye tumbaku ambayo ipo tayari kutengeneza sigara *(cup filler)* inayotengenezwa kutoka nje utaongezeka kutoka Sh.26,888 hadi Sh.28,232.4 kwa kilo ikiwa ni ongezeko la Sh.1,344.4 kwa kilo.

(xvi) Ushuru wa Bidhaa ya *cigar* utabaki kuwa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuanzisha mfumo mpya wa stempu za kodi za kielektroniki utakaoanza kutumia tarehe 1 Septemba, 2018. Mfumo mpya wa Stempu za Kodi za Kielektroniki utaiwezesha Serikali kutumia teknolojia ya kisasa kupata taarifa sahihi za uzalishaji viwandani na kwa wakati *(real time)* zitakazotumika kupanga mipango ya maendeleo ya Taifa. Pia mfumo huu mpya utaiwezesha Serikali kudhibiti uvujaji wa mapato na kutambua mapema kiasi cha Kodi ya Ushuru wa Bidhaa, Kodi ya Mapato na ile ya Ongezeko la Thamani itakayolipwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki utadhibiti tatizo la uwepo wa stempu za karatasi za kugushi, ambalo linachangia uwepo wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na zinazoweza kuathiri afya

ya binadamu. Mfumo huu mpya unatumika katika nchi nyingine ikiwa ni pamoja na Kenya, Morocco, Uturuki, Malyasia na Switzerland na umekuwa na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, hatua za Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake, zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 119.456.6.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kifungu cha 37A kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kuzitaka Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya fedha wanazokusanya kutoka kwenye vyanzo vyao vya mapato kwa ajili ya kuwawezesha makundi ya vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, asilimia 50 ya fedha hizo zitatengwa kwa ajili ya vikundi vya vijana na asilimia 50 kwa ajili ya vikundi vya wanawake. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ataandaa kanuni ambazo zitaweka utaratibu wa kusimamia utoaji wa fedha hizo kwa vikundi vya vijana na wanawake vilivyosajiliwa. Pia fedha zitatolewa kwa kuwakopesha bila kutoza riba yoyote. *(Makofi/Vigelegele)*

(ii) Kurekebisha Kifungu cha 16(6) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 ambacho kinatoa mwanya kwa taasisi au makampuni yanayolipa Ushuru wa Huduma kutolipa Ushuru wa Mazao. Mfano, makampuni mengi yanayochakata zao la mkonge ili kuzalisha nyuzi za katani yanamiliki pia mashamba ya mkonge, hivyo, si busara kuwalipisha Ushuru wa Mazao na Ushuru wa Huduma. *(Makofi)*

Mheshiiwa Spika, hata hivyo, yapo makampuni yenye mashamba ya mkonge ambayo hayachakati mkonge, haya yanapaswa kulipa Ushuru wa Mazao badala ya Ushuru wa

Huduma. Napendekeza kiongezwe kifungu cha 16(7) kwenye sheria hiyo kuyataka makampuni yanayozalisha mazao na hayachakati kwa ajili ya kuyaongezea thamani yawajibike kulipa Ushuru wa Mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438. Napendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 ili kuanzisha utaratibu maalum wa kusamehe kodi *(Tax Amnesty)* ambao unalenga kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu *(interests and penalties)* kwa kiwango cha asilimia 100. Msamaha huu utatolewa kwa kipindi cha miezi sita kinachoanzia tarehe 1 Julai, 2018 mpaka tarehe 31 Desemba, 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kufanya hivyo, Serikali inatarajia kukusanya malimbikizo ya madeni ya nyuma ya kodi *(principal)* pamoja na kuinua kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari kwa zaidi ya asilimia 10. Hatua hiyo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, Sheria ya Fedha ya Umma, Sura 348 na Sheria ya Benki Kuu Sura 197. Napendekeza kurekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Sheria ya Benki Kuu, Sura 197 ili kuanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina *(Treasury Single Account)* ambapo akaunti hii itatumika kupokea fedha zote za Serikali na kufanya malipo yote ya Serikali. Msingi wa kuanzishwa kwa akaunti hii ni kutekeleza makubaliano ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyozitaka nchi wanachama kuanzisha akaunti jumuifu ili kuimarisha usimamizi wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa akaunti hii pamoja na mambo mengine, utarahisisha usimamizi wa fedha za Serikali kwa kupunguza idadi ya akaunti kwenye benki za biashara na Benki Kuu; kupunguza gharama za kibenki zinazolipwa hivi sasa na Serikali kufuatia huduma zinazotolewa kwa

Serikali na benki za biashara; kupunguza nakisi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo akaunti maalum zitajumuishwa kwenye ukokotoaji wa bakaa katika Mfuko Mkuu wa Serikali tofauti na utaratibu wa hivi sasa ambapo akaunti hizi hazijumuishwi katika ukokotoaji huu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha maandalizi ya bajeti kilichofanyika tarehe 4 Mei, 2018, Mjini Arusha, Tanzania kilipendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha *(EAC - Common External Tariff)* na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Customs Management Act, 2004)* kwa mwaka 2018/2019. Mapendekezo haya yanalenga kwa kiwango kikubwa katika kuchochea maendeleo ya viwanda ili kukuza ajira na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuendelea kutoa unafuu kwa viwanda vya wazalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano na kuimarisha utulivu wa bei kwa bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia ngano hiyo.

Aidha, hatua hii inazingatia kwamba bado kiwango cha uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu ni kidogo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo hautoshelezi mahitaji. Ili kudhibiti uagizaji wa bidhaa hii, utaratibu wa *Duty Remission* utatumika ambapo viwanda vinavyotumia ngano ya aina hii katika uzalishaji ndivyo vitahusika na kutumia kiwango hicho cha msamaha wa ushuru wa forodha.

(ii) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali

*(Electronic Fiscal Devices)* zinazotambuliwa kwa *HS Code* 8470.50.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inatarajiwa kuendelea kutoa unafuu na kuhamasisha wafanyabiashara na walipa kodi kutumia mashine hizo katika kufanya mauzo na kuongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa kodi.

(iii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 15 badala ya asilimia 25 kwenye karatasi, utaratibu wa *Duty Remission* utatumika ambapo wazalishaji wa karatasi hizo watatumia karatasi kwa kutengeneza madaftari na vitabu ambao ndiyo watakaofaidika. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wazalishaji hawa. Ni matarajio ya Serikali kwamba wazalishaji watauza bidhaa hizi kwa bei nafuu na hivyo kuwezesha watumiaji, hususan wanafunzi, kuzipata kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

(iv) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazoingizwa kutoka nje kwa ajili ya utengenezaji wa *gypsum board* zinazotambulika katika *HS Code* 4805.92.00.

(v) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 100 kwenye sukari ya matumizi ya kawaida *(consumption sugar)* inayoagizwa kutoa nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo *(gap sugar)* la uzalishaji wa hapa nchini. Hivi sasa sukari hiyo inatozwa ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 100. *(Makofi)*

(vi) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye *gypsum powder* kwa mwaka mmoja. Marekebisho haya yanalenga katika kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo hapa nchini na kuhamasisha wawekezaji watumie *gypsum* inayopatikana hapa nchini kuzalisha *gypsum powder.* Aidha, hatua hii inatarajiwa kuongeza ajira na mapato ya Serikali. *(Makofi)*

(vii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa ijulikanayo kama *Self-adhesive label* ambayo hutumika kama alama ya kutambulisha aina ya bidhaa kwa watengenezaji

wa dawa za meno. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji kwenye viwanda vya dawa za meno kwa kuwa *Self-adhesive labels* hazizalishwi hapa nchini. *(Makofi)*

(viii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwenye bidhaa ijulikanayo kama *Printed Alluminium Barrier Laminates (ABL)* kwa mwaka mmoja. Aidha, utaratibu wa *Duty Remission* utatumika ambapo hatua hii itawahusu wenye viwanda vinavyoagiza bidhaa hiyo kwa matumizi ya viwandani. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama ya uzalishaji kwa viwanda vya dawa za meno. Aidha, ina lengo la kuvilinda viwanda hivi kutokana na ushindani na ajira.

(ix) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ghafi ya kula ya mawese yanayotambulika kwa *HS Code* 1511.10.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta na mafuta ya kula hapa nchini kwa kuzingatia kuwa nchi yetu ina fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo.

Aidha, lengo ni kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mafuta ghafi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Pia inatarajiwa kwamba uzalishaji wa mbegu utaongezeka na kuongeza ajira viwandani na mashambani pamoja na kuongeza kipato cha wakulima. *(Makofi/Vigelegele)*

(x) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 0 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ghafi ya kula, mfano alizeti, mawese, soya, mzaituni, nazi, karanga, mahindi na kadhalika. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa mbegu na mafuta ya kula hapa nchini kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini. Aidha, inatarajiwa kwamba hatua hii italinda viwanda na ajira katika sekta ndogo ya mafuta ya kula na kuongeza mapato ya Serikali na ya wakulima. *(Makofi)*

(xi) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yanayochakatwa kwa kiwango cha kati na cha mwisho *(semi refined, refined and double refined oil)* mfano, alizeti, mawese, soya, mzaituni, nazi, karanga, mahindi na kadhalika. Ongezeko hilo la Ushuru wa Forodha linatarajiwa kulinda uzalishaji wa mafuta ya kula na kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta zinazozalishwa nchini badala ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Aidha, hatua hii inatarajiwa kupunguza fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi.

(xii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au Dola za Kimarekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo *(metric tonne)* kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za chuma za misumari *(corrugated nails staples other than those of heading 83.05).* Hatua ya kuweka kiwango hiki cha Ushuru wa Forodha inalenga katika kulinda viwanda vya bidhaa hizo hapa nchini kutokana na uingizaji wa bidhaa kama hizo kutoka nje.

(xiii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au Dola za Kimarekani 1.35 kwa kilo moja ya vibiriti vinavyotambuliwa kwenye *HS Code* 3605.00.0 kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Hatua hii inazingatia kuwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina uwezo wa kuzalisha vibiriti na kutosheleza mahitaji katika soko, hivyo kuwepo na umuhimu wa kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo.

(xiv) Nchi za Jumuiya zimekubaliana kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwenye malighafi ya kutengeneza bidhaa za rangi za kupaka nyumba ijulikanayo kama *polyvinyl alcohol.* Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa hizo. *(Makofi)*

(xv) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 0 kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwenye malighafi zinazotumika katika kutengeneza dawa za kuua wadudu *(pesticides,*

*fungicides, insecticides* na *acaricides).* Hatua hii itahusisha viwanda vinavyotumia malighafi hizo kutengeneza dawa za kuua wadudu. Aidha, viwanda vitakavyoagiza malighafi hizo vitatakiwa kupata kibali cha Wizara ya Kilimo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda hivyo. *(Makofi)*

(xvi) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwenye bidhaa za kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *RBD Palm Stearin* inayotambulika kwa *HS Code* 1511.90.40. Hatua hii inahusisha viwanda vinavyotumia bidhaa hiyo katika kutengeneza sabuni. Aidha, hatua ya kupunguza ushuru huo imezingatia kwamba Serikali imeongeza Ushuru wa Forodha katika mafuta ghafi ya mawese. *(Makofi)*

(xvii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwenye viazi *(potato fresh or chilled other than seeds)* vinavyotambuliwa katika *HS Code* 0701.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa viazi hapa nchini. *(Makofi)*

(xviii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwenye chingamu *(chewing gum)* zinazotambulika katika *HS Code* 1704.10.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kwa kuwa kuna uwezo wa kuzalisha chingamu katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

(xix) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye peremende. Hatua hii inachukuliwa kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani na ajira. *(Kicheko)*

(xx) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwenye chokoleti. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazalisha bidhaa hizi na zina uwezo wa kutosheleza mahitaji ya soko. *(Makofi)*

(xxi) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye biskuti. Hatua hii inazingatia kuwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina uwezo wa kuzalisha bidhaa hizo na kutosheleza mahitaji ya soko.

(xxii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye nyanya zinazosindikwa *(tomato sauce).* Lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa bidhaa hizo katika viwanda vya ndani na mashambani. Aidha, imezingatia kwamba nchi yetu inazalisha nyanya za kukidhi mahitaji na pia kuna umuhimu wa kusindika nyanya hizo hapa nchini ili kuongeza thamani na kuongeza ajira katika kilimo cha nyanya. *(Makofi)*

(xxiii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 25 kwenye maji *(mineral water).* Hatua hii ni muhimu katika kuhamasisha uzalishaji na kulinda viwanda vya hapa nchini vinavyozalisha bidhaa hiyo.

(xxiv) Kutoza Ushuru wa Forodha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye nyama *(meat and edibe meat offal in chapter 12)* kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya uchakataji wa nyama hapa nchini na hivyo kuongeza thamani yake. Aidha, itaongeza fursa za ajira na kipato katika sekta ya ufugaji na viwandani.

(xxv) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwenye *sausage.* Hatua hii ina lengo la kulinda na kuhamasisha viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya pia marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Customs Management Act, 2004),* kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki linalotoa

msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye magari yanayotumika kwenye mashindano ya mbio za magari *(rally cars)* na kuingiza pikipiki *(motorcycles)* ili nazo ziweze kupata msamaha huo. Aidha, magari na pikipiki husika hutengenezwa mahsusi kwa ajili ya mashindano hayo. Hatua hii inatarajiwa kuhamasisha mashindano hayo na kukuza sekta ya utalii. *(Makofi)*

(ii) Kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa msamaha kwa boti inayotumika mahsusi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa kwenye maji *(motorboat ambulance)* kama yanavyosamehewa magari ya kutoa huduma kwa wagonjwa. Hatua hii ina lengo la kupunguza gharama za kuwezesha utoaji huduma za matibabu katika usafiri wa majini. *(Makofi)*

(iii) Kufanya maboresho katika Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye magari ya kubebea watalii *(motorvehicle for transport of tourists).* Magari haya yanajumuisha magari ya aina mbalimbali ambayo yametengenezwa mahsusi kwa ajili ya kubebea watalii *(motor-sightseeing buses overland trucks).* Lengo la kutoa msamaha huo ni kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya utalii, kuboresha huduma ya usafiri kwa watalii na kuongeza ajira na mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tumekubaliana kupunguza viwango vya Ushuru wa Forodha *(Duty Remission)* kwenye malighafi na vipuri vinavyohitajika katika kutengeneza nguo na viatu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, tayari nchi hizi zimewasilisha orodha ya malighafi na vifaa vitakavyopunguziwa Ushuru wa Forodha. Uamuzi huo utaanza kutekelezwa mwaka 2018/2019. Hatua hizi za Ushuru wa Forodha kwa pamoja zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,630.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria zinazosimamia Bodi za Mazao. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria zote zinazosimamia Bodi za Mazao Mbalimbali kwa lengo la kuwezesha ushuru wote unaokusanywa na Bodi hizo kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba mapato yatokanayo na ushuru unaotozwa kwenye mazao mbalimbali yanasimamiwa ipasavyo na kutumika kwa ajili ya shughuli zilizokusudiwa. Aidha, shughuli za kuendeleza mazao pamoja na gharama za uendeshaji wa Bodi zitagharamiwa kupitia Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41. Napendekeza kufanya mabadiliko ya kiwango cha kodi katika michezo ya kubahatisha, ubashiri wa matokeo ya michezo *(sports betting)* kutoka asilimia 6 ya mauzo ghafi hadi asilimia 10. Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali kutoka kwenye sekta ndogo ya michezo hiyo ya kubahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye mashine za michezo ya kubahatisha *(slot machines)* kutoka Sh.32,000 hadi Sh.100,000 kwa kila mashine kwa mwezi. Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye michezo ya kubahatisha *(casinos)* kutoka asilimia 15 hadi asilimia 18 ya mapato halisi ambayo hupatikana baada ya kutoa zawadi *(gross gaming revenue).* Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali kwa sababu kiwango cha asilimia 15 kimedumu kwa muda mrefu kuanzia mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye mashine 40 *(40 machine sight)* za michezo ya kubahatisha kutoka asilimia 15 hadi asilimia 20 ya mapato halisi ambayo hupatikana baada ya kutoa zawadi *(gross gaming revenue).* Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za marekebisho ya michezo ya kubahatisha zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 21,198.8.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogomadogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali. Napendekeza kufanya marekebisho mengine madogomadogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho haya yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 na Matangazo ya Serikali yaani *Government Notes*.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea. Napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi. Aidha, marekebisho haya yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 na Matangazo ya Serikali. Marekebisho haya yanajumuisha yafuatayo:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ardhi kwa taasisi za Serikali kwa sababu taasisi hizi ni za umma hazitengenezi faida. Aidha, marekebisho mengine ya ada na tozo mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi yalitangazwa na Waziri mwenye dhamana ya ardhi kwenye hotuba yake. *(Makofi)*

(ii) Kufuta na kupunguza baadhi ya viwango vya tozo na ada zinazotozwa kwenye sekta ya uzalishaji chumvi. Hatua hii imetokana na kuwepo kwa utitiri wa tozo na ada zinazotozwa kwenye madini ya chumvi, hali ambayo inasababisha gharama za uzalishaji kuwa juu na kuwakatisha tamaa wazalishaji kuendelea na uzalishaji wa chumvi. Hivyo napendekeza kufanya marekebisho ya tozo na ada kwenye sekta ya uzalishaji chumvi, kama ifuatavyo:-

(a) Kufuta ushuru wa mazao ya chumvi unaotozwa na Halmashauri. *(Makofi)*

(b) Kufuta Ada ya Ukaguzi wa Madini ya Chumvi (*Inspection and Clearance Fee*) inayotozwa kwa kiwango cha asilimia moja ya thamani ya madini hayo.

(c) Kufuta Ushuru wa Mikoko *(Mangrove Levy)* unaotozwa kwenye maeneo ya uzalishaji wa chumvi kwa kiwango cha Sh.100,000 kwa eka moja kwa mwaka.

(d) Kufuta ada ya kupitia andiko la mradi kwenye sekta ya uzalishaji chumvi inayotozwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

(e) Kufuta Ada ya Usajili la Jangwa la Chumvi (*Solar Salt Panel).*

(f) Kufuta Ada ya Usimamizi kwenye eneo la Chumvi *(Supervision Fee)* inayotozwa na Wakala wa Misitu Tanzanzia.

(g) Kufuta Ada ya Usajili wa Mradi wa Uzalishaji Chumvi inayotozwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

(h) Kufuta Ada ya Ukaguzi wa Mazingira *(Environmental Impact Assessment*) inayotozwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kwenye sekta ya uzalishaji chumvi.

(i) Kupunguza ada ya gharama za ukaguzi wa usalama mahali pa kazi inayotozwa kwenye sekta ya uzalishaji chumvi kutoka Sh.2,000,000 hadi Sh.1,000,000 kwa mwaka.

(j) Kupunguza ada ya kibali cha kusafirisha madini ya chumvi nje ya nchi kutoka Dola za Marekani 100 hadi Sh.20,000 kwa mwaka. *(Makofi)*

(iii) Napendekeza kufanya marekebisho ya ada na tozo zinazotozwa na Mamlaka ya Afya na Usalama *(OSHA)* mahali pa kazi, kama ifuatavyo:-

(a) Kufuta ada inayotozwa kwenye fomu ya usajili sehemu za kazi.

(b) Kufuta tozo ya usajili sehemu za kazi.

(c) Kufuta faini zinazohusiana na vifaa vya kuzima moto inayotozwa kwa kiwango cha Sh.500,000. *(Makofi)*

(d) Kufuta leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama.

(e) Kufuta tozo ya ushauri ya kitaalam ya Usalama wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya uchambuzi na tathmini ya tozo na ada zinazotozwa na Mashirika, Taasisi na Wakala mbalimbali ili kuendelea kuweka mazingira bora ya kufanya biashara na kuwekeza na kuondoa kero kwa wananchi. Hii itajumuisha kupitia upya na kuvisawazisha viwango vya tozo na ada hizo na pia kuondoa tozo na ada za usumbufu.

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kuanza kutekeleza hatua mpya za kodi. Hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2018 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti kwa Mwaka 2018/2019. Kwa kuzingatia shabaha na sera za bajeti kwa mwaka 2018/2019, sura ya Bajeti inaonyesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 32.48 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 20.89 sawa na asilimia 64.3 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 18.0 sawa na asilimia 13.6 ya Pato la Taifa. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 2.16 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 735.6.

Mheshimiwa Spika, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 2.68 ambayo ni asilimia 8.2 ya bajeti yote. Misaada na mikopo hii inajumuisha misaada na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo shilingi trilioni 2, mifuko ya pamoja ya kisekta shilingi bilioni 125.9, Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti (*General Budget Support*) shilingi bilioni 545.8.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 8.9 kutoka soko la ndani na nje kwa masharti ya kibiashara. Mikopo ya ndani inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 5.79 ambapo shilingi trilioni 4.6 ni kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi trilioni 1.19 ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Ili kuongeza kasi katika ujenzi wa miundombinu Serikali itarajiwa kukopa shilingi trilioni 3.11 kutoka soko la nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 32.48. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 20.47 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida yakijumuisha shilingi trilioni 7.41 za mishahara na shilingi trilioni 10 kwa ajili ya kulipia deni la Serikali, michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na huduma nyinginezo. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi trilioni 12.01 sawa na asilimia 37 ya bajeti yote, ambapo shilingi trilioni 9.88 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 2.13 ni fedha za nje. Kiwango hiki cha bajeti ya maendeleo kimezingatia matakwa ya Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano wa kutenga bajeti ya maendeleo kati ya asilimia 30 na asilimia 40 ya bajeti yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza, sura ya bajeti ndiyo hiyo kama nilivyoieleza na inaonekana kwenye Jedwali A kwenye kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kama nilivyotangulia kusema hapo awali dhima ya bajeti ya mwaka 2018/2019 ni kuendelea kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii. Mageuzi haya ya uchumi wa viwanda yatajengwa kupitia ushiriki wetu katika shughuli

za kiuchumi, ubia na kuunganisha juhudi zetu pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo tunayokusudia, maamuzi magumu ni lazima yafanyike katika kuelekeza rasilimali chache tulizonazo katika maeneo ya kimkakati, mabadiliko yoyote ni vigumu kuyakubali na mara nyingi mabadiliko hupingwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla tuunganishe nguvu zetu, vipaji vya wananchi wetu na biashara zetu ili kufikia malengo tunayoyakusudia. Hivyo tunahitaji uzalendo na nidhamu ya kazi ya hali ya juu, tukikusudia kuondoa umaskini, kuongeza ajira na kuwa na uchumi jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo, Serikali itaendelea kuchukua hatua zaidi, kuongeza uzalishaji katika sekta za viwanda na kilimo na ukusanyaji wa mapato ya ndani yatakayowezesha ugharamiaji wa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida na hivyo kupunguza utegemezi. Hatua hizo ni pamoja na kuvutia uwekezaji, kuelekeza rasilimali kwenye maeneo machache yenye tija, kusimamia utekelezaji wa sheria za kodi, kurasimisha sekta isiyo rasmi ikiwemo usajili wa wamiliki wa ardhi na majengo katika mfumo wa walipa kodi na kuhimiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika miamala mbalimbali ikiwemo matumizi ya *EFD* na kadi za kielektroniki za Benki (*Debit/Credit Cards*) katika maeneo yanayotoa huduma kama vile katika maduka makubwa, hoteli na vituo vya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, napenda kuwahimiza Watanzania tuwajibike kulipa kodi na kuhakikisha tunatoa na kudai risiti kulingana na muamala uliyofanyika. Aidha, Serikali inawashukuru kwa dhati kabisa wananchi wote ambao wameonesha uzalendo kwa kuendelea kulipa kodi kwa hiari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kikuu cha Serikali ni kujenga uchumi wa viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini na hasa zinazotokana na kilimo,

mifugo na uvuvi ili kupanua fursa za ajira, kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma za jamii hasa maji, afya, elimu na kupunguza umaskini. Aidha, Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa, kuimarisha ulinzi wa rasilimali za umma na kudhibiti matumizi ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itaongoza msukumo katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kutekeleza mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara. Mpango huu pamoja na mambo mengine unakusudia kuhuisha na kurahisisha taratibu za kulipa kodi, tozo na ada mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inalenga kujenga utamaduni na nidhamu ya kukubali maoteo halisi ya ukusanyaji wa mapato ambayo yanapaswa kuwa ndiyo ukomo wa matumizi, badala ya utaratibu uliozoeleka wa kuanza kupanga au kuorodhesha mahitaji kwanza. Hivyo, Serikali itajielekeza katika utekelezaji wa miradi michache ya kimkakati kwa namna ambayo itashirikisha sekta zote zinazotegemeana na kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilika kabla ya kuanza miradi mipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mpenzi sana wa kujisomea kuhusu maisha na sifa ya viongozi mashuhuri, viongozi bora na wa kipekee wa nchi mbalimbali waliyofanikiwa kuongoza mabadiliko makubwa ya kijamii na kisiasa na kiuchumi katika nchi zao kama Deng Tsiaoping –Jamhuri ya Watu wa China; Dkt. Mahithir Mohamed – Malaysia; Lee Kuan Yew – Singapore; Park Chung Hee – Korea; Nelson Mandela –Afrika ya Kusini; Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere; Quett Masire – Botswana na kadhalika. Nilichojifunza na nililieleza hili katika Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali mwaka jana kuwa viongozi wa aina hiyo wana sifa muhimu zifuatazo:

(i) Dira na maono dhahiri kabisa kuhusu maendeleo ya nchi zao. *(Makofi)*

(ii) Hawasiti kutekeleza dira hizo kwa dhamira kubwa tena bila kusita au kubadili msimamo. *(Makofi)*

(iii) Ni jasiri, shupavu na wenye kuthubutu kutekeleza mambo ambayo wanayaamini bila kigugumizi. *(Makofi)*

(iv) Wanakipaji cha kujali maumivu ya wanyonge. *(Makofi)*

(v) Ni waadilifu, wanachukia rushwa na ufisadi na ni wenye nidhamu ya kazi ya hali ya juu. *(Makofi)*

(vi) Wanaongoza kwa vitendo. *(Makofi)*

(vii) Wanavumilia magumu ili kuiletea nchi mabadiliko chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwaambie tena Watanzania kwamba Mwenyezi Mungu ametutunukia Kiongozi Mkuu wa Nchi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye ana sifa zote hizo nilizozitaja. Nilieleza mwanzoni mwa hotuba hii mambo machache ambayo amethubutu kutenda kwa kipindi kifupi. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Rudia, rudia.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, narudia. Napenda niwaambie tena Watanzania...

**SPIKA:** Mnaotumia *microphone,* hebu msitumie, mwacheni Waziri aongee.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda niwaambie Watanzania kwamba Mwenyezi Mungu ametutunukia Kiongozi Mkuu wa Nchi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, mwenye sifa zote nilizozitaja. Nilieleza mwanzoni mambo machache ambayo amethubutu kutenda kwa kipindi cha kifupi kuthibitisha sifa hizo. Rai yangu kwa Watanzania wenzangu ni kuwa tutumie fursa hii adimu

kufanya kazi kama njia bora ya kumuunga mkono Rais wetu katika jitihada zake za kuijenga Tanzania Mpya, Tanzania ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu jambo hili ni muhimu kwa sababu kama Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alivyotabiri katika safari ya maendeleo ya kuelekea kujenga uchumi wa viwanda Kiongozi wetu atakumbana na vikwazo na kelele nyingi za kuzomea kutoka kwa wale wasiotutakia mema ili kutukatisha tamaa tusifikie malengo. Hivyo, Watanzania wote tunao wajibu wa kumtia nguvu Rais wetu ili asirudi nyuma katika safari aliyoianza na aweze kutuvusha kuifikia Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nimalize rai yangu kwa nukuu ya mazungumzo ya Mwalimu Nyerere kwa *TANU Study Group* ya tarehe 13 Juni, 1967.

*"Maendeleo na kazi ni kitu kile kile, hakuna namna nyingine sisi ya kuendelea, hatukupewa namna nyingine sisi ya kuendelea..... Huwezi kutenganisha vitu viwili hivi, kuendelea na kazi, kwani kazi ndiyo shughuli ya ..... kuondoa matatizo yanayomzuia binadamu hali yake kukamilika.... Hakuna njia nyingine lazima kufanya kazi...... na kila unavyozidi kufanya kazi kwa akili zaidi ndivyo mnavyozidi kwenda, ndivyo mnavyozidi kuendelea,..... Kazi ndio utu ...kazi ndio maendeleo...kazi ndio maisha, ni uhai, kazi ndio civilization, ndio uungwana, ndio kula vizuri, ndio kuvaa vizuri, ndio kuishi katika nyumba nzuri,.... ndio kushinda matatizo yote tuliyo nayo duniani – namna ya kuyashinda ni kazi...."(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nukuu hii inatoka katika insha tatu za kifalsafa za Julius Nyerere 'Kivazi *Occasional Papers* Na. 3 ya Mwaka 2016'.

Mheshimiwa Spika, napoelekea mwisho wa hotuba hii, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa misaada na mikopo wanayoendelea kutupatia katika kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo

nchini. Wahisani hao wanatarajiwa kuchangia jumla ya shilingi trilioni 2.6 katika bajeti ya mwaka 2018/2019 kama ifuatavyo: Benki ya Dunia/*IDA* shilingi bilioni 863.13; Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* shilingi bilioni 358.63; *Global Fund* shilingi bilioni 313.9; Sweden shilingi bilioni 179.8; Jumuiya ya Umoja wa Ulaya shilingi bilioni 158.4; India shilingi bilioni 104.57; Ujerumani kwa maana ya *Kfw* na *GIZ* shilingi bilioni 81.31; Japan/*JICA* yake shilingi bilioni 76.96; Uingereza kupitia *DFID* shilingi bilioni 71.21; Denmark shilingi bilioni 69.57; Ufaransa shilingi bilioni 61.06; Canada shilingi bilioni 48.84; BADEA shilingi bilioni 40.01; Korea ya Kusini/*EDCH* shilingi bilioni 39.05; *UNICEF* shilingi bilioni 36.53; Finland shilingi bilioni 28.08; *IFAD* shilingi bilioni 26.82; Italy shilingi bilioni 22.05; Norway shilingi bilioni 20.04; Benki ya Uwekezaji ya Ulaya shilingi bilioni 17.88; Uswis shilingi bilioni 15.74; *UNDP* shilingi bilioni 13.34; Ubelgiji shilingi bilioni 11.08; Saudi Arabia *(Saudi Fund)* shilingi bilioni 4.81; *USAID* shilingi bilioni 4.2; *OPEC/OFID* shilingi bilioni 2.75; na *UNFPA* shilingi bilioni 2.56. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa fedha zilizoahidiwa na marafiki zetu hawa zitatolewa kama nilivyozisoma na kwa wakati muafaka. Sisi katika Serikali tunaahidi kuwa fedha watakazotupatia tutazitumia kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakiri kuwa bajeti niliyowasilisha isingekuwa hivi ilivyo bila kupata michango mizuri ya kuboresha kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Wataalam wa Wizara zote na Taasisi za Serikali. Natoa shukrani kwa kila mmoja wenu kwa michango mliyotoa katika mchakato mzima wa maandalizi ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango, nikianza na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango; Ndugu Dotto James - Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Naibu Makatibu Wakuu Bibi Amina

Shaaban; Dkt. Khatibu Kazungu; Bibi Susan Mkapa, wote hawa kwa pamoja wamenipatia ushirikiano na msaada wa hali ya juu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na wameratibu vizuri maandalizi ya bajeti hii. Aidha, nampongeza Profesa Florens Dominick Makinyika Luoga kwa kuteuliwa na Rais kuwa Gavana mpya wa Benki Kuu ya Tanzania na kwa kusimamia vema majukumu makubwa ya mhimili huo wa sekta ya fedha akisaidiwa na Naibu Gavana watatu, Wakurugenzi na watumishi wote wa Benki Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, napenda kutambua kazi nzuri ya viongozi na watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kukusanya mapato ya Serikali wakiongozwa na Ndugu Charles Kichere - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato, Profesa Mussa Assad - Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Dkt. Albina Chuwa - Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Aidha, nampongeza Ndugu Athumani Selemani Mbuttuka aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni kuwa Msajili wa Hazina *(Treasury Registrar). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru wakuu wengine wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ikijumuisha mabenki, mifuko ya hifadhi ya jamii, rufani za kodi, huduma za bima, mitaji na dhamana, dhamana za uwekezaji, bodi za michezo ya kubahatisha, taasisi za mafunzo na mfuko wa huduma ndogo za fedha. Nawashukuru pia, Wakuu wa Idara na Vitengo bila kuwasahau Wataalam, Makatibu Muhtasi, Watunza Kumbukumbu, Madereva, Wahudumu na Walinzi wa Wizara yetu na taasisi zake kwa kazi kubwa walizofanya katika mwaka 2017/2018 na katika kukamilisha bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashindwa kumaliza hotuba hii bila kumtaja mke wangu na rafiki yangu mpenzi Mbonimpaye. Nafikiri yuko hapa ndani. Moyo wake wa Ibada kwa Mungu na uaminifu wake vimekuwa ndiyo nguzo yangu kuu katika utumishi wangu. Namshukuru sana yeye pamoja

na watoto na wajukuu wetu wote tuliopewa na Mungu na familia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawiwa kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania, wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara. Nawashukuru sana kwa uzalendo wao wa kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wanafunzi wote wa shule za awali, msingi na sekondari na vyuo wanaosoma kwa bidii. Maana miongoni mwao tutapata viongozi na nguvu kazi bora ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia, wazee wetu wote ambao walitoa mchango mkubwa kwa Taifa letu katika umri wao wa kufanya kazi. Aidha, siwezi kuwasahau wananchi wa Wilaya za Buhigwe na Kasulu. Kwa bahati nzuri wamewakilishwa vizuri na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kasulu Brigedia Jenerali Marco Gaguti, Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, ambaye pia ni Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, lakini pia nawashukuru wananchi wote wa Mkoa wetu wa Kigoma kwa ujumla. Napenda niwaambie kwamba ninyi ni fahari yangu maana mlinikuza, nawapenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawashukuru wananchi wenzangu wa Nzinje hapa Dodoma, Zuzu kwa jina la zamani. Wamenipokea vizuri mimi na familia yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inatarajiwa leo itakuwa siku ya mwisho ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, naomba nihitimishe hotuba hii kwa kuwatakia Waislam wote Eid Mubarak. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nimalize kwa kusema ahsante sana Mungu kwa baraka zako zilizoniwezesha kukamilisha kusoma hotuba hii. Kwenu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, *Sandenyi sana; Ngw'abheja Sana; Waitu Mwakora; Okorree Bhuya;*

*Haikeni Sana; Msengwile; Ndaghafijo; Hewela; Kajekaje; Murakozechane; Ahsanteni Sana. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi/ Vigelegele)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana nimewaona. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO, AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## I. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/19. Bajeti hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 137 ikisomwa pamoja na Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015 kifungu cha 26.

***2.*** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na hotuba hii, ninawasilisha vitabu vinne vya bajeti. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2018 ambayo ni sehemu ya bajeti hii.

***3.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** ni heshima kubwa na upendeleo wa hali ya juu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti ya tatu ya Serikali ya awamu ya tano. Hivyo, namshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu neema nyingi, utulivu na amani na kwa kuniwezesha kuwasilisha bajeti kuu ya Serikali kwa wananchi wa Tanzania kwa mara ya tatu. Pili napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kiongozi wetu shupavu; kiongozi anayeaminiwa na kutumainiwa na wananchi, hasa wanyonge; kiongozi anayechukia na kupiga vita rushwa, ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma kwa vitendo; na Rais anayejipambanua kwa kufanya maamuzi magumu ya kulinda rasilimali za Taifa. Ninampongeza kwa kazi kubwa ambazo ameendelea kuzifanya tangu aliposhika hatamu za uongozi wa Taifa letu, ambazo zimepelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa sana katika kipindi kifupi cha miaka miwili na nusu tu ya utawala wake. Napenda niyataje mambo kumi tu aliyothubutu kutenda na kuiletea nchi mafanikio makubwa:

(i) **Kuhamishia makao makuu ya Serikali Dodoma:** Ametekeleza ndoto ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na uamuzi wa Chama Tawala wa mwaka 1972 wa kuhamishia makao makuu ya Serikali Dodoma. Aidha, kwa mamlaka aliyo nayo amepandisha hadhi ya iliyokuwa Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji kuanzia tarehe 26/4/2018;

(ii) **Kujenga ukuta kuzunguka mgodi wa Tanzanite Mirerani:** Amejenga ukuta wenye mzingo wa kilomita 24.5 kuzunguka machimbo ya madini ya Tanzanite Mirerani, Wilaya ya Simanjiro uliogharimu shilingi bilioni 5.42. Lengo likiwa ni kudhibiti uchimbaji na uuzaji holela wa madini hayo yanayopatikana Tanzania pekee na kuliingizia Taifa mapato. Katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi,

2018 Serikali imefanikiwa kukusanya mrabaha wa shilingi milioni 714.6. Kati ya kiasi hicho, shilingi milioni 614.6 kilitokana na makusanyo kutoka kwa wachimbaji wadogo. Kiasi hicho kilichokusanywa kutoka kwa wachimbaji wadogo kinazidi jumla ya makusanyo ya mrabaha wa miaka mitatu iliyopita. Kiasi kilichokusanywa na Serikali kilikuwa shilingi milioni 116.8 (2015), shilingi milioni71.8 (2016), na shilingi milioni 147.1 (2017);

(iii) **Kudhibiti uuzaji wa makinikia nje ya nchi na kutunga sheria kuwezesha nchi kunufaika na rasilimali zake:** Amezuia usafirishaji wa makontena 277 ya makinikia nje ya nchi yenye thamani ya kati ya shilingi bilioni 829.4 na shilingi bilioni 1,438.8 na kuagiza kutungwa kwa sheria mpya za mfano katika Afrika kuwezesha nchi zenye maliasili kunufaika na rasilimali hizo. Sheria hizo ambazo zilipitishwa na Bunge lako Tukufu ni:

(a) Sheria ya Mamlaka ya nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources - Permanent Sovereignity Act*, 2017*)*;

(b) Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contracts* (*Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act*, 2017; na

(c)Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali ya mwaka 2017 (*The Written Laws - Miscellaneous Ammendments ) Act*, 2017.

(iv) **Kutoa elimu msingi bila ada na kuongeza bajeti ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa zaidi ya mara nane:** Ametoa elimu msingi bila ada ambapo kila mwezi Serikali inalipa shilingi bilioni 20.8. Kutokana na hatua hiyo, uandikishwaji wanafunzi wa darasa la kwanza umeongezeka kutoka watoto 1,568,378 mwaka 2015 hadi watoto 2,078,379 mwaka 2018. Aidha, uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza nao umeongezeka kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 562,695 mwaka 2017. Kadhalika, ameongeza fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu

ambapo mgao uliotolewa mwaka 2017/18 ni shilingi bilioni 409.9 ikilinganishwa na matumizi halisi ya shilingi bilioni 367.4 mwaka 2015/16. Idadi ya wanafunzi wanaopata mikopo hiyo imeongeza kutoka wanafunzi 96,589 mwaka 2015 hadi 122,623 mwaka 2017. Katika sekta ya afya, amethubutu kuongeza bajeti kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kufikia shilingi bilioni 269 mwaka 2017/18 kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/16, hivyo kuimarisha huduma za afya;

(v) **Ununuzi wa ndege mpya kufufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL):** Amefufua Shirika la Ndege la Tanzania kwa kufanya maamuzi magumu ya kununua ndege mpya tatu aina ya Bombardier Q400 zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja ambazo tayari ziko nchini na zinafanya safari za ndani. Aidha, ndege kubwa nyingine tatu (3), moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262 na ndege mbili aina ya Bombardier CS 300 zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja zitawasili nchini baadae mwaka huu. Kadhalika, Serikali imekamilisha taratibu za kupata ndege ya pili kubwa aina ya Boeing 787-8 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262 na malipo ya awali yamekamilika;

(vi) **Kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima, kuondoa watumishi hewa na wenye vyeti vya kughushi:** Amedhibiti matumizi yasiyo ya lazima hususan safari za watumishi wa Serikali nje ya nchi, kuondoa watumishi hewa 19,708 waliokuwa wanalipwa mshahara wa jumla ya shilingi bilioni 19.8 kwa mwezi, na watumishi 14,404 wenye vyeti vya kughushi waliokuwa wanalipwa mshahara wa jumla ya shilingi bilioni 15.5 kwa mwezi, ambazo zote hizo zimeokolewa.

Aidha, chini ya utawala wake, nidhamu katika utumishi wa umma imeimarika na ameanzisha Mahakama ya mafisadi ili kupambana na mafisadi wanaonyonya uchumi wa nchi;

(vii) **Ujenzi wa reli ya kati ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa (*Standard Gauge Railway – SGR*):** Ameanza ujenzi

wa reli ya kati ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa *(Standard Gauge Railway – SGR).* Awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 205) na awamu ya pili kutoka Morogoro hadi Makutupora Dodoma (km 422) tayari zinatekelezwa. Awamu zote mbili zitagharimu takriban Dola za Marekani bilioni 3.14;

(viii) **Ujenzi wa mradi wa umeme katika bonde la mto Rufiji**: Amefanya uamuzi wa kuanza ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme katika mto Rufiji (*Stiegler's Gorge*) ambao nao ulikuwa ndoto ya Baba wa Taifa utakaozalisha MW 2,100 utakapokamilika nao umeanza katika hatua za awali;

(ix) **Kuimarisha usimamizi wa mapato ya ndani**: Ametekeleza ahadi yake kwa Watanzania kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti ukwepaji kodi, hatua ambazo zimewezesha Serikali kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 kwa mwezi hadi wastani wa shilingi tirioni 1.3 kwa mwezi;

(x) **Kuendeleza umeme vijijini na kusitisha miradi ya wazalishaji binafsi wa umeme (IPPs):** Ameendeleza utekelezaji wa mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini kupitia REA Awamu ya Tatu kwa ufanisi mkubwa, ambapo ndani ya miaka miwili na nusu ya utawala wake jumla ya vijiji 557 vimeunganishwa umeme. Vijiji hivyo vimetokana na utekelezaji wa miradi ya *REA II* na *REA III* ya kuongeza msongamano (*densification*), mkongo (*backbone*) na ule wa kusafirisha umeme Makambako - Songea. Aidha, amesitisha miradi ya wazalishaji binafsi wa umeme *(Independent Power Producers – IPPs)* ambayo ilikuwa inaigharimu Serikali fedha nyingi. Vile vile, bila yeye mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi bandari ya Tanga usingepatikana na tayari ujenzi unaendelea;

**4.** **Mheshimiwa Spika**, yapo mambo mengi sana makubwa (barabara, meli, madaraja, maji, usimamizi wa sekta ya fedha n.k.) ambayo Jemadari huyu ametekeleza, lakini kwa uchache wa muda siwezi kuyataja yote. Haya yote ni ushahidi usio na mashaka kwamba Tanzania chini ya

Rais Magufuli imeshika kasi ya maendeleo. Hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuchangia katika jitihada hizi za Mheshimiwa Rais kujenga Tanzania mpya. Maeneo matatu ya msingi sana kwa kila mwananchi kuwajibika ni: (i) uzalendo kwa nchi yetu; (ii) kupiga vita wizi, ubadhirifu na ufisadi; na (iii) kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi.

5. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo za dhati kwa Rais wetu, napenda kumshukuru kwa moyo wangu wote kwa kuendelea kuniamini na kuniongoza katika kazi zangu za Waziri wa Fedha na Mipango. Hata pale nilipoelemewa na kazi na kulaumiwa kwamba waziri huyu ni bahili mno katika kutoa fedha na baadhi wakinipaka tope la kiburi, alinitia moyo. Niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Rais kwa nini alinitwika mimi kazi hii nzito kama msalaba wa zege, tena bila matumaini ya kutokea mtu mfano wa Simon wa Kirene katika Biblia wa kuja kunipokea mzigo huu!. Yeye alinijibu kwamba "*Mungu atawatuma malaika wake watakusaidia!*" na akaongeza kwamba *"lazima watu wachache tuwe tayari kuumia kwa faida ya Watanzania wengi maskini".* Naomba nikiri kuwa, majibu hayo yalinichoma na kunikumbusha sala ya wana "*Opus Dei"* katika mateso isemayo "*Mapenzi ya Mungu, yenye haki na yanayopendeza sana, yafanyike, yatimizwe, yasifiwe na kutukuzwa kuliko vitu vyote milele. Amina. Amina*." Baada ya hapo, nilipata amani ya kuendelea katika utumishi huu. Asante sana Mheshimiwa Rais. Najua unasikiliza!.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kumsaidia Rais kuongoza Taifa letu kwa hekima na uadilifu. Kadhalika, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza Zanzibar kwa busara, jambo ambalo limepelekea wananchi wa Zanzibar kuishi katika hali ya amani na utulivu mkubwa kwa kipindi cha miaka saba na nusu sasa. Aidha, ninampongeza sana Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo

la Ruangwa, kwa kuwa kapteni hodari wa timu ya Serikali hapa Bungeni na kwa kumsaidia Rais kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala CCM ya mwaka 2015 – 2020. Vile vile, ninawapongeza wakuu wa mihimili mingine ya dola, nikianza na wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Kongwa kwa kuliongoza Bunge kwa umahiri; na Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa kazi nzuri ya kuongoza chombo cha utoaji haki. Napenda vile vile kumpongeza Mheshimiwa Balozi Mhandisi John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni mkuu wa Utumishi wa Umma na Katibu wa Baraza la Mawaziri kwa utumishi uliotukuka.

7. **Mheshimiwa Spika,** ni vema pia niwapongeze waheshimiwa wenza wa viongozi wakuu wa kitaifa kwa umuhimu wao wa kipekee. Niruhusu niwataje kwa majina yao Mwalimu Janet Magufuli, Bwana Ameir Hafidh Ameir, Mama Mwanamwema Shein, Mwalimu Mary Majaliwa, Dkt. Fatuma Ramadhani Mganga, na Mama Marina Papadopoulos Juma. Tunawapongeza na kuwashukuru kwa kuwawezesha viongozi wetu wakuu wa kitaifa kutekeleza vizuri majukumu yao kwa utulivu, hamasa na tabasamu kutokana na mapenzi makubwa wanayopata nyumbani.

8. **Mheshimiwa Spika,** napenda niwapongeze na kuwashukuru wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama ambao ni Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Mabeyo; Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Sirro; Kamishna Jenerali wa Magereza, Dkt. Juma Ali Malewa; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakala; Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Dkt. Modestus Kipilimba; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Kamishna wa Polisi, Valentino Mlowola; Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya Bw. Rogers William Sianga; na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Bw. Thobias Andengenye. Mimi na Watanzania wenzangu tunawapongeza kwa dhati kabisa viongozi hawa, pamoja na makamanda, askari na watumishi wote wa vyombo hivi nyeti kwa kuendelea kuilinda nchi yetu kwa ushupavu,

kudumisha amani na usalama na kuwawezesha wananchi wote wa Tanzania kufanya shughuli za maendeleo kwa utulivu. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt Adelardus Lubango Kilangi kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na ninamshukuru kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 na Muswada wa Sheria ya Matumizi wa mwaka 2018.

**9.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia fursa hii pia kutoa shukrani mahsusi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mbunge wa Babati Vijijini. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Bajeti wakati wa kuchambua mapendekezo ya bajeti ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, ulikuwa wa kizalendo na wenye tija. Aidha, ninawapongeza Wenyeviti, Makamu wenyeviti na wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa michango yao waliyoitoa kupitia vikao vya kamati za kisekta katika kuboresha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/19 ili kuwapatia wananchi wa Tanzania huduma bora zaidi.

**10.** **Mheshimiwa Spika,** kama ilivyokuwa mwaka 2017/18, dhima ya bajeti ya mwaka 2018/19 kwa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa ni **"kujenga uchumi wa viwanda utakao chochea ajira na ustawi endelevu wa jamii**". Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia uhalisia wa nchi yetu ambao sisi wote tunaufahamu, kwa maana ya changamoto kuu za kiuchumi na kijamii zinazotukabili, fursa tulizo nazo, mafanikio hadi sasa na malengo yetu kama Taifa. Naomba nifafanue haya kwa kifupi:

**a)** **Changamoto**

(i) Bado tuna *kiwango kikubwa cha umaskini* ambapo taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kiwango cha umaskini kimepungua kidogo kutoka asilimia 28.2 (2011/12) hadi asilimia 26.4 (2015/16). Matarajio ni kuwa Utafiti wa

Matumizi ya Kaya unaoendelea hivi sasa utatupatia taarifa nzuri zaidi ya kuendelea kupungua kwa umaskini kwa kuzingatia kuwa uchumi wa Taifa umeendelea kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka katika miongo miwili sasa;

(ii) *Ukosefu wa fursa za ajira* hasa kwa vijana, ambapo takwimu zinaonesha kuwa asilimia 10.4 ya Watanzania hawana ajira. Vile vile kati ya vijana wanaohitimu masomo yao wapatao 800,000 kila mwaka, uwezo wa Serikali kuajiri ni wastani wa watu 40,000 tu;

(iii) *Sekta ya kilimo* (inayojumuisha mazao, mifugo na uvuvi) ambayo inaajiri asilimia 66 ya Watanzania na inachangia asilimia 30 ya Pato la Taifa inaendelea kukua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 3.7 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita kutokana na uwekezaji mdogo, tija ndogo na kutegemea mvua, sambamba na mchango mdogo wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa wa asilimia 5.5;

(iv) *Mahitaji makubwa ya upatikanaji wa huduma muhimu za jamii (hasa maji, afya na elimu bora)* na yanaongezeka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu (asilimia 3.1 kwa mwaka). Aidha, hali ya miundombinu ya umeme, usafiri na usafirishaji (barabara, reli, usafiri wa anga na majini) bado haikidhi mahitaji ya uchumi kukua kwa kasi zaidi na kugusa wananchi wengi. Mathalani, mtandao wa barabara nchini ni kilomita 86,472 ambapo ni asilimia 9.7 tu ndiyo za kiwango cha lami. Aidha, mahitaji ya umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na viwandani bado ni makubwa ikilinganishwa na uwezo wa uzalishaji. Mitambo iliyopo kwa sasa ina uwezo wa kuzalisha Megawati 1,424.6 ikilinganishwa na mahitaji ya zaidi ya Megawati 3,000 ili kuweza kuhimili mahitaji ya uchumi wa viwanda; na

(v) *Wigo mdogo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani* ambapo uwiano wa mapato ya ndani na Pato la Taifa ni takriban asilimia 15.0 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.0 kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

**b)Fursa**

**11. Mheshimiwa Spika,** maandalizi ya bajeti hii pia yamezingatia fursa mbalimbali tulizo nazo katika Taifa letu hususan nguvukazi kubwa ya Taifa ambao ni vijana; rasilimali na fursa nyingi tulizonazo katika kilimo (mazao, mifugo, na uvuvi); madini; gesi; vivutio vya utalii; viwanda vya huduma za kilimo (agri- business); vyanzo mbalimbali vya uzalishaji wa umeme; biashara na huduma za usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani.

**c) Mafanikio**

**12. Mheshimiwa Spika,** bajeti hii pia imezingatia mafanikio tuliyopata hadi hivi sasa ambayo hatuna budi tuyaimarishe na nitayaeleza kwa muhtasari katika sehemu ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti.

**d)Malengo**

**13. Mheshimiwa Spika,** bajeti hii vile vile imeandaliwa kwa kuzingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Ilani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020. Malengo makuu ni kuondokana na umaskini na kuibadilisha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda na kuingia kwenye kundi la nchi zenye kipato cha kati (Middle Income Countries) ifikapo mwaka 2025.

**14. Mheshimiwa Spika**, changamoto, fursa mafanikio na malengo niliyoyaeleza sasa hivi lazima yaende pamoja na wajibu upande wa Serikali, sekta binafsi, wadau wengine na mwananchi mmoja mmoja, wa kuzipatia majibu changamoto hizo na kuchangia ipasavyo katika jitihada za kulipeleka Taifa letu mbele. Tutafanya hivyo ikiwa kila mwananchi atafanya kazi na kutumia uwezo wake wote kwa ajili ya maendeleo yake na ya Taifa. Aidha, ni muhimu pia tuendelee kujenga na kutumia ubia wa kimkakati (*harness strategic partnerships*). Ujumbe wangu kwa Watanzania kupitia bajeti hii ni kuwa, lazima tuendelee kufanya chaguo

gumu (*tough choices*) katika kuelekeza rasilimali kidogo tunazokusanya ili tuweze kuzishinda changamoto hizo zilizoko mbele yetu. Ukweli ni kuwa, mabadiliko ni magumu na mara nyingi yanapingwa!. Hivyo, lazima tuwe imara, tukusudie kufanikiwa na tutumie vizuri fursa na uwezo wa Watanzania, sekta binafsi na Serikali ili kufikia azma yetu.

15. **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba niliyosoma leo asubuhi, nilieleza kwa kirefu hali ya uchumi wetu ilivyokuwa katika mwaka 2017, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/18, mafanikio yetu na changamoto tulizokumbana nazo na niliainisha pia maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2018/19. Katika hotuba hii nitajikita zaidi katika masuala ya kibajeti, nikianza na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/18, hatua muhimu zitakazopewa msukumo zaidi upande wa matumizi katika mwaka ujao wa fedha, maboresho ya mfumo wa kodi na tozo mbalimbali na mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2018/19.

## II. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18

### Mwenendo wa Mapato

16. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 mapato kutoka vyanzo vyote yalifikia shilingi trilioni 21.89 sawa na asilimia 69 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi trilioni 31.71 Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:

### A. Mapato ya Ndani

17. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi trilioni 14.84 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi trilioni 19.98 kwa mwaka sawa na asilimia 74.3. Kati ya kiasi hicho, makusanyo ya kodi yalikuwa shilingi trilioni 12.61; makusanyo yasiyo ya kodi ni shilingi trilioni 1.79; na makusanyo ya Halmashauri ni shilingi bilioni 437.6. Kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji

kumetokana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Ukwepaji wa kodi;

(ii) Ugumu wa kutoza kodi wafanya biashara walioko katika sekta isiyo rasmi kwa vile hawana sehemu rasmi na za kudumu za kufanyia biashara na hawatunzi kumbukumbu;

(iii) Mazingira yasiyo rafiki ya ulipaji kodi na mlolongo wa kodi na tozo, hasa huduma zinazotolewa na mamlaka za udhibiti na usimamizi (zikiwemo *TBS, TFDA, EWURA, TCRA, OSHA*, Zimamoto), viwango vikubwa vya kodi; urasimu katika taratibu za kulipa kodi, na ugumu na gharama kubwa za kulipa kodi;

(iv) Matumizi hafifu ya mashine za kielektroniki za kutolea risiti (*EFD*);

(v) Udhaifu katika usimamizi wa uvunaji wa rasilimali za nchi hasa madini, gesi asilia, misitu, rasilimali bahari, utalii na ardhi; na

(vi) Mchango mdogo na utegemezi wa mashirika ya umma katika bajeti ya Serikali.

**B. Mikopo ya Ndani na Nje yenye Masharti ya Kibiashara**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikopa jumla ya shilingi trilioni 4.96 kutoka soko la ndani sawa na asilimia 80 ya shilingi trilioni 6.17 zilizotarajiwa kukopwa kwa mwaka 2017/18. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 4.13 zilikopwa kwa ajili ya kulipia dhamana na hati fungani za Serikali zilizoiva (rollover), na shilingi bilioni 832.3 zilikopwa ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, Serikali ilikopa kutoka soko la nje shilingi bilioni 224 sawa na asilimia 14 ya lengo la kukopa shilingi trilioni 1.6. Fedha hizi zimeelekezwa kwenye utekelekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati. Aidha, mwezi Mei, 2018, Serikali ilipokea mkopo wa kibiashara kiasi cha shilingi trilioni 1.13.

## C. Misaada na Mikopo Nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

19. **Mheshimiwa Spika,** misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikuwa shilingi trilioni 1.87 sawa na asilimia 47 ya makadirio ya mwaka ya shilingi trilioni 3.97. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 70.2 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti sawa na asilimia 7.5 ya makadirio ya shilingi bilioni 941.3, shilingi bilioni 182.9 ni misaada na mikopo nafuu ya Mifuko ya Kisekta sawa na asilimia 33 ya makadirio ya shilingi bilioni 556.1, na shilingi trilioni 1.61 ni misaada na mikopo nafuu ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 65 ya makadirio ya shilingi trilioni 2.47.

### Mwenendo wa Matumizi

20. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili 2018, Serikali imetoa jumla shilingi trilioni 21.68 sawa na asilimia 68.4 ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 31.71. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 16.56 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha shilingi trilioni 5.63 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa umma na shilingi trilioni 8.42 kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali na mahitaji mengine ya Mfuko Mkuu.

21. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili, 2018 Serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 5.12 kwa ajili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi trilioni 4.35 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 775.8 ni fedha za nje. Hata hivyo, kiasi hiki hakijumuishi fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi ambazo hazikupita kwenye mfumo wa malipo wa Serikali. Fedha hizi zitajumuishwa pindi taratibu ya kiuhasibu zitakapokamilika.

22. **Mheshimiwa Spika,** naomba nieleze mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/18 katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018 kama ifuatavyo:

(i) Jumla ya shilingi bilioni 59.0 zimetolewa katika Halmashauri za Wilaya 110 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya, na shilingi bilioni 24.1 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali za mikoa 24. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 125.7 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi;

(ii) Kiasi cha shilingi bilioni 156.1 kimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini;

(iii) Kiasi cha shilingi bilioni 409.9 kimetolewa kwa ajili ya miradi ya nishati vijijini, umeme wa jotoardhi, uzalishaji wa umeme katika vyanzo mbalimbali na usambazaji wa gesi asilia;

(iv) Katika kutekeleza azma ya kutoa elimumsingi bila ada na kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, Serikali imetoa shilingi bilioni 618.0;

(v) Serikali imeendelea kutekeleza ujenzi wa miundombinu ili kupanua fursa za uchumi, kilimo, biashara na viwanda ikiwemo barabara zinazounganisha mikoa na nchi jirani, barabara zinazopunguza msongamano katika majiji, barabara za vijijini, reli, viwanja vya ndege, na bandari. Katika eneo hili kiasi cha shilingi trilioni 1.87 kimetolewa; na

(vi) Serikali imeendelea kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi umma, wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ambapo kiasi cha shilingi trilioni 1.17 kimelipwa.

**23. Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imeendelea kuchukua hatua nyingine zenye lengo la kuimarisha usimamizi wa bajeti ya Serikali kama ifuatavyo:

### a) Deni la Serikali

**24. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Deni la Serikali linadhibitiwa na linaendelea kuwa himilivu, Serikali inaendelea kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana, na Misaada SURA 134. Aidha, Serikali inatekeleza Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni unaotoa dira ya namna bora ya ukopaji ili kuepuka gharama na athari mbalimbali

zinazoweza kujitokeza katika kusimamia deni la Serikali. Katika kudhibiti kuongezeka kwa gharama za mikopo, Serikali ilijikita zaidi kukopa kwenye mikopo yenye masharti ya kati (*Semi Concessional Loans)* hasa mikopo inayowezesha uagizaji wa vifaa na mitambo kutoka nchi inayokopesha (*Export Credit Agency - ECA)* na pale ilipolazimu, mikopo ya masharti ya kibiashara ilikopwa kwa uangalifu mkubwa ikiwemo kuhakikisha kwamba mikopo hiyo inatumika kwenye maeneo ambayo yanachochea ukuaji wa uchumi.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili 2018, deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 49.65 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 13.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 43.79 Aprili 2017. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 14.05 na deni la nje shilingi trilioni 35.60 sawa na asilimia 71.71 ya deni lote. Ongezeko la deni hilo limetokana na mikopo ya zamani na inayoendelea kupokelewa yenye masharti nafuu au kibiashara na malimbikizo ya riba ya Deni la Nje hasa kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris ambazo Serikali bado inajadiliana nazo kuhusu msamaha wa madeni kulingana na makubaliano na kundi hilo.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** Mikopo nafuu kutoka Mashirika ya Fedha ya Kimataifa imeendelea kuwa chanzo kikubwa cha mikopo kutoka nje ambayo imechangia asilimia 59.6 ya deni lote la nje. Mikopo yenye masharti ya kibiashara imechangia asilimia 28.5, wakati mikopo kutoka nchi wahisani imechangia asilimia 11.9. Mikopo hii imetumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Deni la Serikali limekuwa likiongezeka. Hata hivyo deni hilo limeendelea kuwa himilivu na ukuaji wake unawiana na kasi ya ukuaji wa uchumi wetu. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba 2017 inaonesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Uwiano wa deni kwa thamani ya sasa (present value) kwa Pato la Taifa ni asilimia 34.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 56; thamani ya deni la nje kwa mauzo ya nje ilikuwa asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150; thamani ya deni la nje kwa mapato ya ndani

asilimia 117.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250; ulipaji wa deni la nje kwa mapato yatokanayo na mauzo nje asilimia 9.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ulifikia asilimia 13.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Napenda kusisitiza tena kwamba hakuna dhambi kwa nchi kukopa kwa busara (prudently). Mambo ya muhimu ya kujiridhisha nayo ni kuwa mikopo hiyo inatumika kujenga uwezo zaidi wa kuzalisha mali (productive capacity) na kurejesha mikopo hiyo kwa kuzingatia uwezo wa uchumi kuhimili mzigo wa madeni (debt sustainability).

**b) Kudhibiti Malimbikizo ya Madai ya Serikali**

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kupunguza malimbikizo ya madai ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kila mwaka kwenye bajeti kwa ajili ya kulipa madai yaliyohakikiwa; kuhimiza uzingatiaji wa sheria na kanuni zake kama vile, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; Sheria ya Ununuzi wa Umma SURA 410; Sheria ya Fedha za Umma SURA 348 na kanuni zake na kutoa miongozo na maelekezo mbalimbali yakiwemo Waraka Na. 1 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali unaotolewa kila mwaka kuhusu utekelezaji wa bajeti na Mwongozo wa Mpango na Bajeti unaotolewa kila mwaka.

**29.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na changamoto hiyo ya malimbikizo ya madai, Serikali imeandaa *Mkakati wa Kulipa Madeni na Kuzuia ulimbikizaji wa Madeni*. Madai yanayohusika kwenye Mkakati huo ni yale yaliyozalishwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea (*MDAs*) na Sekretarieti za Mikoa (*RSs*) yakiwemo madeni ya Watumishi, Wazabuni na Watoa Huduma, pamoja na madai ya Wakandarasi. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa madai yaliyohakikiwa kwa kuzingatia mpango (roadmap) ulioandaliwa kulipa madeni hayo hadi yatakapofikia kiwango himilivu. Katika ulipaji wa madeni, kipaumbele kitatolewa kwa madeni yanayogusa watoa huduma wengi na yale ambayo yanaongezeka kutokana na riba.

**30. Mheshimiwa Spika,** Mkakati huo unamtaka kila Afisa Masuuli kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake ili kuiwezesha Serikali kufikia malengo yake ya kudhibiti malimbikizo ya madai na kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati. Hivyo, katika kuhakikisha kwamba hakuna madeni mapya yanayozalishwa, kila Afisa Masuuli atapaswa kuzingatia yafuatayo:

(i) Mikataba yote ya ujenzi wa miundombinu inazingatia viwango vya bajeti vilivyowekwa katika kila Fungu. Aidha, Fungu husika lisiingie mikataba nje ya viwango hivyo bila kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali; vile vile Kifungu cha 51(1) na (2) cha Sheria ya Bajeti ya 2015 kinaelekeza kwamba miadi yote ya miaka zaidi ya mmoja (*Multi-year Commitments*) lazima ipate idhini ya Waziri wa Fedha ikiwa imezingatia viwango vya bajeti, malipo ya miadi hii isizidi viwango/bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, pamoja na kulipa madai baada ya uhakiki;

(ii) Kutoa kipaumbele kwa ukamilishaji wa miradi inayoendelea kabla ya kuanzisha miradi mipya, sambamba na kuhakikisha kwamba miradi inayoanzishwa inatengewa fedha katika bajeti;

(iii) Maafisa Masuuli kutoingia makubaliano ya kupatiwa huduma au bidhaa bila ya kuwa na fedha au kibali cha maandishi kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali; na miadi yoyote ni lazima iingizwe kwenye mtandao wa *IFMS*;

(iv) Madai ya watoa huduma wote na Wakandarasi lazima yafanyike baada ya kupata hati za ununuzi (*LPO*) kutoka kwenye mfumo wa *IFMS* iliyozingatia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, pamoja na kuwepo kwa ridhaa ya matumizi (*Exchequer Issue Notification*) kwa vifungu husika vya matumizi. Hivyo, Serikali inasisitiza kwamba, LPO zilizotoka kwenye mfumo wa Malipo ya Serikali (*IFMIS*) ndiyo zitumike kama msingi wa malipo kwa Watoa Huduma; na

(v) Kuzingatia matumizi ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Sheria ya Fedha za Umma SURA 348 na

waraka wa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu utekelezaji wa bajeti.

**III. SERA ZA BAJETI KWA MWAKA 2018/19 Shabaha za Uchumi Jumla na Bajeti**

**31. Mheshimiwa Spika,** Shabaha za uchumi jumla na bajeti katika kipindi cha mwaka 2018/19 ni kama ifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 7.1 mwaka 2017;

(ii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 15.3 mwaka 2017/18 na uwiano halisi wa asilimia 15.6 mwaka 2016/17;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.6 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 13.0 mwaka 2017/18 na uwiano halisi wa asilimia 13.3 mwaka 2016/17;

(v) Matumizi ya Serikali kufikia asilimia 24.5 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 23.0 mwaka 2017/18 na matumizi halisi ya asilimia 22.2 mwaka 2016/17; na

(vi) Nakisi ya bajeti kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 2.1 mwaka 2017/18 na uwiano halisi wa asilimia 1.5 mwaka 2016/17.

**Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato**

**32. Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, sera za mapato kwa mwaka 2018/19 zitalenga katika kuongeza wigo wa kodi, kuimarisha usimamizi wa vyanzo vilivyopo hususan katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki na hatua nyingine za kiutawala.

**33.** **Mheshimiwa Spika,** katika **kuongeza wigo wa kodi**, yapo maeneo makuu mawili yatakayozingatiwa na Serikali ambayo ni kurasimisha sekta isiyo rasmi na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kupata vyanzo vipya vya mapato vitokanavyo na uwekezaji huo. Zipo hatua za urasimishaji zilizoanza kufanyika mfano uthaminishaji wa majengo, na upimaji wa viwanja, zoezi ambalo linaendelea nchi nzima. Serikali itaongeza kasi ya urasimishaji ikiwa ni pamoja na kuwepo na mbinu bunifu, rafiki, shirikishi na za kimkakati.

**34.** **Mheshimiwa Spika,** mazingira bora ndio msingi mkuu wa kuvutia biashara na uwekezaji ikiwemo kuboresha miundombinu msingi, vivutio vya kikodi, sera zisizobadilika (*policy consistency and predictability*), upatikanaji wa ardhi na taratibu za kisheria na usimamizi. Pale mazingira yanapokuwa mazuri, uwekezaji, uzalishaji, ajira na miamala ya kibiashara inaongezeka na hivyo kupelekea kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Serikali mwaka 2017/18 ulibaini changamoto zifuatazo kuhusiana na mazingira ya biashara na uwekezaji :

(i) Migongano ya sheria, kanuni na taratibu zinazotumiwa na mamlaka mbalimbali;

(ii) Gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara kutokana na wingi wa kodi, ada na tozo zinazoambatana na taratibu ngumu na nyingi zenye urasimu usio na tija na hivyo kutoa mianya na mazingira ya rushwa; na

(iii) Muingiliano wa majukumu na wingi wa mamlaka za udhibiti katika kuidhinisha na kutoa hati, vibali na vyeti kwenye shughuli za uwekezaji na biashara.

**36.** **Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Serikali imeandaa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve Business Environment for Tanzania*). Miongoni mwa mapendekezo ya Mpango huo ambayo yatatekelezwa kwa

nguvu zaidi kuanzia mwaka ujao wa fedha (2018/19) ni kurahisisha taratibu za kulipa kodi, tozo na ada mbalimbali, na kupunguza muda na mlolongo mrefu wa kusajili makampuni na biashara. Serikali ya Awamu ya Tano inaamini kuwa maendeleo endelevu yatapatikana kwa haraka zaidi katika mazingira yenye ushirikiano wa kweli na wa dhati kati ya sekta ya um
ma na sekta binafsi.

**37.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyopo, Serikali itaendelea na zoezi la uunganishaji wa Wizara, Idara, Wakala, taasisi na mashirika ya umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato (*Government electronic Payment Gateway* - GePG) ili kuboresha ukusanyaji na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Mfumo huu ulianzishwa mwaka 2017 na kupitishwa na Bunge kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma SURA 348 ambayo iliziagiza taasisi zote za Serikali kukusanya mapato kwa kutumia Mfumo wa *GePG*. Hadi mwezi Mei, 2018, jumla ya taasisi 234 zinazokusanya maduhuli zikijumuisha Halmashauri zote 185 zimeunganishwa kwenye Mfumo huu. Nachukua fursa hii kuagiza Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali zilizobaki zihakikishe kwamba zimeunganishwa na kuanza kutumia mfumo wa *GePG* kabla ya Juni, 2019. Mbali na Mfumo huu, ninawakumbusha Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa maduhuli unafanyika kwa kutumia mashine za kielektroniki (EFDs) pamoja na benki na siyo risiti za kuandikwa kwa mkono.

**38.** **Mheshimiwa Spika,** kuhusu **hatua nyingine za kiutawala** za kuongeza mapato ya Serikali, ninaelekeza yafuatayo:

(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ichukue hatua za makusudi za kuboresha mahusiano kati yake na walipa kodi kwa lengo la kuondoa dhana iliojengeka miongoni mwa walipa kodi kuwa TRA inatumia nguvu na vitisho kudai kodi;

(ii) Ofisi ya Msajili wa Hazina iimarishe usimamizi na ukaguzi kwenye kampuni ambazo Serikali ina hisa ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata gawio stahiki katika uwekezaji wake; na

(iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa zijielekeze kwenye miradi itakayochochea upatikanaji wa mapato katika mamlaka hizo hususan viwanda, masoko na machinjio ya kisasa, stendi za mabasi, stendi za maegesho ya malori kwenye mipaka na nchi jirani na maghala ya kuhifadhi nafaka.

**Kuimarisha Ushirikiano na Washirika wa Maendeleo**

**39. Mheshimiwa Spika,** misaada na mikopo nafuu imekuwa ikipungua kutoka wastani wa asilimia 26.3 ya bajeti halisi ya mwaka 2010/11 hadi asilimia 10.4 mwaka 2016/17. Kutokana na umuhimu wa kuwa na maendeleo endelevu na kuhakikisha kuwa misaada na mikopo nafuu inapatikana kama ilivyoahidiwa na kwa wakati, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendelo na wadau wengine imekamilisha Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework - DCF*). Mwongozo huo uliidhinishwa na Serikali mwezi Agosti 2017 na umebainisha:

(i) Misingi ya jumla ya kuongoza ushirikiano ambayo ni pamoja na Serikali kuongoza michakato ya kuibua vipaumbele vya miradi ya maendeleo; na

(ii) Mfumo wa majadiliano ambao uko katika ngazi tatu; Majadiliano ya Kitaifa ya Kimkakati, Majadiliano ya Kisekta na Majadiliano yenye Mwelekeo wa Kisiasa.

**Sera za Matumizi**

**40. Mheshimiwa Spika,** sera za matumizi katika mwaka 2018/19 zitajumuisha:

(i) Kudhibiti nakisi ya bajeti isizidi asilimia 3.2 ya Pato la Taifa;

(ii) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele na yenye tija ili kuchochea ukuaji wa kilimo na viwanda, kupanua fursa za ajira, kujenga na kuboresha miundombnu ya uchumi na kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za jamii;

(iii) Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuendelea kupunguza matumizi yasiyo ya lazima; na

(iv) Kudhibiti ulimbikizaji wa madai.

**41. Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia sera hizi, Serikali itachukua hatua zifuatazo:

(i) Kuwachukulia hatua za kisheria kinidhamu na kiutawala wote watakaothibitika kwenda kinyume na sheria na kanuni zinazoongoza utendaji katika nafasi zao. Napenda niwakumbushe tena kuwa kula fedha za miradi ya wananchi ni sawa na kula sumu – wasijaribu!!

(ii) Kuhakikisha kuwa Maafisa Masuuli hawaingii mikataba bila kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha au ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali na kuzuia matumizi na ahadi (*commitments*) za matumizi nje ya mfumo wa "IFMS". Lengo ni kudhibiti ulimbikizaji wa madai;

(iii) Kuwianisha matumizi na mapato halisi yatakayopatikana kwa kila mwezi;

(iv) Kulipa madai mbalimbali yaliyohakikiwa;

(v) Kuhakikisha kuwa ununuzi wa umma unawiana na thamani ya fedha itakayotumika; na

(vi) Kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma ili zitumike kama ilivyokusudiwa.

**Maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2018/19**

**42.** **Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 ambao niliuwasilisha leo asubuhi, bajeti ya matumizi katika mwaka 2018/19 itaweka mkazo zaidi katika uendelezaji wa miradi ya kielelezo; kufungamanisha maendeleo ya watu; na ujenzi wa mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji na uendeshaji biashara.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** maeneo ya kipaumbele katika bajeti hii ni yafuatayo:

(i) **Kilimo:** Fedha zitaelekezwa zaidi kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo, kupanua huduma za ugani, kuboresha mfumo wa utafiti na utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wananchi, na uendelezaji wa sekta ndogo za uvuvi na mifugo. Mkazo umewekwa katika sekta hii kwa kuzingatia kuwa inategemewa na wananchi wengi na ndiyo itakayotupatia malighafi kwa ajili ya viwanda, kutuhakikishia usalama wa chakula na kuongezeka kwa kipato cha wananchi;

(ii) **Viwanda:** Katika kuchochea ukuaji wa viwanda nchini, Serikali itaelekeza nguvu zake kwa kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi hususan viwanda vya nguo, ngozi na nyama, samaki, mafuta ya kula, madawa na vifaa tiba, vyakula vya binadamu na mifugo, na katika sekta ya madini. Aidha, uendelezaji wa viwanda na kilimo utapaswa kuzingatia uendelevu wa mazingira;

(iii) **Huduma za Jamii: Maji:** Eneo lingine muhimu ni kuongeza upatikanaji na usambazaji wa maji safi hasa vijijini na uondoshaji wa majitaka, uchimbaji wa visima katika maeneo kame nchini na ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati. **Elimu:** Serikali itaendelea kugharamia elimu msingi bila ada, kuongeza idadi ya wataalam katika fani adimu kwenye maeneo ya madini, mafuta na gesi, madaktari

bingwa (moyo na figo) pamoja na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. **Afya:** rasilimali fedha zitaelekezwa kuongeza usambazaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na uboreshaji wa huduma katika vituo vya afya, zahanati na hospitali za rufaa. Vile vile katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaelekeza fedha zaidi za *LGCD* kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri hususan miradi ya elimu na afya. Aidha, Serikali itaweka msukumo kuimarisha upatikanaji wa **lishe bora** kwa mama na mtoto hususan katika siku 1,000 za mtoto tangu kutungwa kwa mimba ili kuondokana na changamoto ya kuwa na watoto wenye udumavu na hivyo kukua vema kimwili na kiakili. Aidha, mahitaji ya **makundi maalum** katika jamii yetu (wanawake, vijana, watoto, watu wenye ulemavu na wazee) yataendelea kuangaliwa kipekee;

(iv) Kujenga na kukarabati **miundombinu wezeshi** hususan kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali, kuendelea na ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha kimataifa (*standard gauge*), ujenzi wa barabara za kuunganisha mikoa na zile za vijijini, na kuimarisha usafiri wa anga na majini; na

(v) Maeneo mengine ya kipaumbele ni: kurahisisha umiliki wa ardhi, kuimarisha huduma za mawasiliano, kifedha na utalii na kuimarisha ulinzi, usalama, utawala bora, na utoaji haki.

## IV. HATUA ZA MAPATO NA MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA NA TOZO MBALIMBALI

### Maboresho ya Mfumo wa Kodi, Ada na Tozo Mbalimbali

**44.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali na pia taratibu za ukusanyaji na usimamiaji wa mapato ya Serikali. Marekebisho haya yanalenga pamoja na mambo mengine, kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika sekta

ya Viwanda, Utalii, kukuza ajira, na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, marekebisho haya yamezingatia dhamira ya Serikali ya kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wenye kutabirika. Marekebisho hayo yanahusu Sheria zifuatazo:-

a. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;

b. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;

c. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;

d. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290;

e. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;

f. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; na Sheria ya Benki Kuu, SURA 197;

g. Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;

h. Sheria zinazosimamia Bodi za Mazao;

i. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha SURA 41;

j. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali; na

k. Marekebisho ya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea.

**a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148**

**45.** **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani,Sura 148 kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya madawa ya binadamu

vitakavyotengenezwa mahsusi kwa ajili ya viwanda vinavyozalisha dawa hapa nchini. Aidha, vifungashio hivyo vitakuwa na machapisho ya majina ya kiwanda husika cha utengenezaji madawa ili kuhakikisha kwamba vinatumiwa na viwanda hivyo na siyo vinginevyo. Lengo la hatua hii nikupunguza gharama za uzalishaji na kuvilinda viwanda vinavyotengeneza madawa hapa nchini ili viweze kumudu ushindani na kuongeza uzalishaji;

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye virutubisho vinavyotumika kutengenezea vyakula vya mifugo (*animal and poultry feeds additives*) vinavyoagizwa kutoka nje. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wafugaji na kuhamasisha ufugaji bora ili kuongeza mchango wa Sekta hiyo katika Uchumi;

(iii) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 6(2)(a) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na maswala ya fedha kutoa msamaha wa kodi kwa miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa mikopo ya kibiashara. Hivi sasa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inakataza kusamehe kodi kwenye mikopo ya kibiashara hali ambayo imesababisha kukwama kwa utekelezaji wa miradi muhimu ya Serikali kama vile miradi ya Maji, barabara n.k. Hivyo, marekebisho yanayopendekezwa yatawezesha utekelezaji wa miradi ya Serikali kwa wakati uliopangwa;

(iv) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 6(2)(a) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kusamehe kodi hiyo pale ambapo kuna mkataba uliosainiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Taasisi ya Fedha au Benki ambayo ni "mwakilishi" wa Serikali nyingine aliyepewa dhamana na Serikali hiyo kuingia mikataba na kusimamia utekelezaji wa miradi husika. Hivi sasa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inampa mamlaka Waziri huyo kusamehe kodi pale ambapo kuna mkataba baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya nchi nyingine unaotoa msamaha wa kodi. Hivyo miradi mingi inayohusisha mikataba ya

misaada au mikopo kupitia mabenki na Taasisi za fedha imekwama utekelezaji wake. Kwa msingi huo, marekebisho haya yanalenga katika kuondoa ukwamishaji na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi mingi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kupitia mikataba inayosainiwa na Serikali yetu na Benki au Taasisi za Fedha za Serikali za nchi nyingine; na

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike (*sanitary pads)* HS Code 9619.00.10. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hii muhimu kwa bei nafuu kwa ajili ya kulinda afya ya mama na mtoto wa kike hasa watoto walio shuleni na vijijini. Ni matarajio ya Serikali kuwa wazalishaji na wauzaji wa taulo za kike wataziuza kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi hii.

Hatua hizi zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 219.1**

**b) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**46. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ili kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni (*Corporate Income Tax*) kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2018/19 hadi mwaka 2022/23 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya madawa ya binadamu na viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi. Aidha, Serikali itaingia mkataba wa makubaliano (*performance agreement*) na kila mwekezaji ambao utaainisha wajibu wa kila upande. Lengo la hatua hii ni kuongeza uwekezaji katika sekta ya madawa ya binadamu na usindikaji wa ngozi ambao kwa sasa haufanyiki nchini na pia kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Aidha, hatua hii itapunguza matumizi ya fedha za kigeni

zinazotumika kuagiza dawa hizo kutoka nje na kuhamasisha uzalishaji wa madawa mengi zaidi hapa nchini;

(ii) Kufuta kifungu cha 10A cha Sheria ya Kodi ya Mapato kinachomkataza Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kutoa msamaha wa kodi kwenye miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ya kibiashara *(non concessional loans)*. Lengo la hatua hii ni kumpa mamlaka Waziri huyo kutoa msamaha wa kodi ya mapato kwa miradi hiyo ambayo imekuwa na changamoto katika utekelezaji wakati Serikali inapopata mikopo ya aina hiyo; na

(iii) Kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato ili kutoa msamaha wa Kodi ya zuio inayotozwa kwenye riba kwa mikopo inayotolewa kwa Serikali na Benki, Taasisi za Fedha na wahisani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali.

Hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 220.5.**

**c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**47.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Kifungu cha 124(2), marekebisho ya viwango maalum vya Ushuru wa Bidhaa *(specific duty rates)* zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Hata hivyo, ili kutekeleza azma ya Serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa viwanda, napendekeza kutofanya mabadiliko ya viwango maalum vya Ushuru wa Bidhaa zisizo za petroli zinazozalishwa hapa nchini na kuongeza viwango vya Ushuru wa Bidhaa zisizo za petroli zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo:-

(i) Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji baridi utaendelea kutozwa kwa kiwango cha shilingi 61 kwa lita;

(ii) Ushuru wa Bidhaa kwenye maji ya kunywa yaliyosindikwa kwenye chupa yaliyoagizwa kutoka nje utaongezeka kutoka shilingi 61 kwa lita hadi shilingi 64.05 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 3.05 kwa lita. Aidha, Ushuru wa Bidhaa kwenye maji yanayozalishwa hapa nchini utaendelea kutozwa kwa kiwango cha sasa cha shilingi 58 kwa lita;

(iii) Ushuru wa Bidhaa kwenye maji ya matunda (juisi) iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini *(local juices)* hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha shilingi 9 kwa lita;

(iv) Ushuru wa Bidhaa kwenye maji ya matunda (juisi) iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini *(imported juices)* utaongezeka kutoka shilingi 221 kwa lita hadi shilingi 232 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 11 kwa lita;

(v) Ushuru wa Bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa *(Beer from Local Unmalted Cereals)* hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha shilingi 450 kwa lita;

(vi) Ushuru wa Bidhaa kwenye bia zinazoagizwa kutoka nje ya nchi utaongezeka kutoka shilingi 765 kwa lita hadi shilingi 803.25 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 38.25 kwa lita;

(vii) Ushuru wa Bidhaa kwenye bia zisizo za kilevi, ikijumuisha vinywaji vya kuongeza nguvu vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi utaongezeka kutoka shilingi 561 kwa lita hadi shilingi 589.05 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 28.05 kwa lita. Aidha, Ushuru wa Bidhaa kwenye bia zisizo za kilevi, ikijumuisha vinywaji vya kuongeza nguvu vinavyozalishwa hapa nchini utaendelea kutozwa kwa kiwango cha sasa cha shilingi 561 kwa lita;

(viii) Kuanzisha Ushuru wa Bidhaa wa shilingi 200 kwa lita kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda (kama ndizi, rozela/choya, nyanya, nk)

yanayozalishwa hapa nchini tofauti na zabibu kwa kiwango kinachozidi asilimia 75;

(ix) Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha shilingi 200 kwa lita;

(x) Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, utaongezeka kutoka shilingi 2,349 kwa lita hadi shilingi 2,466 kwa lita, ikiwa ni ongezeko la shilingi 117 kwa lita;

(xi) Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyoagizwa kutoka nje utaongezeka kutoka shilingi 3,481 kwa lita hadi shilingi 3,655.05 kwa lita, ikiwa ni ongezeko la shilingi 174.05 kwa lita. Aidha, Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyozalishwa nchini hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha shilingi 3,315 kwa lita;

(xii) Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha shilingi 12,447 kwa kila sigara elfu moja;

(xiii) Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zenye kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, hautaongezeka na utaendelea kutozwa kwa kiwango cha shilingi 29,425 kwa kila sigara elfu moja;

(xiv) Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zenye sifa tofauti na **(xii) na (xiii)** utaongezeka kutoka shilingi 53,235 hadi shilingi 55,896.75 kwa kila sigara elfu moja ikiwa ni ongezeko la shilingi 2,661.75 kwa kila sigara elfu moja;

(xv) Ushuru wa Bidhaa kwenye tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* inayoagizwa kutoka nje

utaongezeka kutoka shilingi 26,888 hadi shilingi 28,232.4 kwa kilo, ikiwa ni ongezeko la shilingi 1,344.4 kwa kilo; na

(xvi) Ushuru wa Bidhaa wa 'cigar' unabaki kuwa asilimia 30.

**48.** **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kuanzisha Mfumo Mpya wa Stempu za Kodi za kielektroniki utakaoanza kutumika tarehe 1 Septemba 2018. Mfumo mpya wa Stempu za Kodi za kielektroniki utaiwezesha Serikali kutumia teknolojia ya kisasa kupata taarifa sahihi za uzalishaji viwandani na kwa wakati (real time) zinazotumika kupanga mipango ya maendeleo ya Taifa. Pia mfumo huu mpyautaiwezesha Serikali kudhibiti uvujaji wa mapato na kutambua mapema kiasi cha Kodi ya Ushuru wa Bidhaa, Kodi ya Mapato na ile ya Ongezeko la Thamani itakayolipwa. Aidha, mfumo wa Stempu za Kodi za kielektroniki utadhibiti tatizo la uwepo wa stempu za karatasi za kughushi ambalo linachangia uwepo wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na zinazoweza kuathiri afya za binadamu. Mfumo huu mpya unatumika katika nchi nyingine ikiwa pamoja na Kenya, Morocco, Uturuki, Malaysia na Switzerland na umekuwa na mafanikio makubwa.

Hatua za Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 119,456.6**

**d) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290.**

**49.** **Mheshimiwa Spika** napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 kama ifutavyo:-

(i) Kuongeza kifungu cha 37A kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa ili kumpa Mamlaka Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa Kuzitaka Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya fedha wanazokusanya kutoka kwenye vyanzo vyao vya mapato kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya vijana na wanawake. Aidha asilimia 50 ya fedha hizo zitatengwa kwa

ajili ya vikundi vya vijana na asilimia 50 kwa vikundi vya wanawake. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais- TAMISEMI ataandaa Kanuni ambazo zitaweka utaratibu wa kusimamia utoaji wa fedha hizo kwa vikundi vya vijana na wanawake vilivyosajiliwa. Pia, fedha zitatolewa kwa kuwakopesha bila kutoza riba yoyote; na

(ii) Kurekebisha kifungu cha 16(6) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, ambacho kinatoa mwanya kwa Taasisi/Makampuni yanayolipa Ushuru wa Huduma kutolipa Ushuru wa Mazao. Mfano, Makampuni mengi yanayochakata zao la mkonge ili kuzalisha nyuzi za katani yanamiliki pia mashamba ya mkonge. Hivyo siyo busara kuwalipisha ushuru wa mazao na ushuru wa huduma. Hata hivyo, yapo makampuni yenye mashamba ya mkonge ambayo hayachakati mkonge, haya yanapaswa kulipa ushuru wa mazao badala ya ushuru wa huduma. Napendekeza kiongezwe kifungu cha 16(7) kwenye Sheria hiyo kuyataka Makampuni yanayozalisha mazao na hayachakati kwa ajili ya kuyaongezea thamani yawajibike kulipa Ushuru wa Mazao.

**e) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**

**50.** **Mheshimiwa Spika,** napendekeza Kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi SURA 438, ili kuanzisha utaratibu maalum wa kusamehe kodi (Tax Amnesty) ambao unalenga kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu (Interest and Penalties) kwa kiwango cha asilimia 100. Msamaha huo utatolewa kwa kipindi cha miezi sita (6) kinachoanzia tarehe 1 Julai 2018 mpaka tarehe 31 Desemba 2018. Aidha kwa kufanya hivyo, Serikali inatarajia kukusanya malimbikizo ya madeni ya nyuma ya kodi (Principal Tax) pamoja na kuinua kiwango cha ulipaji kodi kwa hiyari kwa zaidi ya asilimia 10.

Hatua hiyo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 500,000.**

**f) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290, Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348 na Sheria ya Benki Kuu, SURA 197.**

**51. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kurekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290, Sheria ya Fedha za Umma Sura 348, na Sheria ya Benki Kuu, Sura 197 ili kuanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina (Treasury Single Account) ambapo akaunti hii itatumika kupokea fedha zote za Serikali na kufanya malipo yote ya Serikali. Msingi wa kuanzishwa kwa akaunti hii ni kutekeleza makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyozitaka nchi wanachama kuanzisha akaunti jumuifu ili kuimarisha usimamizi wa fedha za Serikali. Uwepo wa akaunti hii pamoja na mambo mengine utarahisisha usimamizi wa fedha za Serikali kwa kupunguza idadi ya akaunti kwenye benki za biashara na Benki Kuu, kupunguza gharama za kibenki zinazolipwa hivi sasa na Serikali kufuatia huduma zinazotolewa kwa Serikali na Benki za Biashara, kupunguza nakisi kwenye mfuko Mkuu wa Serikali ambapo akaunti maalum zitajumuishwa kwenye ukokotoaji wa bakaa katika Mfuko Mkuu wa Serikali tofauti na utaratibu wa hivi sasa ambapo akaunti hizi hazijumuishwi katika ukokotoaji huo.

**g) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

**52. Mheshimiwa Spika,** kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi ya Bajeti (Pre-Budget consultations of Ministers of Finance) kilichofanyika tarehe 4 Mei, 2018 mjini Arusha, Tanzania kilipendekeza kufanya marekebisho ya Viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha (EAC – Common External Tariff "CET") na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Customs Management Act, 2004) kwa Mwaka 2018/19. Mapendekezo hayo yanalenga kwa kiwango kikubwa katika kuchochea maendeleo ya viwanda ili kukuza ajira na ustawi wa jamii (Industrialization for Job Creation and Shared Prosperity).

**53. Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano (HS Code 1001.99.00 na HS Code 1001.99.90) kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuendelea kutoa unafuu kwa viwanda vya wazalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano na kuimarisha utulivu wa bei kwa bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia ngano hiyo. Aidha, hatua hii inazingatia kwamba bado kiwango cha uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu ni kidogo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo hautoshelezi mahitaji. Ili kudhibiti uagizaji wa bidhaa hii, utaratibu wa *"Duty Remission"* utatumika ambapo viwanda vinavyotumia ngano ya aina hii katika uzalishaji ndivyo vitakavyohusika na kutumia kiwango hicho cha msamaha wa Ushuru wa Forodha;

(ii) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwenye mashine za Kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali (Electronic Fiscal Devices) zinazotambulika katika HS Code 8470.50.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inatarajiwa kuendelea kutoa unafuu na kuhamasisha wafanyabiashara na walipa kodi kutumia mashine hizo katika kufanya mauzo na kuongeza ufanisi katika Usimamizi na Udhibiti wa kodi;

(iii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 15 badala ya asilimia 25 kwenye karatasi zinazotambulika katika HS Codes 4804.11.00; 4804.21.00; 4804.31.00; na 4804.41.00. Utaratibu wa *"Duty Remission"* utatumika ambapo wazalishaji wanaotumia karatasi hizo katika kutengeneza madaftari na vitabu ndio watakaofaidika. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wazalishaji hao. Ni matarajio ya Serikali kwamba wazalishaji watauza bidhaa hizi kwa bei nafuu na hivyo kuwezesha watumiaji, hususan wanafunzi, kuzipata kwa gharama nafuu;

(iv) Kutoza Ushuru wa forodha wa asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazoingizwa kutoka nje kwa ajili ya utengenezaji wa gypsum board (Gypsum paper for manufacturing of gypsum board) zinazotambulika katika HS Code 4805.92.00;

(v) Kutoza Ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 100 kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (consumption sugar) inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (gap sugar) la uzalishaji hapa nchini. Hivi sasa sukari hiyo inatozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 100;

(vi) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye *"Gypsum Powder"* inayotambuliwa kwa HS Code 2520.20.00 kwa mwaka mmoja. Marekebisho haya yanalenga katika kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo hapa nchini na kuhamasisha wawekezaji watumie *"gypsum"* inayopatikana hapa nchini kuzalisha *"gypsum" powder*. Aidha, hatua hii inatarajiwa kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

(vii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa ijulikanayo kama *"Self- adhesive label"* (HS Code 4821.10.90) ambayo hutumika kama alama ya kutambulisha aina ya bidhaa kwa watengenezaji wa dawa za meno. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama ya uzalishaji kwenye viwanda vya dawa za meno kwa kuwa self-adhesive labels hazizalishwi hapa nchini;

(viii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwenye bidhaa ijulikanayo kama *"Printed Alluminium Barrier Laminates"* (ABL) HS Code 3920.10.90 kwa mwaka mmoja. Aidha utaratibu wa *"duty remission"* utatumika ambapo hatua hii itawahusu wenye viwanda vinavyoagiza bidhaa hiyo kwa matumizi ya kiwandani. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama ya uzalishaji kwa viwanda vya dawa za meno. Aidha, ina lengo la kuvilinda viwanda hivi kutokana na ushindani na ajira;

(ix) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ghafi ya kula ya mawese (Crude Palm Oil) yanayotambulika katika HS Code 1511.10.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta na mafuta ya kula hapa nchini kwa kuzingatia kuwa nchi yetu ina fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo. Aidha, lengo ni kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mafuta ghafi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Pia inatarajiwa kwamba uzalishaji wa mbegu utaongezeka na kuongeza ajira viwandani na mashambani pamoja na kuongeza kipato cha wakulima;

(x) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 0 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ghafi ya kula (mfano alizeti, mawese, soya, mzaituni, nazi, karanga, mahindi n.k). Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa mbegu na mafuta ya kula hapa nchini kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini. Aidha, inatarajiwa kwamba hatua hii italinda viwanda na ajira katika sekta ndogo ya mafuta ya kula, na kuongeza mapato ya serikali na wakulima;

(xi) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati na cha mwisho (*semi-refined, refined/double refined oil*) mfano alizeti, mawese, soya, mzaituni, nazi, karanga, mahindi n.k. Ongezeko hilo la Ushuru wa Forodha linatarajiwa kulinda uzalishaji wa mafuta ya kula na kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta zinazozalishwa nchini badala ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Aidha, hatua hii inatarajiwa kupunguza fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi;

(xii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za chuma za misumari zinazotambulika

katika HS Code 7317.00.00 (nails, tacks, drawing pins, corrugated nails, staples other than those of heading 83.05). Hatua ya kuweka kiwango hicho cha Ushuru wa Forodha inalenga katika kulinda viwanda vya bidhaa hizo hapa nchini kutokana na uingizaji wa bidhaa kama hizo kutoka nje ya nchi;

(xiii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za kimarekani 1.35 kwa kilo moja ya viberiti (safety matches) vinavyotambuliwa kwenye HS Code 3605.00.00 kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Hatua hii inazingatia kuwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina uwezo wa kuzalisha viberiti na kutosheleza mahitaji katika soko hivyo kuwepo na umuhimu wa kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo;

(xiv) Nchi za Jumuiya zimekubaliana kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwenye malighafi ya kutengeneza bidhaa za rangi za kupaka nyumba ijulikanayo kama *"polyvinyl Alcohol"* (HS Code 3905.30.00). Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa hizo;

(xv) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 0 kwa utaratibu wa *"duty remission"* kwenye malighafi (*inputs*) zinazotumika katika kutengeneza dawa za kuua wadudu (*pesticides, fungicides, insecticides na acaricides*). Hatua hii itahusisha viwanda vinavyotumia malighafi hizo kutengeneza dawa za kuua wadudu. Aidha, viwanda vitakavyoagiza malighafi hizo vitatakiwa kupata kibali cha Wizara ya Kilimo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda hivyo;

(xvi) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa utaratibu wa duty remission kwenye bidhaa ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *"RBD Palm Stearin"* inayotambulika katika HS Code 1511.90.40. Hatua hii inahusisha viwanda vinavyotumia bidhaa hiyo katika kutengeneza sabuni. Aidha, hatua ya kupunguza ushuru huo imezingatia kwamba Serikali imeongeza ushuru wa forodha katika mafuta ghafi ya mawese;

(xvii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye viazi *(potatoes fresh or chilled, other than seeds)* vinavyotambulika katika HS Code 0701.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa viazi hapa nchini;

(xviii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye Chingamu (*Chewing Gum*) zinazotambulilka katika HS Code 1704.10.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kwa kuwa kuna uwezo wa kuzalisha chewing gum katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(xix) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye peremende HS Code 1704.90.00. Hatua hii inachukuliwa kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani na ajira;

(xx) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye Chokoleti *(chocolates)* HS Code 18.06. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazalisha bidhaa hizi na zina uwezo wa kutosheleza mahitaji ya soko;

(xxi) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye Biskuti (*Biscuits*) zinazotambullika kwa HS Code 1905. Hatua hii inazingatia kuwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina uwezo wa kuzalisha bidhaa hiyo na kutosheleza mahitaji ya soko;

(xxii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye nyanya zilizosindikwa (*tomato sauce*) zinazotambulika katika HS Code 2103.20.00. Lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa bidhaa hiyo katika viwanda vya ndani na mashambani. Aidha, imezingatia kwamba nchi yetu inazalisha nyanya za kukidhi mahitaji na pia kuna umuhimu wa kusindika nyanya hizo hapa nchini ili kuongeza thamani na kuongeza ajira katika kilimo cha nyanya;

(xxiii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 25 kwenye maji (*mineral water*) yanayotambulika

katika HS Code 2201.10.00. Hatua hii ni muhimu katika kuhamasisha uzalishaji na kulinda viwanda vya hapa nchini vinavyozalisha bidhaa hiyo;

(xxiv) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye nyama (*meat and edible meat offal in chapter 12*) kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya uchakataji wa nyama hapa nchini na hivyo kuongeza thamani yake. Aidha, itaongeza fursa za ajira na kipato katika sekta ya ufugaji na viwandani; na

(xxv) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye Soseji (*sausages)* na bidhaa za aina hiyo (HS Code 1601.00.00). Hatua hii ina lengo la kulinda na kuhamasisha Viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**54.** Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya pia marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Customs Management Act, 2004*) kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki linalotoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye magari yanayotumika kwenye mashindano ya mbio za magari (*rally cars*) na kuingiza pikipiki (*motorcycles*) ili nazo ziweze kupata msamaha huo. Aidha, magari na pikipiki husika hutengenezwa mahsusi kwa ajili ya mashindano hayo. Hatua hiyo inatarajiwa kuhamasisha mashindano hayo na kukuza sekta ya utalii;

(ii) Kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa msamaha kwa boti inayotumika mahsusi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa kwenye maji (*Motor Boat Ambulance*) inayotambulika katika HS Code 8903.99.10 kama vile yanavyosamehewa magari ya kutoa huduma kwa

wagonjwa (*Motor Vehicle Ambulance*). Hatua hii ina lengo la kupunguza gharama na kuwezesha utoaji wa huduma za matibabu katika usafiri wa majini; na

(iii) Kufanya Marekebisho katika Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye magari ya kubebea watalii (*Motor vehicle for Transport of Tourists*). Magari haya yanajumuisha magari ya aina mbalimbali ambayo yametengenezwa mahsusi kwa ajili ya kubebea watalii (*Motor sightseeing buses, overland trucks*). Lengo la kutoa msamaha huo ni kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya utalii, kuboresha huduma ya usafiri kwa watalii na kuongeza ajira na mapato ya Serikali.

**55**. **Mheshimiwa Spika,** Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tumekubaliana kupunguza Viwango vya Ushuru wa Forodha (*duty remission*) kwenye malighafi na vipuri vinavyohitajika katika kutengeneza nguo na viatu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, tayari nchi hizi zimewasilisha orodha ya malighafi na vifaa vitakavyopunguziwa Ushuru wa Forodha. Uamuzi huo utaanza kutekelezwa mwaka 2018/19.Hatua hizi za Ushuru wa Forodha kwa pamoja zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 1,630.2**

**h) Sheria zinazosimamia Bodi za Mazao.**

**56.** **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria zote zinazosimamia Bodi za mazao mbalimbali kwa lengo la kuwezesha ushuru wote unaokusanywa na bodi hizo kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba mapato yatokanayo na ushuru unaotozwa kwenye mazao mbalimbali yanasimamiwa ipasavyo na kutumika kwa ajili ya shughuli zilizokusudiwa. Aidha, shughuli za kuendeleza mazao pamoja na gharama za uendeshaji wa Bodi zitagharamiwa kupitia Bajeti ya Serikali.

**i) Sheria ya Michezo ya kubahatisha, SURA 41**

**57. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya mabadiliko ya kiwango cha kodi katika michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo (*sports betting*) kutoka asilimia 6 ya mauzo ghafi hadi asilimia 10. Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali kutoka kwenye sekta ndogo ya michezo hiyo ya kubahatisha.

**58. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho ya kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye mashine za michezo ya kubahatisha (*slot machines*) kutoka shilingi 32,000 hadi shilingi 100,000 kwa kila mashine kwa mwezi. Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali.

**59. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye michezo ya kubahatisha (*Casino*) kutoka asilimia 15 hadi asilimia 18 ya mapato halisi ambayo hupatikana baada ya kutoa zawadi (*Gross Gaming Revenue -GGR*). Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali kwa sababu kiwango cha asilimia 15 kimedumu kwa muda mrefu kuanzia mwaka 2012.

**60. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho ya kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye mashine arubaini (*Forty Machines Site*) za michezo ya kubahatisha kutoka asilimia 15 hadi asilimia 20 ya mapato halisi ambayo hupatikana baada ya kutoa zawadi (*Gross Gaming Revenue -GGR*). Lengo ni kuongeza mapato ya Serikali.

Hatua hizi za marekebisho ya michezo ya kubahatisha zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 21,198.8.**

**j) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.**

**61. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera

katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine mbalimbali ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 na Matangazo ya Serikali *(Government Notices).*

**k) Marekebisho ya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea.**

**62. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi. Aidha, marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 na Matangazo ya Serikali (*Government Notices*). Marekebisho hayo yatajumuisha:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ardhi kwa Taasisi za Serikali kwa sababu taasisi hizi ni za umma hazitengenezi faida. Aidha, marekebisho mengine ya ada na tozo mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi yalitangazwa na Waziri mwenye dhamana ya ardhi kwenye hotuba yake;

(ii) Kufuta na kupunguza baadhi ya viwango vya tozo na ada zinazotozwa kwenye sekta ya uzalishaji wa Chumvi. Hatua hii imetokana na kuwepo kwa utitiri wa tozo na ada zinazotozwa kwenye Madini ya Chumvi hali ambayo inasababisha gharama za uzalishaji kuwa juu na kuwakatisha tamaa wazalishaji kuendelea na uzalishaji wa chumvi. Hivyo napendekeza kufanya marekebisho ya tozo na ada kwenye sekta ya uzalishaji chumvi kama ifuatavyo:-

a) Kufuta ushuru wa mazao ya chumvi unaotozwa na Halmashauri;

b) Kufuta ada ya ukaguzi wa madini ya chumvi (*Inspection and Clearance fee*) inayotozwa kwa kiwango cha asilimia moja (1%) ya thamani ya madini;

c) Kufuta ushuru wa Mikoko (*Mangrove Levy*) unaotozwa kwenye maeneo ya uzalishaji wa chumvi kwa kiwango cha shillingi 100,000 kwa eka moja kwa mwaka;

d) Kufuta ada ya kupitia andiko la mradi kwenye sekta ya uzalishaji chumvi inayotozwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira;

e) Kufuta ada ya usajili wa Jangwa la Chumvi (*Solar Salt Panel);*

f) Kufuta ada ya Usimamizi kwenye eneo la Chumvi (*Supervision fee*) inayotozwa na Wakala wa Misitu Tanzania;

g) Kufuta ada ya usajili wa mradi wa uzalishaji chumvi inayotozwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira;

h) Kufuta ada ya Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Impact Assesment*) inayotozwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kwenye sekta ya uzalishaji chumvi;

i) Kupunguza ada ya gharama za ukaguzi wa usalama mahala pa kazi inayotozwa kwenye sekta ya uzalishaji chumvi kutoka shilingi millioni 2 hadi shilingi millioni 1 kwa mwaka; na

j) Kupunguza ada ya kibali cha kusafirisha madini ya chumvi nje ya nchi kutoka Dola za Kimarekani 100 hadi shilingi 20,000 kwa mwaka.

(iii) Napendekeza kufanya marekebisho ya ada na tozo zinazotozwa na Mamlaka ya Afya na Usalama (OSHA) mahali pa kazi kama ifuatavyo:-

a) Kufuta ada inayotozwa kwenye fomu ya usajili sehemu za kazi;

b) Kufuta tozo ya usajili sehemu za kazi;

c)Kufuta faini zinazohusiana na vifaa vya kuzimia moto inayotozwa kwa kiwango cha shilingi 500,000;

d) Kufuta Leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya afya na usalama; na

e) Kufuta tozo ya ushauri wa kitaalam ya usalama wa afya.

**63.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kufanya uchambuzi na tathmini ya tozo na ada zinazotozwa na mashirika, taasisi na wakala mbalimbali ili kuendelea kuweka mazingira bora ya kufanya biashara na kuwekeza na kuondoa kero kwa wananchi. Hii itajumuisha kupitia upya na kuvisawazisha viwango vya tozo na ada hizo na pia kuondoa tozo na ada za usumbufu.

### l) Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi

**64.** **Mheshimiwa Spika,** hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2018, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

## V. SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2018/19

**65.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia shabaha na sera za bajeti kwa mwaka 2018/19, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 32.48 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Jumla ya mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 20.89, sawa na asilimia 64.3 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 18.0 sawa na asilimia 13.6 ya Pato la Taifa. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yanakadiriwa kuwa

shilingi trilioni 2.16 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 735.6.

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 2.68 ambayo ni asilimia 8.2 ya bajeti yote. Misaada na mikopo hii inajumuisha misaada na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo shilingi trilioni 2.0; mifuko ya pamoja ya kisekta shilingi bilioni 125.9; na misaada na mikopo nafuu ya kibajeti (*GBS*) shilingi bilioni 545.8.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 8.90 kutoka soko la ndani na nje kwa masharti ya kibiashara. Mikopo ya ndani inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 5.79, ambapo shilingi trilioni 4.6 ni kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zinazoiva (*rollover*) na shilingi trilioni 1.19 ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Ili kuongeza kasi katika ujenzi wa miundombinu, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 3.11 kutoka soko la nje.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 32.48. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20.47 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi trilioni 7.41 za mishahara na shilingi trilioni 10.00 kwa ajili ya kulipia deni la Serikali, michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na huduma nyinginezo. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi trilioni 12.01 sawa na asilimia 37 ya bajeti yote, ambapo shilingi trilioni 9.88 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 2.13 ni fedha za nje. Kiwango hiki cha bajeti ya maendeleo kimezingatia matakwa ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 wa kutenga bajeti ya maendeleo kati ya asilimia 30 na 40 ya bajeti yote.

***69.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza, sura ya bajeti kwa mwaka 2018/19 ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali A.**

**Jedwali A: Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2018/19**

| | | |
|---|---|---|
| | | **Shilingi Milioni** |
| | | |
| **A.** | **Mapato ya Ndani-Serikali Kuu** | **20,158,989** |
| | (i) Mapato ya Kodi (TRA) | *18,000,219* |
| | (ii) Mapato yasiyo ya kodi | *2,158,770* |
| **B.** | **Mapato ya Halmashauri** | **735,589** |
| **C.** | **Mapato na Mikopo nafuu kutoka nje** | **2,676,645** |
| | (i) Misaada na Mikopo nafuu -GBS | *545,765* |
| | (ii) Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | *2,005,016* |
| | (iii) Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | *125,864* |
| **D.** | **Mikopo ya Ndani na Nje yenye Masharti ya Kibiashara** | **8,904,727** |
| | (i) Mikopo ya Nje | *3,111,058* |
| | (ii) Mikopo ya Ndani | *1,193,669* |
| | (iii)Mikopo ya Ndani- Rollover | *4,600,000* |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)** | **32,475,950** |
| | | |
| | **Matumizi** | |
| **E.** | **Matumizi ya Kawaida** | **20,468,676** |
| | | |
| | o/w (i) Deni la Taifa | **10,004,480** |
| | -Malipo ya Riba Ndani | *1,413,631* |
| | -Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | *4,600,000* |
| | -Malipo ya Mtaji Nje | *1,669,653* |
| | - Malipo ya Riba Nje | *689,667* |
| | - Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii | *1,195,866* |
| | -Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | *435,663* |
| | (ii) Mishahara | ***7,409,952*** |
| | (iii)Matumizi Mengineyo (OC) | ***3,054,244*** |
| | - Matumizi yaliyolindwa (Protected Expenditure) | *1,891,695* |
| | - Matumizi ya Halmashauri (own source) | *389,862* |
| | - Matumizi mengine ya kuendesha ofisi | 772,687 |
| **F.** | **Matumizi ya Maendeleo (Asilimia 37.0) ya BGT** | **12,007,273** |
| | (i) Fedha za Ndani | *9,876,393* |
| | o/w Matumizi ya Halmashauri | *345,727* |
| | (ii) Fedha za Nje | *2,130,880* |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)** | **32,475,950** |
| | **NAKISI YA BAJETI (ASILIMIA YA PATO LA TAIFA)** | **3.2%** |

*Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango*

## VI. HITIMISHO

**70.** **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyotangulia kusema hapo awali, dhima ya bajeti ya mwaka 2018/19 ni kuendelea **"kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii".** Mageuzi haya ya uchumi wa viwanda yatajengwa kupitia ushiriki wetu katika shughuli za kiuchumi, ubia na kuunganisha juhudi zetu pamoja. Ili kufikia malengo tunayoyakusudia, maamuzi magumu ni lazima yafanyike katika kuelekeza rasilimali chache tulizonazo katika maeneo ya kimkakati. Mabadiliko yoyote ni vigumu kuyakubali na mara nyingi mabadiliko hupingwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla tuunganishe nguvu zetu, vipaji vya wananchi wetu na biashara zetu ili kufikia malengo tunayoyakusudia. Hivyo, tunahitaji uzalendo na nidhamu ya kazi ya hali ya juu tukikusudia kuondoa umasikini, kuongeza ajira na kuwa na uchumi jumuishi.

**71.** **Mheshimiwa Spika,** ili kufikia malengo hayo, Serikali itaendelea kuchukua hatua zaidi kuongeza uzalishaji katika sekta za viwanda na kilimo na ukusanyaji wa mapato ya ndani yatakayowezesha ugharamiaji wa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida na hivyo kupunguza utegemezi. Hatua hizo ni pamoja na: kuvutia uwekezaji; kuelekeza rasilimali kwenye maeneo machache yenye tija; kusimamia utekelezaji wa sheria za kodi; kurasimisha sekta isiyo rasmi ikiwemo usajili wa wamiliki wa ardhi na majengo katika mfumo wa walipa kodi; na kuhimiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika miamala mbalimbali ikiwemo matumizi ya *EFD* na kadi za kielectroniki za benki (*Debt/credit cards*) katika maeneo yanayotoa huduma kama vile katika maduka makubwa, hoteli na vituo vya mafuta. Hivyo, napenda kuwahimiza Watanzania tuwajibike kulipa kodi na kuhakikisha tunatoa na kudai risiti kulingana na muamala uliofanyika. Aidha, Serikali inawashukuru kwa dhati wananchi wote ambao wameonesha uzalendo kwa kuendelea kulipa kodi kwa hiari.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** kipaumbele kikuu cha Serikali ni kujenga uchumi wa viwanda vinavyotumia malighafi

zinazopatikana nchini hususan zinazotokana na kilimo, mifugo na uvuvi ili kupanua fursa za ajira, kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma za jamii (maji, afya, elimu) na kupunguza umaskini. Aidha, Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa, kuimarisha ulinzi wa rasilimali za umma na kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Serikali pia itaongeza msukumo katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*). Mpango huu, pamoja na mambo mengine unakusudia kuhuisha na kurahisisha taratibu za kulipa kodi, tozo na ada mbalimbali.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya tano inalenga kujenga utamaduni na nidhamu ya kukubali maoteo halisia ya ukusanyaji wa mapato ambayo yanapaswa kuwa ukomo wa matumizi (*expenditure ceiling*) badala ya utarabu uliozoeleka wa kuanza kupanga au kuorodhesha mahitaji kwanza. Hivyo, Serikali itajielekeza katika utekelezaji wa miradi michache ya kimkakati kwa namna ambayo itashirikisha sekta zote zinazotegemeana na kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilika kabla ya kuanza miradi mipya.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** mimi ni mpenzi sana wa kujisomea kuhusu maisha na sifa za viongozi mashuhuri, viongozi bora na wa kipekee wa nchi mbalimbali waliofanikiwa kuongoza mabadiliko makubwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika nchi zao kama vile Deng Tsiaoping –Jamhuri ya Watu wa China; Dkt. Mahithir Mohamed – Malaysia; Lee Kuan Yew – Singapore; Park Chung Hee – Korea, Nelson Mandela –Afrika ya Kusini, Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere, Quett Masire – Botswana nk. Nilichojifunza na nilieleza katika hotuba ya bajeti kuu ya Serikali mwaka jana kuwa viongozi wa aina hiyo wana sifa muhimu zifuatazo:

(i) Dira au maono dhahiri kuhusu maendeleo ya nchi zao;

(ii) Hawasiti kutekeleza dira hizo kwa dhamira kubwa tena bila kusita au kubadili msimamo;

(iii) Ni jasiri, shupavu na wenye kuthubutu kutekeleza jambo wanaloliamini bila kigugumizi;

(iv) Wana kipaji cha kujali maumivu ya wanyonge;

(v) Ni waadilifu, wanachukia rushwa na ufisadi na ni wenye nidhamu ya kazi ya hali ya juu;

(vi) Wanaongoza kwa vitendo; na

(vii) Huvumilia magumu ili kuiletea nchi mabadiliko chanya.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** ninapenda niwaambie tena Watanzania kwamba Mwenyezi Mungu ametutunukia kiongozi Mkuu wa nchi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwenye sifa hizo zote nilizotaja. Nilieleza mwanzoni mambo machache ambayo amethubutu kutenda kwa kipindi kifupi kuthibitisha sifa hizo. Rai yangu kwa Watanzania wenzangu ni kuwa tutumie fursa hii adimu kwa kufanya kazi kama njia bora ya kumuunga mkono Rais wetu katika jitihada zake za kuijenga Tanzania mpya, Tanzania ya Viwanda. Jambo hili ni muhimu kwa sababu kama Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alivyotabiri, katika safari ya maendeleo – ya kuelekea kujenga uchumi wa viwanda – kiongozi wetu atakumbana na vikwazo na kelele nyingi za kuzomea kutoka kwa wale wasiotutakia mema ili kutukatisha tamaa tusifikie malengo. Hivyo, Watanzania wote tunao wajibu wa kumtia nguvu Rais wetu ili asirudi nyuma katika safari aliyoianza na aweze kutuvusha kuifikia Tanzania ya viwanda. Niruhusu nimalizie rai yangu kwa nukuu ya mazungumzo ya Mwalimu Nyerere kwa "*TANU study Group*" tarehe 13 Juni, 1967:

"***Maendeleo** na **kazi** ni kitu kile kile, hakuna namna nyingine sisi ya kuendelea, hatukupewa namna nyingine sisi ya kuendelea….. Huwezi kutenganisha vitu viwili hivi, **kuendelea***

*na **kazi,** kwani kazi ndiyo shughuli ya ..... kuondoa matatizo yanayomzuia binadamu hali yake kukamilika.... Hakuna njia nyingine lazima kufanya kazi...... na kila unavyozidi kufanya kazi kwa akili zaidi ndivyo mnavyozidi kwenda, ndivyo mnavyozidi kuendelea,..... Kazi ndio utu ...kazi ndio maendeleo...kazi ndio maisha, ni uhai, kazi ndio civilization, ndio uungwana, ndio kula vizuri, ndio kuvaa vizuri, ndio kuishi katika nyumba nzuri,.... ndio kushinda matatizo yote tuliyo nayo duniani – namna ya kuyashinda ni kazi....”*[1]

**76. Mheshimiwa Spika,** ninapoelekea mwisho wa hotuba hii, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa misaada na mikopo wanayoendelea kutupatia katika kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo nchini. Wahisani hao wanatarajiwa kuchangia jumla ya shilingi bilioni 2,676.6 katika bajeti ya mwaka 2018/19 kama ifuatavyo: Benki ya Dunia/IDA shilingi bilioni 863.13; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) shilingi bilioni 358.63; Global Fund shilingi bilioni 313.90; Sweden shilingi bilioni 179.80; Jumuiya ya Umoja wa Ulaya shilingi bilioni 158.40; India shilingi bilioni 104.57; Ujerumani (Kfw & GIZ) shilingi bilioni 81.31; Japan/JICA shilingi bilioni 76.96; Uingereza/DFID shilingi bilioni 71.21; Denmark shilingi bilioni 69.57; French/AFD shilingi bilioni 61.06; Canada shilingi bilioni 48.84; BADEA shilingi bilioni 40.01; Korea ya Kusini/EDCH shilingi bilioni 39.05; UNICEF shilingi bilioni 36.53; Finland shilingi bilioni 28.08; IFAD shilingi bilioni 26.82; Italy shilingi bilioni 22.05; Norway shilingi bilioni 20.04; Benki ya Uwekezaji ya Ulaya shilingi bilioni 17.88; Uswisi shilingi bilioni 15.74; UNDP shilingi bilioni 12.34 ; Ubelgiji shilingi bilioni 11.08; Saudi Arabia/Saud Fund shilingi bilioni 4.81; USAID shilingi bilioni 4.20; OPEC/OFID shilingi bilioni 2.75; na UNFPA shilingi bilioni 2.56. Ni matarajio yetu kuwa fedha zilizoahidiwa na marafiki zetu hawa zitatolewa kama nilivyozisoma na kwa wakati muafaka.

Sisi kama Serikali tunaahidi kuwa fedha watakazotupatia zitatumika kamailivyokusudiwa.

---

[1] Insha Tatu za Kifalsafa, Julius Nyerere, Kivazi Occassional Papers, No. 3, 2016

**77. Mheshimiwa Spika,** ninakiri kuwa bajeti niliyowasilisha isingekuwa hivi ilivyo bila kupata michango mizuri ya kuboresha kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Sekretariaeti ya Baraza la Mawaziri na wataalam wa wizara zote na taasisi za Serikali. Ninatoa shukrani kwa kila mmoja wenu kwa michango mliyotoa katika mchakato mzima wa maandalizi ya bajeti hii.

**78. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango, nikianza na Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji, Mbunge wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, pia Bwana Dotto M. James, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, na Naibu Makatibu Wakuu, Bibi Amina Kh. Shaaban, Dkt. Khatibu M. Kazungu, na Bibi Susan B. Mkapa. Wote hawa kwa pamoja wamenipatia ushirikiano na msaada wa hali ya juu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na wameratibu vizuri maandalizi ya bajeti hii. Aidha, ninampongeza Profesa Florens Dominick Makinyika Luoga kwa kuteuliwa na Rais kuwa Gavana mpya wa Benki Kuu ya Tanzania na kwa kusimamia vema majukumu makubwa ya mhimili huo wa sekta ya fedha akisaidiwa na Naibu Gavana watatu, Wakurugenzi na watumishi wote wa Benki Kuu ya Tanzania. Vivyo hivyo, napenda kutambua kazi nzuri ya viongozi na watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kukusanya mapato ya Serikali wakiongozwa na Bw. Charles E. Kichere, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Profesa Musa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Dkt. Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa yaTakwimu. Aidha, nampongeza Bwana Athumani Selemani Mbuttuka aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni kuwa Msajili wa Hazina (*Treasury Registrar*).

**79. Mheshimiwa Spika,** vile vile, ninawashukuru Wakuu wengine wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ikijumuisha Mabenki (TADB, TIB-DFI, TIB- CBL,TPB Bank); Mifuko ya hifadhi ya jamii (PSPF, GEPF, PPF); Rufani za kodi (TRAB, TRAT); Huduma za bima (TIRA,NIC); Mitaji na dhamana (CMSA,

TCEM, DSE); Dhamana za uwekezaji (UTT-MFI, UTT-AMIS,UTT-PID); Bodi ya michezo ya kubahatisha; Taasisi za mafunzo (IFM, IRDP, IAA, TIA, EASTC); na Mfuko wa huduma ndogo za fedha (*SELF Microfinance Fund*). Nawashukuru pia Wakuu wa Idara na Vitengo, bila kuwasahau wataalam, makatibu muhtasi, watunza kumbukumbu, madereva, wahudumu na walinzi wa Wizara yetu na taasisi zake kwa kazi kubwa walizofanya katika mwaka 2017/18 na katika kukamilisha Bajeti hii.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** nashindwa kumaliza hotuba hii bila kumtaja mke wangu na rafiki yangu mpenzi Mbonimpaye. Moyo wake wa ibada kwa Mungu na uaminifu wake vimekuwa ndiyo nguzo yangu kuu katika utumishi wangu. Ninamshukuru sana yeye pamoja na watoto na wajukuu wetu wote tuliopewa na Mungu na familia nzima. Aidha, ninawiwa kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania (wakulima, wafanyakazi, na wafanyabiashara). Ninawashukuru sana kwa uzalendo wao wa kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Ninawashukuru pia wanafunzi wote wa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo wanaosoma kwa bidii maana miongoni mwao tutapata viongozi na nguvukazi bora ya Taifa. Ninawashukuru pia Wazee wetu ambao walitoa mchango mkubwa kwa Taifa letu katika umri wao wa kufanya kazi. Aidha, siwezi kuwasahau wananchi wa wilaya za Buhigwe na Kasulu, na mkoa wetu wa Kigoma kwa ujumla. Ninyi ni fahari yangu maana mlinikuza. Ninawapenda! Vile vile ninawashukuru wananchi wenzangu wa Nzinje hapa Dodoma (Zuzu kwa jina la zamani), kwa kunipokea vizuri mimi na familia yangu.

**81.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa inatarajiwa leo itakuwa siku ya mwisho wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan, naomba nihitimishe hotuba hii kwa kuwatakia Waislamu wote Eid Mubarak.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** nimalizie kwa kusema ASANTE SANA MUNGU" kwa Baraka zako zilizoniwezesha kukamilisha kusoma hotuba hii. Na kwenu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote …….

(i) "SANDENYI SANA"!
(ii) "NGW'ABHEJA SANA"
(iii) "WAITU MWAKORA"
(iv) "OKORREE BHUYA"
(v) "HAIKENI SANA"
(vi) "MSENGWILE"
(vii) "NDAGHA FIJO"
(viii) "HEWELA"
(ix) "KAJEKAJE"
(x) "MURAKOZE CHANE"
(xi) "ASANTENI SANA"

**83.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, *Murakozee*. Tunakushukuru sana kwa hotuba hii nzuri kabisa iliyochukua saa moja na robo tatu, yenye matumaini makubwa sana kwa Watanzania. Sasa kwa robo saa hii niweke mambo sawa ili tuweze kuelewana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, alichokuwa akikisoma Mheshimiwa Waziri ni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi. Kwa hiyo, bado haya ni mapendekezo ya Serikali, maana wengine kwenye magazeti kesho wataanza kuandika vitu vyao. Ni mapendekezo kwa sababu ya Kanuni yetu lakini kuanzia Jumatatu tunaanza kujadili haya mapendekezo tarehe 18 kwa siku saba, kufuatana na Kanuni yetu. Kwa hiyo, itakapofika Jumanne inayofuata, nadhani itakuwa kwenye tarehe 26 kama sijakosea lakini itakuwa siku ya Jumanne ndiyo siku ambayo tutapiga kura sasa kupitisha rasmi jambo hili ambalo limewekwa mbele yetu hapa tulipo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo ya kwa kifupi sana niende kwenye kuwatambulisha wageni wetu, kama mtakavyoona Waheshimiwa Wabunge *gallaries* zetu zote zimejaa kabisa. Wageni wetu wote tuwashukuru sana kwa kufika siku ya leo, kama nitakosa kumtambulisha yeyote miongoni mwenu msikasirike, ni kwa sababu ya wingi wa wageni tulionao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo haya ya Serikali ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kazi hii inatafsiri ahadi zilizomo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa maana hiyo, Chama cha Mapinduzi wamekuja hapa kushuhudia wakiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM - Taifa, Dkt. Ally Bashiru Kakurwa. Naomba nimtambulishe pale alipo asimame. Karibu sana Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Karibu sana Bungeni na unashuhudia nguvu ya CCM humu ndani. *(Makofi/Vigelegele)*

Pamoja naye ameongozana na Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Bara), Ndugu Rodrick Mpogoro. Sasa sikilizeni vizuri hii, pia Katibu Mkuu ameongozana na Katibu wa *NEC* Itikadi na Uenezi, Ndugu Humphrey Polepole. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, wanasema Mheshimiwa Polepole hujaonekana, uko wapi? Mheshimiwa Polepole. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Katibu wa *NEC Organisation,* Ndugu Pereira Silima; Katibu wa *NEC* Uchumi na Fedha, Dkt. Frank George Haule, kipekee kabisa yuko Katibu Mkuu wa UWT, Ndugu Queen Mlozi. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuwatambulisha wageni wetu wapendwa, tunaye Katibu Mkuu Kiongozi Balozi John Kijazi; Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Ndugu Binilith Mahenge; na Meya wa Jiji la Dodoma Profesa Davis Mwamfupe. *(Makofi)*

Pia, tunayo familia ya Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango wakiongozwa na mke wa Mheshimiwa Waziri Ndugu Mbonimpaye Mpango. Yupo pia mtoto wa Waziri Christina Mpango, mjukuu Angellah Mpango, yupo pia Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe ambaye anakaimu kule Kasulu Brigedia Jenerali Marco Gaguti. Pia yupo Mshauri Mkuu wa Mkurugenzi wa Benki ya Dunia Kanda ya Afrika Dkt. Zarau Wendeline. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa naenda kwenye Hapa Kazi Tu, Viongozi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Tunaye Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Venance Mabeyo. Jamani mmenuna hata Jenerali wetu wa Ulinzi naye mmenuna tu jamani? Eeh, namna hiyo jamani, eeh! *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Tunaye Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Dkt. Modestus Kipilimba, *Inspector General* wa Polisi (*IGP)* Simon Sirro, hapo je?

**WABUNGE FULANI:** Sawa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, yupo Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Ndugu Valentino Mlowola; Kamishna Jenerali wa Magereza, Dkt. Juma Malewa; Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Martin Busungu; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji mwanamama, Dkt. Anna Makakala. *(Makofi)*

Pia, yupo Mwakilishi wa Kamishna Jenererali wa Jeshi la Zima Moto na Ukoaji ambaye ni Kamishna Bili Mwakatage. Pia yupo Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ndugu Rogers Siang'a. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Watendaji Wakuu ambao ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Ndugu Doto James; Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Ndugu Charles Kichere; Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Profesa Florens Luoga; na *CAG,* Profesa Mussa Assad. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mhasibu Mkuu wa Serikali, Ndugu Francis Mwakapalila; Msajili wa Hazina Ndugu Athumani Mbuttuka; Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, Ndugu Ramadhani Kailima. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane jamani.

**WABUNGE FULANI:** Rudia.

**SPIKA:** Namtambulisha kwenu Mkurugenzi wa Uchaguzi, Ndugu Ramadhani Kailima. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hii, hii, hii, hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, tusikilizane. Mkurugenzi wa Uchaguzi sijakuona, kama Spika.

**WABUNGE FULANI:** Hii, hii, hii, hii.

**SPIKA:** Ndugu Ramadhani Kailima ni huyo. *(Makofi/ Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mwizi huyoo, mwizi huyo.

**SPIKA:** Ahsanteni sana. (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Hii, hii, hii, hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naendelea na wageni wengine ambao ni Katibu wa CCM wa Mkoa wa Dodoma, Ndugu Jamila Yusuph; Mjumbe wa *NEC* wa Mkoa wa Dodoma, Ndugu Ismail Jama; Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dodoma, Ndugu Godwin Mkanwa; Mwenezi wa Mkoa wa Dodoma, Ndugu Henry Msunga, Mjumbe wa *NEC* kupitia kundi la vijana, Ndugu Mussa Mwakitinya; Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma, Ndugu Robert Mwinje; Katibu wa CCM wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Ndugu Pili Augustino; Katibu wa Umoja wa Vijana Mkoa wa Dodoma, Ndugu Asia Halamga; Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Ndugu White Zubeir; Katibu wa CCM Wilaya ya Kongwa, Ndugu Mfaume Kizigo; Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa, Ndugu Omari Nkulo; pia kuna wageni kutoka Kongwa Ustaadhi Yahya Kandoro, Mchungaji Luznet Kingamkono na Ndugu Julius Lepuhma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao Mabalozi wa kutoka katika nchi mbalimbali na Taasisi za Kimataifa ambao ni Balozi wa Norway Hanne Marie Kaarstad (*Norwegian Ambassador),* ahsante sana. Balozi wa Ujerumani Dkt. Watche Ditif, ahsante Balozi wa Ujerumani. Yupo Balozi wa Uingereza Sarar Cooke. Waheshimiwa mbona kelele nyingi? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Rudia hatujasikia.

**SPIKA:** Hata nilipomtambulisha Balozi wa Ujerumani hampigi makofi, inakuwaje? *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Balozi wa Zambia Charlie Benson Keith; Balozi wa Denmark, Ndugu Jensen Einar Hebogard; Balozi wa Afrika Kusini, Ndugu Thami Mseleku; Kaimu Balozi wa Kenya, Ndugu Muhia Boniphace; Kaimu Balozi wa Marekani, Dkt. Inmi Patterson; Kaimu Balozi wa Burundi, Ndugu Prefere Ndayishimiye; Kaimu Balozi wa Angola, Ndugu Joel Kuvuna; Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *UNDP,* Ndugu Alvaro Rodriguez; na Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia, Ndugu Bella Berd. *(Makofi)*

Pia, tunao Makatibu Wakuu wa Wizara Mbalimbali, Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *Development Partners* wote mliopo karibuni; wawakilishi wa wazee wa Mkoa wa Dodoma karibuni; Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dodoma wako hapa; Viongozi wa Dini Mkoa wa Dodoma mpo na karibuni sana; Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Fedha mliopo, wote karibuni; Wakuu wa Taasisi za Elimu ya Juu za Mkoa wa Dodoma; Wawakilishi wa Wakfu wa Sekta Binafsi Tanzania; na Mwakilishi wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina Mwakilishi sikuweza kumtambulisha mapema, lakini tunaye Mwakilishi wa Msajili wa Vyama ya Siasa, pale alipo asimame. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hii, hii, hii, hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii ni ofisi muhimu sana ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

**WABUNGE FULANI:** Hii, hii, hii, hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangaze Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, mara tu tukiahirisha shughuli hizi wageni wetu wote mliopo, Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge wote tumeandaa futari ya pamoja katika uwanja wetu wa kawaida, nyuma ya Jengo la Utawala pale. Tunaomba sote Waheshimiwa tukachanganyike na wageni wetu kutoka sehemu mbalimbali ili tuweze kupata futari hii ya pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hapo mwanzo, kuanzia Jumatatu tutaanza mjadala wa hoja hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa siku saba. Kwa maana hiyo, tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Ashatu Kijaji na timu yote ikiongozwa na Katibu Mkuu kwa kweli, kwa kazi kubwa ambayo mmekuwa mkifanya na Mmekesha nasi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema mwenyewe wakati mwingine tumewasema, lakini tunawashukuru ninyi ni watu wapole mnatuvulimia sana. Sasa aliyekaa kwenye kihenge anafikiri atakaa kwa amani, hawezi kulala kwa amani, lazima tu na hasa kwenye nchi kama ya kwetu ambayo tunanyang'anyana rasilimali chache, lazima tu itakuwa inakuwaje, inakuwaje? Unahisi kama aliye karibu na ugali anamega tonge kubwa, kumbe sio lazima. Kwa hiyo, tunakupongeza sana na tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kumbe leo wamebadilisha kwa sababu pale ni padogo kwa futari, kwa hiyo, futari itakuwa kwenye *car park* karibu na jengo la zahanati yetu mpya huku, siyo kule kwa siku zote kwa sababu lile eneo ni pana zaidi linaweza kuchukua wageni wote hawa, kwa hiyo, tuonane pale.

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, mwisho kabisa na mimi niwatakie sikukuu njema ya Iddi, vyovyote itakavyokuwa iwe kesho au keshokutwa, niwaambie kabisa *Eid Mubarak.* Kwa wale mtakaosafiri kwenda nje ya Dodoma tunawaomba muende taratibu, muwaambie madereva wetu waendeshe kwa uangalifu mkubwa, hasa wakati huu wa sikukuu barabara zetu zinakuwa kidogo hatari, magari ni mengi watu wengi wanasafiri, wale watakaobaki Dodoma basi tunawatakia Sikukuu njema ya Iddi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo basi, naahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu, tarehe 18, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.05 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 18 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*